**19 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 19 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Ally Makoa.

Na. 371

### Ujenzi wa Shule ya Bweni ya Wasichana – Kondoa

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule ya Bweni ya Wasichana katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Kondoa tayari ina shule moja ya wasichana ya Serikali inayoitwa *Kondoa Girls*. Shule hii ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 660. Kwa sasa shule ina wanafunzi 572 wa kidato cha tano na sita na Halmashauri imeomba kuongezewa mchepuo wa *HGE* ili iweze kutumika kwa *full capacity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuongeza shule za bweni za wasichana kulingana na uhitaji na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu ya Serikali, *Kondoa Girls* hii ilikuwa ni Shule ya Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne, lakini Serikali ilifanya maamuzi ya kuibadilisha kuwa Kidato cha tano na sita na ikawaondoa wale wa *O'level.* Sasa Kondoa bado tuna uhitaji wa Sekondari ya Bweni ya Wasichana: Je, ni lini Serikali itairudishia sekondari ambayo waliichukua kujengea sekondari ya wasichana ya bweni ya *O'Level?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wananchi wa Kata ya Bolisa wana hamu ya kuona sekondari yao ya kata inaazwa kujengwa, na tayari kama Halmashauri ya Mji tulipokea barua ya mapokezi ya fedha: Sasa ni lini Serikali italeta fedha ili wananchi wa Bolisa waanze kujenga sekondari yao ya kata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Makoa, kwanza kutokuwa na shule ya bweni ya wasichana katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa, Serikali kwa sasa inaweka nguvu katika kuhakikisha kila mkoa unapata shule moja ya wasichana

ya bweni ambayo ni kubwa itakayoweza kuchukua watoto katika mkoa husika na tayari shilingi bilioni 30 ilikuwa imeshatengwa, ambapo shule 10 katika mikoa 10 zimeshajengwa na tunaenda kwenye *Phase II* ambapo tutajenga tena shule tano. Vilevile tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuona Kondoa nao wanapata shule ya bweni ya wasichana ya Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne kadiri ya bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la Kata ya Bolisa kupata shule yao ya sekondari, nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imeshakamilisha michakato yote ya kuweza kupeleka fedha katika Halmashauri zote 184 nchini kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari. Muda siyo mrefu Halmashauri hizi 184 zitapata fedha hii kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ikiwemo Kata ya Bolisa kule Halmashauri ya Kondoa Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Wizara hiyo hiyo.

Na. 372

**Serikali kukamilisha ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa majengo yaliyobaki ya Kituo cha Afya Mlimba utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Jimbo la Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi mbili; jengo la upasuaji na nyumba ya mtumishi katika Kituo cha Afya Mlimba. Ujenzi wa majengo hayo umekamilika na kwa sasa kituo kinatoa huduma katika ngazi ya kituo cha afya ikiwemo huduma za upasuaji wa dharura wa akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakamilisha ujenzi wa majengo yaliyobaki ya Kituo cha Afya Mlimba, kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa haya majengo yanayoelezwa yamejengwa kwa nguvu za wananchi na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri: Ni lini Serikali kwa maana ya Wizara ya TAMISEMI itapeleka fedha kukamilisha majengo haya yaliyobaki; jengo la maabara, jengo la mochwari na jengo la mganga? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, kwanza nipongeze jitihada za wananchi wa Mlimba kwa kuweza kujenga kituo hiki cha afya kwa shilingi milioni 500. Serikali kwa sasa itatafuta fedha kadiri ya bajeti itakavyoruhusu ili tuweze kwenda kujenga maabara, mochwari na nyumba ya mganga. Tayari Mheshimiwa Mbunge hili alikuwa amekuja kulifuatilia na tunaona uwezekano wa upatikanaji wa hizi fedha katika bajeti ya mwaka huu tunaoenda kuanza 2023/2024. Kama ikikosekana hapo, basi tutenge katika mwaka 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Sigula.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya cha Ngongowele kilipata fedha za Matokeo Makubwa Sasa, tulipata shilingi milioni 250, mradi ambao umeshaisha; je, Serikali haioni imefika wakati kutupatia shilingi milioni 250 nyingine kumalizia kituo kile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kituo hiki cha afya cha Ngongowele kule katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Serikali itatenga fedha ya kumalizia kadiri ya upatikanaji wa fedha hizi na bajeti itakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigula.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tangu mwaka 2010 tuliahidiwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Nyarubanda, lakini zaidi ya miaka 12 mpaka leo ujenzi haujaanza: Nataka kujua, ni lini hasa ujenzi huo utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huu katika Kata ya Nyapanda utaanza kadiri ya upatikanaji wa fedha. Tutaangalia katika bajeti hii ambayo inakuja ya 2023/2024 kama haijatengewa, basi tutaangalia kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Na. 373

**Serikali kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA K.n.y. MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kukarabati Vituo vya Afya ili kuendana na utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango na mikakati madhubuti ya kujenga na kukarabati vituo vya afya nchini ambapo katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 jumla ya Shilingi bilioni 118 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya 236 katika Kata za kimkakati nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha huduma ya Afya nchini, kiasi cha Shilingi bilioni 8.75 kimetengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vipya 15 na ukamilishaji wa vituo vya afya vitano. Vituo hivi vya afya vinapaswa kutoa huduma kwa wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* pamoja Mfuko wa Afya wa Jamii ulioboreshwa *(iCHF)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei. Je, lini Serikali itakarabati kituo cha Mwika Kaskanzini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika maeneo ambayo kuna zahanati, lakini maeneo ni madogo: Je, Serikali ipo tayari kupandisha zahanati za Rombo kuwa vituo vya afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza; la kwanza kuhusu lini Serikali itafanya ukarabati wa katika Kituo cha Afya cha Mwika, Serikali itafanya ukarabati katika kituo hiki cha afya kadiri ya upatikanaji wa fedha. Tutaangalia katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama kimetengewa fedha ya ukarabati, basi tutahakikisha fedha inaenda mara moja. Kama hakijatengewa fedha kwenye mwaka huu wa fedha, tutahakikisha katika mwaka wa fedha 2024/2025 Kituo cha Afya cha Mwika kinatengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali la pili la kupandisha hadhi zahanati kuwa kituo cha afya katika eneo la Rombo, tunalipokea hili kama Serikali. Nichukue nafasi hii kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kufika katika zahanati hizi ambazo zimetajwa na kuangalia kama zinakidhi vigezo vya kupandishwa kuwa vituo vya afya na kuwasilisha taarifa hii katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuona ni namna gani tunawasaidia wananchi wa maeneo haya kupata vituo vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Anton Mwantona.

Na. 374

**Bajeti ya TARURA kuzingatia mitandao ya barabara katika Halmashauri**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha Bajeti ya *TARURA* inazingatia mitandao ya Barabara katika Halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la msingi la *TARURA* ni kuhakikisha kuwa bajeti inayotengwa inaendana na mtandao wa barabara zilizopo katika Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kendelea kutekeleza jukumu hili, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya barabara ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 kiasi cha shilingi milioni 962.48 kilitengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kumekuwa na ongezeko la bajeti ambapo shilingi bilioni 2.31 zimetengwa kwa ajili ya kazi za barabara katika Wilaya ya Rungwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantona.

**MHE. ANTON A. MWANATONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini maana yangu hasa ilikuwa mgawanyo wa fedha za *TARURA* kwa kuzingatia mtandao wa barabara katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, ukichukua Mbeya peke yake, Rungwe ni ya pili. Mbeya Vijiji ya kwanza, mtandao

mkubwa kama kilometa 1,000 na Rungwe inafuata, lakini bajeti tunayopata ni ndogo kuliko Halmashauri nyingine. Kwa hiyo, naomba Serikali ituambie ni vigezo gani vinatumika kugawanya hizi pesa za barabara katika Halmashauri zetu, kwa mfano, utakuta Halmashauri ina kilometa nyingi zaidi, lakini inapata fedha chache?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mwaka jana 2022 Mheshimiwa Rais alitembelea Rungwe akaahidi kutoa kilometa mbili za lami pale Mji wa Tukuyu: Je, ni lini fedha hizo zitakuja ili mradi huo wa barabara ya kilometa mbili za lami uweze kutekelezwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantona, la kwanza hili la vigezo vya mgawanyo. *TARURA* ilipokea vigezo vilevile vilivyokuwepo awali kabla ya taasisi hii kuanzishwa ambapo vilikuwa vimetengenezwa na *Road Fund* nchini kuweza kuwapelekea fedha Halmashauri mbalimbali. Baada ya *TARURA* kuanzishwa, changamoto hii Serikali imeiona na tayari Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Angellah Kairuki alielekeza *TARURA* kufanya tathmini na kuona ni namna gani fedha inaweza ikapelekwa kulingana na barabara ambazo zipo na ukubwa wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari kazi hiyo ilikuwa imeshafanyika na baada ya kazi hiyo kufanyika, sasa kuna *independent team* ambayo imepewa ku-*verify* tu, kuona. Vigezo ambavyo vitatumika sasa, ni kuona urefu wa barabara, kuangalia ukubwa wa eneo husika, vilevile kuangalia milima, wingi wa mvua, *agri-connect* katika maeneo hayo shughuli za kilimo zinafanyika kiasi gani, na kadhalika kuweza kutoa fedha ya kwenda kwenye barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la pili la nyongeza la kilomita mbili ambazo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan hii tutaendana kadiri ya upatikanaji wa fedha kuweza kukamilisha ahadi hii. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za Dkt. Samia Suluhu Hassan huwa zinatekelezeka kwa wakati, na tayari tutaangalia katika bajeti ya mwaka huu kupitia Taasisi ya *TARURA* kuona ni nini kinaweza kikatengwa ili ahadi hii ianze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu aliyoyatoa, naomba kuuliza swali kwamba, Jimbo la Njombe Mjini ambalo ndiyo Halmashauri kubwa kuliko Halmashauri zote katika nchi hii; je, litaangaliwa kwa namna ya kipekee katika hiyo tathmini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Njombe Mjini na maeneo mengine yote ya nchi yetu ya Tanzania ambayo Waheshimiwa Wabunge mnatokea, yataangaliwa kwa vigezo vile vile ambavyo nimevitaja hapa. Ukubwa au urefu wa barabara katika wilaya husika, kuangalia ukubwa wa eneo husika, kuangalia milima, kuangalia wingi wa mvua, kuangalia shughuli za kiuchumi kama kilimo…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa ameshakuelewa. Mheshimiwa Getere, jiandae Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda kuuliza, hivi ni lini Serikali itaamua kutengeneza mikataba ya Kiswahili katika utengenezaji wa barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Mheshimiwa Getere, niseme tunalichukua na tutaangalia ni namna gani tunaweza tukaboresha na kuwa na mikataba ya Kiswahili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niulize swali la nyongeza. Pamoja na kwamba Mji wa Tabora unaitwa Toronto kwa sababu ya ubora wake, lakini kuna kata nyingi ambazo zina shida pale mjini kwenye barabara, hasa Kata ya Ng'ambo, Kata ya Isevya, Kata ya Kitete, na kata nyingine; je, Serikali lini ita…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Mwakasaka ukidandia swali huanzi tena umaarufu humu ndani, haya Mheshimiwa Waziri. Kaa chini Mheshimiwa Mwakasaka.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Barabara kadri upatikanaji wa fedha hizo katika Kata za N'gambo, Isevya na Kitete katika Manispaa ya Tabora Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mbunge wangu wa Jimbo la Rungwe ameuliza swali la msingi tukizingatia Wilaya ya Rungwe ina mvua nyingi na ina mtandao mkubwa sana. Ninaomba kuhakikishiwa kwa sababu yeye ndiye swali lake Mbunge wangu ameuliza ni lini mtatutengenezea hizo Barabara za *TARURA* na kutupatia fedha za kutosha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nimeishasema kwenye majibu yangu ya msingi ukiangalia mwaka wa fedha 2020/2021 *TARURA* katika Halmashauri ya Wilaya Rungwe ilikuwa imetengewa milioni 962 tu lakini mwaka huu wa fedha tunaoenda kuutekeleza *TARURA* inatengewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.31 katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunakwenda kutekeleza barabara nyingi zaidi kuliko hapo awali na hiyo ndiyo azma ya Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. tunaendelea Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Londo.

Na. 375

**Watumishi wa umma waliofikishwa mahakamani kwa rushwa**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza:-

Je, ni watumishi wangapi wa umma wamefikishwa Mahakamani kwa rushwa, wangapi wameshinda kesi na kurejeshwa kazini kwa kipindi cha 2010 – 2020?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010 mpaka 2020, jumla ya Watumishi 2,060 walifikishwa Mahakamani na kushtakiwa kwa makosa mbalimbali ya rushwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 ya Sheria za Tanzania. Kati ya watumishi hao 2,060 walioshtakiwa, watumishi 1,157 walitiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu mbalimbali kwa mujibu wa sheria, huku watumishi 863 wakishinda kesi na kuachiwa huru waendelee na kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini tunazungumzia maisha ya watu kwa idadi ya watu 863 ambao wameonekana hawana hatia ni asilimia 41.8 ni watu wengi sana katika utendaji wa umma na watu hawa wamepitia mateso, wamedhalilika katika jamii ambayo tunaishi ambapo tuhuma tayari ni uhalifu sasa swali. Serikali inachukua jitihada gani kuwasafisha watumishi ambao wamepelekwa Mahakamani kwa tuhuma za rushwa asilimia 41.8 wameoneka hawana hatia kutumia nguvu ile ile ya kuwatangaza ni wahalifu, wanatumia nguvu gani kuwasafisha watumishi hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa madhara ni makubwa ya kisaikolojia, kijamii na haiba yao imechafuka kwenye macho ya umma. Kwa muda gani Serikali itaendelea kuvumilia kuwaona watumishi hawa wanaendelea kuhangaika na nini jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba wanarudi katika utumishi wakiwa wana haiba njema na safi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Dennis Londo utaratibu wa utumishi wa umma umeelezwa ndani ya sheria kama nilivyozitaja pamoja na sheria nyingine lakini pia utaratibu wa kuwarudisha watumishi kazini nao pia umeelezwa katika sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Dennis Londo utaratibu wa kuwaandikia wale ambao wamekwisha safishwa na Mahakama na kuonekana kwamba hawana makosa utaendelea kufanyika. Pamoja na hilo pia Mheshimiwa Rais, ameelekeza na ndiyo tunayo yafanyia kazi kwamba lazima tuhakikishe kwamba hawa watu ambao wanakutwa hawana makosa tunawafanyia haki la kwanza, lakini pili wanarudishwa kazini mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo lote Mheshimiwa Rais ameendelea kuhakikisha kwamba kupitia Tume yake wa Utumishi wa Umma taratibu na haki zote wa watumishi hawa zinafuatwa na kusimamiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Makamu wa Rais, Muungano Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli.

Na. 376

**Kutoa elimu ya utunzaji mazingira kwa wananchi**

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO K.n.y. MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inawapa elimu ya utunzaji mazingira wananchi wanaofanya shughuli za kilimo katika vyanzo na njia za mito ili wafanye kilimo bila kuleta athari za mazingira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha mpango mkakati wa kutoa elimu kwa umma wa miaka mitano na lengo la mpango mkakati huu ni kuhamasisha umma wa Tanzania kuhusu maendeleo endelevu pamoja na uhifadhi wa mazingira. Mkakati huu umehusisha namna ya utoaji elimu kuhusu matumizi ya ardhi ndani ya mita 60 katika maeneo ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, licha ya Serikali kuruhusu wananchi kufanya shughuli za kilimo kwa umbali wa mita 60 katika maeneo ya vyanzo vya maji, bado kuna changamoto nyingi za uharibifu mkubwa wa mazingira. Hivyo, naomba nichukue fursa hii kuwaomba viongozi wenzangu wa siasa tutumie uwezo wa kuwashawishi na kuhamasisha jamii zinazofanya shughuli za kiuchumi katika maeneo ya vyanzo vya maji na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkumbo.

**MHE. PROF. KITILA. A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu hilo kwa umakini huo ambao ameonyesha Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye jibu lake.

Je, lini atakuja kwenye Mtaa wa Kibangu Kata ya Makuburi ili kushughulikia changamoto ya uchafuzi wa mazingira kutoka kwenye Viwanda vya *EPZA?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nipo tayari kwenda kuona uharibufu ambao umefanyika huko na badala ya hapo kukaa na wamiliki wa viwanda hao na kuwaeleza namna bora ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa wananchi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Ahmed Salum.

Na. 377

**Kukamilisha ujenzi wa Skimu Umwagiliaji – Ishololo Shinyanga**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. AHMED A. SALUM** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Kata ya Ishololo wilayani Shinyanga utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K. n. y WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Jimbo la Solwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Ishololo wenye ukubwa wa hekta 600 ni mojawapo ya miradi ambayo ilikuwa ikitekelezwa kupitia mpango wa kuendeleza kilimo wilayani *(District Agricultural Sector Investiment* Projects). Kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)*. Ufadhili wa mpango huu ulifikia kikomo tarehe 31/12/2013 kabla ya mradi huo kukamilika. Wakati mpango wa utekelezaji wa *DASIP*

unafikia kikomo, Utekelezaji wa Mradi wa Ishololo ulikuwa umefikia aslimia 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya mapitio ya usanifu katika mradi wa Ishololo ili kupata gharama halisi za kukamilisha mradi huo. Ukarabati wa mradi huo utapangwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa mradi huu ulianza 2012 na 2013 mkandarasi akaondoka na gharama yake ni takribani bilioni 1.4 je, Serikali inatoa ahadi gani kwa wakazi wa Ishololo Usule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa mradi huu ni muhimu sana kwa wananchi wa Ishololo Kata ya Usule je, Waziri uko tayari kutembelea mradi huu ukaone ni jinsi gani wananchi wa Ishololo – Usule wanauhitaji wa mradi huu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Waziri yuko tayari kufika katika eneo la Ishololo – Usule ili kujionea hali halisi ya huo Mradi. *Commitment* ya Serikali ni kama katika jibu la msingi lilivyoandikwa kwamba katika mwaka wa fedha huu unaokuja 2023/2024 tutafanya tathimini na utekelezaji wa huu mradi utaanza 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

Na. 378

**Hitaji la mbegu mpya za migomba**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mbegu mpya za migomba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali kupitia Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha *TARI* – Tengeru imefanikiwa kutumia teknolojia ya chupa *(Tissue Culture)* katika kuzalisha mbegu bora aina ya *TARIBAN* 1, *TARIBAN* 2, *TARIBAN* 3, *TARIBAN* 4, *FHIA* 17 na *FHIA* 23 ambayo ina ukinzani dhidi ya magonjwa (Madoa meusi na *Panama (banana wilt)* ambayo yamekuwa yakiathiri tija na uzalishaji wa zao la migomba. Uzalishaji wa miche hiyo pia unafanyika kupitia vituo vya utafiti vya *TARI* – Uyole na *TARI* – Maruku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 jumla ya miche 30,000 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika Mikoa ya Kilimanjaro miche 5,000, Kigoma miche 9,000 na Kagera miche 9,000. Uzalishaji na usambazaji wa miche hiyo unaendelea ili kuwafikia wakulima katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Arusha na maeneo mengine yenye fursa ya uzalishaji wa zao la migomba ili kuwezesha wakulima kupanda mbegu bora za migomba na hivyo kuongeza tija na kipato cha mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa mwaka 2023/2024 Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania imepanga kushirikiana na maabara binafsi za *Crop Bioscience* na maua mazuri kuzalisha na kusambaza takribani miche 1,500,000 ya migomba aina ya *Grand Nain* ambayo itasambazwa kwa wakulima wakiwemo wakulima wa mkoa wa Kilimanjaro.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa naomba nimtaarifu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hiyo miche ya migomba Hai haijafika kwa hiyo niombe sasa *commitment* ya Serikali kwa kuwa zao hili ni zao muhimu sana katika Jimbo la Hai ni lini mtatuletea miche mipya ya migomba kuondoa changamoto tuliyonayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa zao la mgomba linaenda sambamba na zao la vanila lakini zao la vanila kwa sasa bei imeshuka sana ukilinganisha na ile ya Dunia sasa hivi kilo moja ni shilingi 20,000 lakini inatokana na mazao yanayotokana na vanila inayotoka nje ya nchi yanakuja kwa wingi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia mazao ya vanila yanayotoka nje ya nchi ili zao hili liweze kuongezeka bei hapa Tanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kwa kuwa sasa hivi Serikali inaendelea na utaratibu wake wa teknolojia ya chupa kwa maana ya *tissue culture* kwenye zao la mgomba kama ambavyo ameeleza na anataka commitment ya Serikali kwenye kupeleka miche hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu kwamba Serikali itapeleka kulingana na mahitaji ya eneo husika, kwa hiyo kusema lini *exactly* kwa wakati huu hatuwezi kutaja moja kwa moja lakini

tuwahakikishie wananchi wa Hai kupitia Mbunge wao Serikali itapeleka miche katika baadhi ya maeneo ya Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vanila ni kwamba tumechukua wazo la Mheshimiwa Mbunge Serikali itafanya tathimini ili kuweza kusaidia zao hilo la vanila.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali la nyongeza. Kumekuwa na hasara kubwa kwa wakulima wa migomba kwa sababu ya ugonjwa wa mnyauko. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanatokomeza ugonjwa huu ili wakulima wa migomba wapate faida? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mkakati wa Serikali ndiyo pamoja na hizi tafiti ambazo zinafanyika za kuja na aina mpya ya mbegu ambayo itakuwa na uwezo wa kukabiliana na magonjwa mnyauko na huo ndiyo mkakati sahihi kwa sasa, kwa hiyo tuwahakikishie tu wananchi kwamba Serikali ipo kazini ili kuondoa hii adha ya wakulima ususani katika zao la mgomba.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Khenani.

Na. 379

**Kuwapatia Wavuvi Wa Ziwa Tanganyika Zana Za Kisasa**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wavuvi wa Ziwa Tanganyika zana za uvuvi za kisasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto za wavuvi zilizopo ikiwemo ukosefu wa zana za kisasa za uvuvi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga fedha kwenye programu maalum ya mikopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* kupitia dirisha la *extended credit facilities (ECF)* kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi boti za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango huo, Serikali inakamilisha taratibu za kutoa boti 158 kwa mkopo kupitia Benki ya Kilimo *(TADB)* kwa Vyama vya Ushirika 45, Vikundi vya Wavuvi 71 na watu binafsi 43. Aidha, katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika jumla ya Vyama vya Ushirika vinne, Vikundi vinne na watu binafsi watano wanatarajiwa kunufaika na mikopo wa boti hizo usiokuwa na riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali kupitia *TADB* inatoa mitaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi ili kuboresha shughuli zao za maendeleo. Aidha, Serikali inawahimiza wavuvi kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika vya msingi, *SACCOS* na *VICOBA* ili waweze kukopesheka na kuweza kununua zana na vyombo bora vya uvuvi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nimesikiliza majibu ya Serikali na kwa takwimu

alizozitoa Naibu Waziri ni wazi kabisa kwamba bado atujawa na dhamira ya dhati ya kuwasaidia wavuvi wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu ni mkakati upi wa Serikali kwa sasa kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wa Ziwa Tanganyika kwa sababu na ninyi mmekili kuna changamoto ya zana ya kisasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanakabiliana na changamoto nyingi ikiwemo utitiri wa leseni lakini changamoto ya vizimba pamoja na changamoto ya kanuni zilizopo. Mheshimiwa Waziri uko tayari kwenda kukutana na wavuvi uwasikilize ili mtakapo kuja na kauli au na utekelezaji uendane na uhalisia wa Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu spika, ahsante sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwanza niko tayari kuambana pamoja na yeye Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika kwenda kujionea hizi adha ambazo Mheshimiwa Mbunge anazieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; mkakati wa Serikali ni pamoja na kuongeza zana za kisasa najua kwenye suala ya uwiano ndiyo ambalo limeleta changamoto. Lakini mwaka wa fedha ujao tumepanga hivyo hivyo maana yake tutaongeza kulingana na mahitaji ya maeneo husika ikiwemo mikopo, tutaleta vilevile vizimba ili kuongeza sasa wigo mpana wa wavuvi katika ziwa hilo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi.

Na. 380

**Ujenzi wa ofisi ya NIDA Wilaya ya Mkoani**

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN. MWINYI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga ofisi ya *NIDA* katika wilaya ya Mkoani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge wa Jimbo la Chambani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mpango wa ujenzi wa ofisi za usajili za wilaya kwa awamu. Katika awamu ya kwanza Serikali imejenga ofisi 13 na awamu ya pili inatarajia kujenga ofisi 31 kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024. Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itaendelea kujenga ofisi za usajili kulingana na upatikanaji wa fedha kwa wilaya nyingine nchini ikiwemo Wilaya ya Mkoani, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdulrahman.

**MHE. MOHAMED ABDULRAHAMAN. MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Ofisi ya *NIDA* ya Wilaya ya Mkoani ni kichumba kidogo sana ambacho akiingia mteja mmoja wengine wanabakia nje wanapigwa na mvua, wanapigwa na jua…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa swali.

**MHE. MOHAMED ABDULRAHAMAN. MWINYI:** Je, Serikali haioni haja ya kuwatafutia jengo jingine kuondoa adha hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa kuna wananchi ambao wamejisajili mwaka 2018, 2019, 2020 mpaka leo hawajapata vitambulisho vya *NIDA* na wanaojisajili sasa hivi wanapata vitambulisho vya *NIDA;* je, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwatafutia jengo lingine kwa kweli tunatambua kwamba zipo wilaya zenye changamoto ndiyo maana tumesema zitaendelea kujengewa ofisi baada ya hizi 31 zitakazofanyika kwenye mwaka wa bajeti ujayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa hali ambayo ameieleza Mheshimiwa Mbunge niombe uongozi wa Wilaya ya Mkoani kule Mwinyi Pemba waone uwezekano wa kuwatafutia, kwa sababu wananchi wanaosajiliwa ni wananchi walewale walio chini ya Mkuu wa Wilaya, chini ya mamlaka zao za serikali za mitaa. Lakini nimuahidi pia tutatembelea huko baada ya bajeti hii ili kuona namna ya kutatua hilo tatizo alilolisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wananchi waliojisajili muda mrefu na hawajapata vitambulisho, tuliahidi hapa Mheshimiwa kwamba mwaka huu tunashukuru Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweza kutupatia 17,000,000,000 ambazo zilikuwa zinadaiwa na mkandarsi na tumeshamlipa, kinachoendelea ni kuanza kutekeleza kadi ghafi ambazo zilisimama uzalishwaji wake kutokana na masuala ya UVIKO. Lakini tunayo matarajio kwamba ndani ya miezi sita ijayo tunaweza kuanza kupokea na wananchi wake watapokea vitambulisho kama ambavyo vitagaiwa kwa wananchi wengine, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Je, Serikali haioni haja ya kupeleka Ofisi za *NIDA* kwenye kila Halmashauri badala ya kwenye kila Wilaya ili kusiogeza huduma za wananchi hususani katika Halmashauri ya Msalala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba inaweza ikaonekana umuhimu wa kuzipeleka ofisi hizi kwenye ngazi ya Halmashauri, lakini shughuli za *NIDA* ziko sehemu ya Serikali Kuu, na kama sehemu ya Serikali Kuu iko chini ya Mkuu wa Wilaya, ndiyo maana tumeanzia pale. Pale ambapo kutakuwa na haja, kwa mfano Wilaya yenye majimbo zaidi ya moja, tutaona uwezekano wa kuimarisha huduma hizo kwenye majimbo ya mbali na makao makuu ya wilaya, ili wananchi hawa waweze kupata hizo huduma stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Afya. Mheshimiwa Asia.

Na. 381

**Hali ya ugonjwa wa figo nchini**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza: -

Je, hadi sasa hali ya ugonjwa wa figo ipoje nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika hapa nchini Tanzania katika jamii ulionyesha kuwa asilimia saba ya Watanzania wanaishi na ugonjwa wa figo, ambao kwa kiasi kikubwa unahusishwa na ugonjwa wa shinikizo la juu la damu, ugonjwa wa sukari na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa wananchi kupima afya mara kwa mara kwani kwa kuchelewa kutambua tatizo la afya madhara yake ni makubwa na gharama ya matitabu inakuwa kubwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nachukua nafasi kwa kuipongeza Serikali kwa kujengwa kwa hospitali za mMikoa;

Je, ni lini Hospitali hizo za Mikoa zitaanza huduma za *dialysis*?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu la pili. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba gharama za matibabu ziko juu;

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kuwasaidia wale wananchi masikini ambao hawana uwezo wa kukidhi gharama hizo za matibabu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa namna ambavyo anashirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Manyara kufutilia shughuli mbalimbali za afya katika mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza linahusu huduma kwenye hospitali zetu za mikoa. Kati ya bilioni 290.9 ambazo Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu amezileta zimetumika kununua vifaa kwa ajili ya *dialysis* kwa hospitali zote za mikoa. Na hata Mkoa wako wa Manyara vifaa tayari vimefika na nategemea mpaka sasa kazi hiyo imeanza na watu wanapata huduma pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili linahusu suala la gharama. Ni kweli ni gharama kubwa sana kwenye eneo la kutibu figo, na nilisema juzi hapa. Tunafikiri kwamba bei yake inaweza ikashuka kuanzia tisini hadi 150,000, hapo inawezekana kushusha. Lakini kuna utaratibu wa *exemption* kwa watu ambao wananshindwa kulipa. Kama yuko kule Manyara kwenye kata yake akiwa na barua ya mtendaji wake wa kata, akifika hospitali anastahili kutibiwa bure.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa matibabu ya ugonjwa wa figo nchini yakemkuwa na gharama kubwa sana na kwa kuwa bima ya afya kwa sasa haitoi huduma ya ugonjwa huu; je, ni utaratibu upi mbadala wa Serikali ili kusaidia kundi la wananchi wa ngazi za chini kwa sababu ugonjwa huu unawakabili rika mbalimbali nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimwambie kaka yangu kwamba bima ya afya inatoa huduma hiyo, ndio maana katika *presentation* tuliyowasomea Wabunge, utaona eneo linalotumia fedha nyingi kwenye eneo la bima ni eneo hilo, lakini liawezekana Mbunge anamaanisha Bima ya Afya ya *CHF* ambayo ndio iko kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile bima ya afya ya *CHF* na tulitaka tuitafute namna ya kuiboresha iweze kuwapa wananchi manufaa

mazuri zaidi. Kama ambavyo nimesema kwenye maswali ya nyongeza, kwamba utaratibu ni ule ule. Niendelee kusisitiza Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuendelee kuwa mabalozi wazuri wa bima ya afya kwa watu wote kwa sababu ndipo tutakapoweza kupata suluhisho la kudumu kwa matatizo haya.

**NAIBU SPIIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafsi niulize swali dogo la nyongeza. Huu ugonjwa wa figo, ugonjwa ambao unatesa sana, kuanzia sasa hivi mpaka watoto wadogo sana; lakini gharama za matibabu ni kubwa sana. Wakati sasa hivi bima haijaanza kwa nini…

**NAIBU SPIIKA:** Uliza swali.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Kwa nini wasiondoe gharama kwa ugonjwa huu tu, Kwa sababu watu wengi wanakufa kwa sababu ya kukosa pesa ya matibabu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mlisikia juzi kwenye bajeti yetu kwamba Rais wetu ametoa bilioni tano kwa ajili ya kuwasaidia watu wasiojiweza kwenye eneo hili la matatizo ya figo na mengine. Lakini bado tuna utaratibu mzuri sana kama nchi wa kuweza kuwapa *exemption* wale ambao hawajiwezi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nafikiri kikubwa ambacho naendelea kukuomba Mheshimiwa Mbunge uwe balozi mzuri wa bima ya afya kwa wote kwa sababu ni suluhisho la kudumu kwenye matatizo haya. Tuna magonjwa mengine hapa ni asilimia 15, hii ni asilimia saba, wanateseka sana watanzania. Kwa hiyo mimi ninachosema tuwe mabaloozi wazuiri wa bima ya afya kwa wote tutapata suluhisho la kudumu kwenye tatizo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mitambo yenu mmenunua kwenye makampuni ambayo gharama zao ziko juu sana. Tafuteni

makampuni ambayo yanauza vifaa hivi ambavyo gharama zake za chini ili wananchi wapate huduma bora na waweze kuokoa maisha yao. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumelipokea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Shangazi.

Na. 382

**Wamachinga waliofuzu kuwa wafanyabiashara rasmi**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Je, Wamachinga wangapi wamefuzu kuwa Wafanyabiashara rasmi kwa kipindi cha kuanzia 2016 hadi 2021?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA,** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2023 kuna jumla ya Machinga 1,987,361 nchini. Aidha, kwa sasa Serikali inaanda utaratibu wa kuwatambua Wamachinga waliofuzu kuwa wafanyabiashara mara baada ya kurasimisha biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha urasimishaji wa biashara nchini kupitia njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya faida za urasimishaji biashara kupitia mafunzo mbalimbali ya biashara ya ujasiriamali. Mikakati iliyopo

kwa sasa ni uanzishwaji wa vituo jumuishi vya urasimishaji wa biashara na uandaaji wa mwongozo wa taratibu za kurasimisha biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Serikali inakiri kwamba bado haijapata kutambua vizuri kundi hili na ilihali na yenyewe inatambua kwamba ilitoa vitambulisho;

Je, Serikali iko tayari kukiri kwamba vitambulisho vile havikusaidia kutambua kundi hili, haswa kwa teknolojia duni ambayo imetumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ili machinga atoke kwenye hali ya umachinga na Kwenda katika kundi la wafanyabiashara wagodo na wa kati, ni lazima apewe afua mbalimbali za kikodi;

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuzibainisha hizo afua za kikodi ili hawa wamachinga waweze kuzitambua na waweze kuingia kwenye kundi la wafanyabiashara rasmi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni kweli moja ya changamoto zilizojitokeza kwa vitambulisho vile vya awali vya kuwatambua wamachinga ilikuwa ni kwamba vinaweza vikatumika na mtu yoyote kwa sababu havikuwa vya kielektroniki. Moja ya kazi kubwa tunayofanya sasa katika bajeti inayokuja ni Serikali Kwenda kutoa vitambuilisho vya kielektroniki ambavyo

vitasaidia kuwatambua wajasiriamali walipo, lakini pia pale ambapo watakuwa wamekua, kwa maana kutoka mitaji ile midogo ya 4,000,000 ambayo tunatambua kama wajasiriamali, kwenda juu tutawatambua kama wafanyabiashara halali na kuwarasimisha kwenye kundi halali la wafanyabiashara kutoka wajasiriamlali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye swali la pili; Serikali inafanya kazi kubwa sana. Moja ni kurasimisha kuwatambua wajasiriamali hawa na Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan ametoa fedha 10,000,000 kuanzisha ofisi za wamachinga kila Mkoa. Sasa kupitia hizo tutawatambua na kuwasaidia kupata mikopo nafuu kwenye taasisi zetu za fedha, lakini pia utaratibu unaokuja ni kuona zile fedha asilimia 10 ambazo zilikuwa zinatolewa ziweze kuwa na manufaa kupitia benki ili wajasiriamali hawa wadogo ambao wanahitaji mitaji kwa ajili ya kuendeleza biashara zao wanufaike.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 383

**Ulinzi wa maeneo yenye vyanzo vya maji**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza: -

Je, maeneo mangapi yameshabainishwa kuwa ni vyanzo vya maji salama ardhini na hatua gani zinachukuliwa kulinda maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde nchini na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ina jukumu la kutambua, kutunza, kuhifadhi na kuendeleza vyanzo vya maji vya juu ya ardhi na chini ya ardhi pamoja na kutambua uwezo wa chanzo na ubora wa maji yake. Hadi sasa vyanzo vya maji chini ya ardhi vilivyotambuliwa ni 152 na kati yake, vyanzo 30 vimewekewa mipaka na vyanzo 10 vimetangazwa kwenye gazeti la Serikali na hivyo kulindwa kisheria. Vilevile, Wizara inaendelea kufanya utafiti katika maeneo mengine 172 yenye maji chini ya ardhi ili kubaini uwezo wa chanzo na ubora wa maji yake.

Aidha, Serikali kupitia maabara za maji nchini hufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa ubora wa maji chini ya ardhi kupitia visima vya uchunguzi vilivyochimbwa kwenye maeneo mbalimbali nchini. Sampuli za maji huchukuliwa kutoka visima hivyo na kufanyiwa uchunguzi na pale inapothibitika kuwepo kwa mabadiliko ya mwenendo wa ubora hatua stahiki huchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Serikali kulinda maeneo yaliyotambuliwa kuwa vyanzo vya maji chini ya ardhi ikiwemo kuyawekea mipaka na kuyatangaza kwenye gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu, pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utunzani na uhifadhi wa maeneo husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu spika, swali la kwanza. Kwa kuwa maji chini ya ardhi ni Pamoja na chemchem zinazofumuka wakati wa masika na kupotea wakati wa kiangazi hasa mkoani Kilimanjaro;

Je, Serikali inazitambua na kuziwekea udhibiti chemchem hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa utafiti wa Chuo Kikuu cha *SUA* kimebaini kuwa maji chini ya ardhi yanapungua sana lakini Serikali haijaweza kudhibiti maji ya mvua ya kila msimu na kila mwaka yanayotiririka na kutuharibia barabara. Serikali ina mpango gani sasa wa kufanya *project* ambayo itaweza kudhibiti hali hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, chemchem zote za Mkoa wa Kilimanjaro ni chemchem ambazo zina manufaa makubwa katika kuongeza maji katika miradi yetu inayoenda kwa wananchi. Hivyo tunailinda na kuidhibiti na tunaitambua vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kuhusu maji chini ya ardhi hupungua na sasa maji yanapotea. Hapa tumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hasssan, tuna mitambo mitano ya kuchimba mabwawa na lengo la kuchimba mabwawa haya ni kuhakikisha maji yote ya mvua tuweze kuyatunza kwa ajili ya mhitaji wakati wa kiangazi. Tunataka kuonesha kwamba mvua ambazo Mwenyezi Mungu anatupatia siyo laana bali ni baraka na yanakwenda kutumika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kumekuwa kuna utaratibu wa uuzwaji wa maji kupitia ma – *bowser* ya magari kwa gharama kubwa kwa wananchi na ilihali ya Serikali imeweka mtandao mzuri sasa hivi wa maji Kibamba;

Je, Serikali mko tayari kutoa kauli ya usitishaji wa uuzaji wa maji kupitia magari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, usitishaji wa kuuza maji kwenye magari, huu sio utaratibu rasmi. Tutalifanyia kazi pamoja na Wizara husika.

**NAIBU SPIKA:** Weheshimiwa Tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Paresso.

Na. 384

**Uhitaji wa kuvuna fisi Kata ya Endamarariek – Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuvuna fisi wanaovamia makazi ya Wananchi, kujeruhi na kuua Watu katika Kata ya Endamarariek?

**NAIBU SPIKA:** Popo, leo fisi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto ya fisi kuvamia maeneo ya makazi ya wananchi hususan kwenye Kata ya Endamarariek Wilayani Karatu, Wizara kupitia Jeshi la Uhifadhi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu imekuwa ikifanya msako wa fisi katika maeneo husika ambapo tangu mwaka 2019 hadi sasa jumla ya fisi saba wamevunwa. Aidha, mapango/makazi ya fisi 11 yameharibiwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fisi wanaishi katika makundi, Wizara inaendelea kufanya soroveya ili kuyabaini makundi ya fisi yaliyosalia na kuyavunja ikiwa ni pamoja na kuharibu makazi yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza niseme siridhiki na majibu ya Serikali kwa sababu hizo jitihada zimefanywa na wananchi na takribani watu 24 ndani ya miaka mitatu wakiwemo Watoto wameuawa na fisi. Sasa swali langu;

a) Je, ni lini na kwa uhakika hilo jeshi la uhifadhi litafika katika eneo hilo na kuwavuna fisi hao ili wananchi waendelee kukaa kwa amani?

b) Je, ni lini, Serikali itakuja na mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi ili yanapotokea majanga kama hiyo waweze kujihami na kukabiliana na Wanyama wa namna hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye swali lake la nyongeza linalohusiana na lini Jeshi la Uhifadhi litaenda kuwasaka, naomba tu niendelee kuelekeza kuanzia sasa kwamba Jeshi la Uhifadhi Kanda ya Kaskazini waelekee Karatu, wakaamnze kufanya msako wa fisi hao ili wananchi waweze kuona umuhimu wa uhifadhi lakini pia fisi hao waweze kurudishwa hifadhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala hili la elimu. Kwa sasa hivi tumeanza programu za kufundisha au kuelimisha wananchi namna ya kujikinga na wanyama wakali na uharibifu. Kwa hiyo naendelea kuelekeza kwenye upande wa Kanda ya Kaskazini kwamba, pamoja na msako huo utakaofanyika pia watoe elimu kwa wananchi ili tuweze kuwa na mashirikiano ya pamoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mbali na fisi kusumbua wananchi na kuleta madhara kwa watu wenye hifadhi pia kumekuwa na tatizo kubwa la mamba katika Ukanda wa Ziwa Victoria hasa maeneo ya Tairo na Guta Pamoja na Wilaya ya Bunda upande wa Mwibala;

Je, nini tamko la Serikali katika kuhakikisha mnaenda kuvuna mamba hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwenye upande wa mamba tumeshaanza programu ya kutengeneza vizimba na kuwafundisha wananchi namna ya kujikinga nao. Kwa sababu tatizo linajitokeza ni pale ambapo wananchi walizoea kuogelea ziwani, wengine wana mazoea ya kwenda kucheza kandokando ya ziwa. Nakumbuka enzi za zamani hasa wale tulioishi Kanda ya Ziwa, tulikuwa tuna maeneo yetu ambayo huruhusiwi kwenda kucheza maeneo hayo kwa sababu kuna Wanyama wakali hususan mamba na viboko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kadri tunavyozidi kuongezeka wananchi wanaendelea kuyasogelea yale maeneo. Kwa hiyo tunaendelea kuwaelimisha wananchi kama yale mazoea ya wananchi ya kila siku ya Kwenda kuogelea kama ilivyo zamani tuyaache, na matokeo yake tunatengeneza vizimba kama wanaenda kuchota maji basi waende kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kadri tunavyozidi kuongezeka wananchi wanaendelea kuyasogelea yale maeneo. Kwa hiyo, tunaendelea kuwaelimisha wananchi kwamba, yale mazoea ya kila siku ya kwenda kuogelea kama ilivyokuwa zamani tuyaache na matokeo yake tunatengeneza vizimba, kama wanaenda kuchota maji, basi waende kwenye maeneo yale tu ambayo yameainishwa, ili kuepuka hii athari inayojitokeza ya hasa watoto

wanachukuliwa na mamba na inakuwa ni athari kwa wazazi pia na kwa jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, tunawaelimisha wananchi pia waendelee kuyaheshimu haya maeneo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa ameshakuelewa.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Mwikwabe Mwita.

Na. 385

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* – Nyamongo, Wilayani Tarime**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Nyamongo Wilayani Tarime?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita, Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila mkoa na wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo. Tayari Serikali imeshakamilisha kuandaa michoro na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Tarime eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi ni katika Kijiji cha Nyabichune, Kitongoji cha Komoware, Kata ya Matongo.

Aidha, pamoja na kiasi cha shilingi milioni 45 kilichotolewa awali kwa ajili ya shughuli za maandalizi, tayari Serikali imetuma kiasi cha shilingi milioni 228 kwa kila Chuo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya watu wa Tarime naomba niishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha ya kujenga *VETA* kule Tarime Vijijini, hasa Nyamongo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; napenda kujua kimetengwa kiasi gani cha fedha angalau chuo kianze kufanya kazi kwa hatua ya mwanzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nini kauli ya Serikali kwa wananchi pale ambao wengi ni wachimbaji wadogo wadogo, wavuvi karibu na Ziwa Victoria, lakini pia na wakulima wa mazao mbalimbali na Tarime pia mazao yanastawi. Nini matarajio ya wananchi hasa vijana kwa uwepo wa Chuo cha *VETA* katika eneo langu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kujenga vyuo hivi katika kila wilaya kama nilivyoeleza awali. Katika awamu ya kwanza hii ya mwaka 2022/2023 Serikali imetenga bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo. Tafsiri yake ni nini, katika kila chuo katika awamu ya kwanza tunapeleka bilioni moja na milioni 400 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo tisa ya awamu ya kwanza. Majengo haya tisa ya awamu ya kwanza yatakapokuwa

yamekamilika, vyuo hivi bila shaka vitaanza kufanya kazi ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wetu ni nini? Katika awamu ya pili vilevile tutatenga tena fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo mengine tisa. Jumla kuu ya bajeti yote ili chuo kiweze kukamilika ni jumla ya bilioni tatu na milioni mia tano. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan imeweza kutenga katika mwaka huu, lakini vilevile katika mwaka ujao tunakwenda kukamilisha ujenzi huu ambapo vyuo hivi vyote vitakapokamilika ni zaidi ya bilioni 200 tunatarajia kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa pili, upande wa mafunzo yatakayotolewa, tunafanya mapitio sasa hivi ya mitaala ile ya utoaji wa mafunzo ya ufundi wa *VETA* na hasa hasa tutazingatia zile shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika maeneo husika. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi kwenye maeneo ya kilimo kutakuwa na mitaala ya kilimo, kwenye maeneo ya madini kutakuwa na mitaala ya shughuli za madini, kwenye maeneo ya uvuvi, tutakwenda hivyo angalau ku-*customize* kulingana na shughuli za kiuchumi za eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. RASHID V. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naomba niishukuru Serikali niliomba ituletee vifaa vya kufundishia, walituletea katika Chuo chetu cha *VETA,* Wilaya, lakini pia niliomba gari na wakatuletea kwa ajili ya utawala, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, kwa kuwa wananchi wamejitokeza kwa wingi, kwa maana kuna wanafunzi wengi katika chuo kile. Je, Serikali inaweza sasa kutuongezea wakufunzi wa masomo mbalimbali wanaosoma pale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Kawawa na Waheshimiwa Wabunge wote, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tayari alishatoa kibali cha kuajiri watumishi wakiwemo wakufunzi pamoja na walimu. Tumepata kibali cha watumishi 571 na mpaka hivi sasa tunavyozungumza watumishi 151 tayari wameshaajiriwa, tutawapeleka Namtumbo na maeneo mengine ya vile vyuo vya zamani, lakini tuna vyuo 25 vipya na vile vinne vya mikoa watakwenda watumishi hawa na tunaendelea kuajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sima, jiandae Mheshimiwa Mchafu.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Hili kombe linafanya mwonekane sasa humu ndani.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kujenga vyuo vingi vya *VETA* na ili kuweza kueta hamasa kwa wanafunzi na wazazi kujiunga kwenye vyuo hivi, Serikali ina mpango gani ama mkakati gani wa kutoa mikopo kwa wanafunzi hawa wanaojiunga na Vyuo vya *VETA* ama vyuo vya kati? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, tunatoa mikopo katika elimu ya juu na elimu hii ya kati. Tumetengeneza mkakati huo, lakini kwa mkakati wa muda mfupi tumezungumza na wadau ikiwemo benki na taasisi nyingine za kifedha. Wenzetu wa *NMB* tayari katika mwaka huu wametoa zaidi ya bilioni 200 kwa ajili ya mikopo katika kada ya hii ya kati ikiwemo na wanafunzi wa vyuo vya *VETA* na sisi kama Serikali tunatengeneza mkakati. Baada ya mapitio ya mitaala tutajua kitu gani cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchafu.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha *VETA,* Wilayani Mkuranga, ikizingatia Wilaya ya Mkuranga ni ukanda wa viwanda? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Hawa Mchafu, Mbunge wa kutoka Mkoa wa Pwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa mchafu na Wabunge wengine wote wa Mkoa wa Pwani. Katika zile wilaya 64 nilizozizungumza awali ipo Wilaya ya Mkuranga, ipo Wilaya ya Kibiti, ipo Wilaya ya Bagamoyo, ipo Wilaya ya Kisarawe. Kazi imeshaanza na shughuli zinaendelea kule Mkuranga na maeneo hayo mengine niliyoyataja kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi, kazi tayari imeshaanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni wanne wa Mheshimiwa Naibu

Spika, wanafunzi kutoka Chuo cha *DIT* Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Miriam Mkanza, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Nape Nnauye, Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ndugu Mohammed Abdulla, Katibu Mkuu; Ndugu Selestine Kakele, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Othman Khatib, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya *TCRA;* Ndugu Stephen Kagaigai, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Utangazaji *TBC,* karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna Ndugu Zuhura Muro, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la *TTCL;* Brigedia Jenerali Yohana Mabongo, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Posta Tanzania; Profesa John Nkoma, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; Ndugu Hawa Ngumbi, Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Ushauri la *TCCRA, CCC;* Ndugu Hab Mkwizu, Mwenyekiti wa Bodi ya Makampuni ya Magazeti ya Serikali; Dkt. Jabiri Bakari, Mkurugenzi Mtendaji wa *TCRA;* Mhandisi Peter Ulanga, Mkurugenzi *TTCL;* Dkt. Dapthrosa Kimbory, Mwakilishi Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Utangazaji *TBC;* Ndugu Nkundwe Mwasaga, Mkurugenzi *ICTC;* Ndugu Macrice Mbodo, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Posta *TPC;* na Ndugu Justina Mashiba, Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo vilevile Ndugu Mary Shao, Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano; Ndugu Tuma Abdallah, Mkurugenzi Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania; na Ndugu Nasibu Abdul, Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya *Wasafi Media, (Diamond Platinum),* karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile wao Ndugu Francis Ciza (Majizzo), Mkurugenzi Mtendaji wa *EFM* na *TV E;* Ndugu Bakari Machumu, Mkurugenzi wa *Mwananchi Communications;* Ndugu Deodatus Balile, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania na Rais wa Wahariri wa Tanzania, Afrika Mashariki; Ndugu Sebastian Maganga, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa *Clouds;* Ndugu Maxence Mello, Mkurugenzi Mtendaji *Jamii Forum;* Ndugu Philip Besiimire, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya *Vodacom Tanzania;* Ndugu Dinesh Dalsingh, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya *Airtel*

*Tanzania;* Ndugu Silivia Balwire, Mwakilishi wa Kampuni ya *tiGO Tanzania;* Ndugu Nagib Fereji, Mwakilishi Kampuni ya *Halotel Tanzania;* Ndugu Tao Mian, Mwakilishi wa Kampuni ya *Huawei*. *(Makofi)*

Wageni hawa wameambatana na Menejimenti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Nape ni mama yake mzazi, Ndugu Kezia Mhana. Karibu sana mama. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni kumi wa Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo, wachungaji na wanafunzi kutoka Nzuguni B, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Taasisi ya Sanaa Utamaduni *Holy Smile* kutoka Msalala, Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, Viongozi wa *Kolping Society Tanzania* kutoka Bukoba, Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Waandishi wa Habari kutoka Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Jessica Kishoa, chawa wa mama kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni 40 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 36 wa Mheshimiwa Joseph Kamonga, wanafunzi wa vyuo mbalimbali vya Jijini Dodoma wanatokea Ludewa, Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Ngwasi Kamani, viongozi wa *Tanzania Youth in Protecting Society* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Simon Songe, watumishi wa *TARURA* kutoka Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo:-

Wanafunzi 30 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Jamhuri ya Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Nape anakwenda na wakati, anakwenda na dunia inavyobadilika kidigitali. Pamoja na taarifa yake na *speech* ya bajeti kuwemo kwenye vishkwambi vyenu, lakini vilevile kuna *QR* hii na maana ya *QR* mnajua? *Quick Response,* ukii-*scan*, taarifa nzima inapatikana. Inaonesha namna Tanzania inavyobadilika kidigitali.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Nape ahsante sana na hongera sana kwa namna unavyoitendea haki Wizara yako wewe na wataalam wako. *(Makofi)*

Wageni wengine, watangazaji wa kipindi cha "Dadas", Kituo cha *East African TV*. Karibuni. *(Makofi)*

Watangazaji wa kipindi cha *"Cloud 360" Clouds Media*. *(Makofi)*

Wadau wengine wa Wizara, wote msimame kwa pamoja ambao hawakutambuliwa. Karibuni. *(Makofi)*

Haya tunasubiri sasa wale mabingwa wetu wa Afrika Kusini wakija tuwatambue vilevile. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge, kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili. Nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka miwili sasa ambacho kimekuwa na maendeleo na uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue nafasi hii kumshukuru sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa maelekezo yake, miongozo yake na ushauri wake, ambavyo kwa kweli imesaidia sana katika kutimiza majukumu yetu Wizarani. Naomba pia, kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kwa usimamizi wake kwetu. Miongozo yake, ushauri wake na maelekezo yake kwetu ambayo yamekuwa chachu ya ufanyaji kazi wetu. tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua matarajio waliyonayo wananchi ya kufikishiwa huduma za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe pamoja na Spika kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuliongoza Bunge letu na uongozi mzima wa Bunge letu, kwa kuongoza Bunge letu kwa weledi, busara, hekima, tunawapongeza sana. Napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupa katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu yetu Wizarani, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso - Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela - Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki na Wajumbe

wote wa Kamati kwa namna ambavyo wanatusimamia na kutuelekeza na kutuongoza vizuri, Wizara inanufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hii katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika hotuba hii, ninawaahidi mimi na wenzangu Wizarani hatutawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwako na kwa Bunge kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Hayati Mussa Hassan Mussa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani - Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Nitoe pole pia kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na wananchi wa Jimbo la Amani kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inasimamia Taasisi Tisa ambazo ni ambazo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania, Shirika la Posta Tanzania, Shirika la Utangazaji Tanzania, Kampuni ya Magazeti ya Serikali, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Tume ya TEHAMA, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano na sasa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Hotuba hii itaeleza kwa ufupi masuala yaliyotekelezwa na Wizara pamoja na taasisi tunazosimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara iliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 282.06. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 26.3 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 255.8 ziliidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, Wizara imepokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 125.1. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 12.8 sawa na asilimia 48.7 ya fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 112.3 sawa na asilimia 43.9 ya fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia Tarehe 30 Aprili, 2023 Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 24.9 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, tozo, kuongeza salio, mauzo ya picha za Viongozi Wakuu wa nchi, machapisho na ada ya mwaka ya magazeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea na upangaji wa masafa kwa huduma za mawasiliano, ambapo mnada wa wa masafa ulifanyika Tarehe 11 Oktoba, 2022 kwenye bendi za 700 MHz, 2300 MHz, 2600 MHz na 3500 MHz ambayo yanatumika kwa ajili ya mawasiliano ya simu na intaneti katika kuwezesha huduma za *4G* na *5G* hapa nchini. Makampuni manne ya ndani yalifanikiwa kushinda zabuni kwa mauzo ya Dola za Marekani milioni 187.5, hadi mwezi Aprili, 2023, asilimia 75 ya fedha hizo, kiasi cha Dola za Marekani 140.6 zimeshalipwa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya habari, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imefanya masuala yafuatayo: -

(i) Kwanza tumefanya mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ambapo Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza mwezi Februari mwaka huu.

(ii) Imeratibu mikutano 13 ya Msemaji Mkuu wa Serikali, jumla ya vipindi 25 vya televisheni vinavyohusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo viliandaliwa na kurushwa hewani. Tumefanikiwa kujenga studio ya muda Jijini Dodoma kwa ajili ya kuzalisha vipindi vya Kitaifa na Kimataifa.

(iii) *TBC* imeboresha maudhui yanayorushwa kwenye redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Aidha, *TBC* ilifanikiwa kununua haki za kutangaza michuano ya Kombe la Dunia la *FIFA* ambapo jumla ya michezo 28 ilirushwa *TBC1* na michezo yote 64 ilirushwa *TBC* Taifa na *TBC online*. Uanzishwaji wa kurusha taarifa ya habari kwa Kiingereza umeanza mwezi Novemba, mwaka jana, na hivyo kupanua wigo wa habari zinazotolewa na Shirika letu la Utangazaji.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 210 mwaka jana hadi kufikia vituo 215 Mwezi Aprili, 2023 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo 56 mwaka jana na kufikia vituo 65 mwezi Aprili, 2023.

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi katika sekta ya habari, Wizara kupitia *TCRA* na Idara ya Habari Maelezo, imetoa jumla ya leseni mpya 20 za magazeti na leseni 18 za maudhui ya mtandao.

(vi) Serikali imeendelea kuboresha huduma za utangazaji hususan wa redio jamii *(community radio)* katika maeneo ya vijijini.

(vii) Serikali kupitia *UCSAF* imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya kurushia matangazo na studio za Redio ya Taifa katika maeneo ya kimkakati na hasa mipakani.

(viii) Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Magazeti ya *Daily News,* Habari leo na Habari Mtandao, Kampuni ya Magazeti ya Serikali imeendelea kutekeleza mpango wake mahususi *(Editorial Transformational Plan)* kwa kuandika habari za kina za uchambuzi.

(ix) Mradi wa kufunga mtambo mpya wa kisasa wa uchapaji wa magazeti unaendelea na uko katika hatua za kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa sekta ya mawasiliano. Kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa, Sekta ya Habari na Mawasiliano imekua kwa kasi ya asilimia 9.1. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 55 mwaka jana mwezi Aprili hadi kufikia laini milioni 62 mwezi Aprili mwaka huu, sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka milioni 29.9 Aprili, mwaka jana hadi kufikia milioni 33.1 Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Takwimu hizi zinaashiria hali ya ukuaji wa sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara imeendelea kutekeleza mambo mengine yafuatayo:-

(i) Wizara inaendelea kufanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003;

(ii) Utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa binafsi na kanuni zake, ukiwemo mchakato wa uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

(iii) Maboresho ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi ambayo yamezingatia maslahi mapana ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya mawasiliano, tumefanikiwa kuandaa mkakati wa sekta ya mawasiliano wa kuimarisha ushiriki wa nchi Kikanda na Kimataifa ambapo Tanzania imefanikiwa kupata nafasi mbalimbali katika Jumuiya ya Kimataifa kwenye nyanja ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanikiwa kutekeleza mfumo wa anuani za makazi nchini kupitia mradi wa anwani za makazi na postikodi. Aidha, mfumo wa anwani za makazi umeweza kuunganisha taasisi za umma kama ile Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kuboresha taarifa za wamiliki wa viwanja pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa kuboresha taarifa za walipakodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti ambapo jumla ya laini za simu 997 zilizokuwa zikitumika kwenye mawasiliano ya ulaghai wa mawasiliano ya simu za kimataifa zilisitishwa matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesimamia zoezi la usajili na uhakiki wa laini za simu nchini ambapo hadi Tarehe 30 Aprili mwaka huu, laini za simu zinazotumika kwenye mitandao ya simu zilizofikia milioni 63.3 zimesajiliwa kwa alama za vidole.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* imetoa jumla ya leseni 26 kwa watoa huduma za posta na usafirishaji, ujenzi wa jengo la Umoja wa Posta Afrika linalojengwa kwa ubia wa *TCRA* ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 98. Nchi yetu imebahatika kuwa Makao Makuu ya Umoja wa Posta Afrika na Makao Makuu yake yako Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* limekabidhiwa rasmi jukumu kutekeleza mradi wa mkongo wa Taifa na kituo cha Taifa cha kutunzia *data* na Shirika la Mawasiliano Tanzania limeendelea kufanya maboresho na usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa kodi kwa njia ya kielekroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya kupeleka huduma za mawasiliano vijijini imesainiwa ambapo jumla ya minara 758 kwa ajili ya kupeleka huduma za mawasiliano itajengwa na jumla ya minara 304 itaongezewa nguvu, hafla hii ilifanyika hapa Dodoma na Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru kwa kuhudhuria hafla

hiyo. Pia jumla ya minara 42 katika shehia 38 imekamilika na kuzinduliwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufikishwaji wa huduma za mawasiliano vijijini ikiwemo maeneo ya kimkakati kama Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Julius Nyerere na Msomera kule Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa TEHAMA. Tumesimamia na kuratibu utungaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022. Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa kanuni za utekelezaji wa sheria hii. Pia tumewezesha kujenga uwezo wa wataalam 500 wa Jeshi la Polisi kwenye nyanja ya usalama wa mtandao na kusimamia maendeleo ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, pia tumekamilisha taratibu za kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa Kituo ha Kuhifadhi *Data* Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekamilisha upembuzi yakinifu wa kubaini maeneo yenye changamoto ambayo minara 758 itakwenda kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo Wizara imeendelea kuyafanyia kazi ni pamoja na:-

(i) Ukamilishaji wa Mpango Mkakati wa Uchumi wa Kidigidali *(Digital Economy Framework)* wa 2023 – 2033;

(ii) Kuhuisha ununuzi wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali *(Extension of Government Internet Bandwidth)* wenye kasi ya *5G;*

(iii) Kufanikiwa kuandaa daftari la huduma za Serikali kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA ambapo shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

Moja, kukamilika kwa usanifu wa kituo cha kampuni changa za TEHAMA cha Kanda ya Dar es Saalam na kutengeneza mfumo jumuishi utakaowezesha kuwa na taarifa za wabunfifu, kampuni za TEHAMA, wawekezaji katika huduma za bidhaa na ubunifu katika TEHAMA, vituo atamizi vya TEHAMA na vituo vya kuendeleza ubunifu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara umeainishwa katika ukurasa wa 34 hadi 59 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara inakadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 150.7 ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za mkongo wa Taifa wa mawasiliano, tozo itokanayo na kuongeza salio la simu, usajili wa magazeti na ada ya mwaka ya magazeti, vitambulisho vya Waandishi wa Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Upande wa sekta ya Habari.

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya Habari tunakusudia kufanya mapitio ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 ili kuendana na mabadiliko katika sekta ya habari. Hapa tunakusudia tuwe na sheria moja inayosimamia sekta ya habari kwa ujumla wake badala ya sasa utangazaji na *print media* kuwa na sheria tofauti.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, kuratibu utungwaji wa Sheria ya Shirika la Utangazaji la Tanzania *(TBC)*. Tunataka *TBC* iwe na sheria inayojitegemea;

(iii) Kujenga studio maalum kwa ajili ya vipindi vya moja kwa moja vya redio na televisheni;

(iv) Kuanzisha redio ya Afrika itakayotangaza kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuendeleza matumizi ya Kiswahili na kujenga Umoja wa Afrika. Tunaanzisha redio itakayokata Afrika nzima tulilete Bara letu pamoja, tupandishe hadhi ya Kiswahili chetu.

(v) Kuendelea kusimamia sekta ya habari kwa kuisimamia iendelee kukua;

(vi) Kuhamasisha vyombo vya habari vya nje katika kutangaza Tanzania, kui-*brand* nchi yetu;

(vii) Kuendelea kujenga na kufunga miundombinu ya utangazaji katika Wilaya Tisa kati ya 21 ambazo hazina usikivu au zina usikivu hafifu;

(viii) Kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya *TBC* Jijini Dodoma;

(ix) Ununuzi wa mitambo na vifaa vya utangazaji vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii kwa lengo la kuunganisha studio tano za mikocheni, Zanzibar, Barabara ya Nyerere, Dodoma na Arusha.

(x) Kununua gari moja la kurushia matangazo ya televisheni mbashara;

(xi) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya kiwanda cha uchapaji na kufunga mitambo ya kisasa ya uchapaji wa magazeti ya Serikali;

(xii) Kuanza taratibu za ujenzi wa kituo cha habari ambacho kitajumuisha chaneli ya televisheni ya Serikali, studio ya kuzalisha maudhui, vyumba vya mikutano, mifumo ya kufuatilia habari zinazotokea duniani na kutoa fursa kwa Waandishi wa Habari kufanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mawasiliano. Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997 na kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003;

(ii) Kuratibu uimarishaji na upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na posta kote nchini;

(iii) Kuanzisha utaratibu mahsusi wa kugawa masafa kwa ajili ya redio za utangazaji kidigitali *(digital frequencies),* mwaka huu tunaanzisha kwa sababu pamekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa *frequencies;*

(iv) Kuratibu utungwaji wa sheria ya kuimarisha matumizi na kuhakikisha uendelevu wa mfumo wa anwani za makazi hapa nchini;

(v) Kuratibu uanzishwaji wa anga la juu nchini ikiwemo kufanya maandalizi ya kurusha *satellite* yetu kama nchi na kuwezesha urahisi na unafuu katika upatikanaji wa huduma za mawasiliano hapa nchini. Hapa ninamshukuru sana Rais Samia, jana ametangaza hadharani sasa mwaka huu wa fedha Tanzania tutakuwa na *satellite* yetu Mwenyezi Mungu akitujalia. *(Makofi)*

(vi) Kuandaa mpango wa uwekezaji katika sekta ya mawasiliano;

(vii) Kusimamia utekelezaji wa biashara mtandao *(e-Commerce);*

(viii) Kuratibu uanzishwaji wa maghala maalum ya kuhifadhia bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao;

(ix) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Brodibandi wenye kasi zaidi *(National Broadband Strategy);*

(x) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa miundombinu ya mawasiliano ya simu, redio na televisheni vijijini; na

(xi) Ukamilishwaji wa shughuli za ujenzi wa Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa TEHAMA. Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA nchini, Wizara inategemea kufanya majukumu yafuatayo: -

(i) Kuhuisha Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 na kuandaa mkakati wa utekelezaji;

(ii) Kuandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Teknolojia zinazoibukia *(emerging technologies)* kama vile *Artificial Intelligence, robotics, internet of things* ili kuiwezesha nchi kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda *(Fourth Industrial Revolution);*

(iii) Kuratibu na kuwezesha matumizi ya mfumo wa mikutano ya video *(video conferencing)* katika ngazi za Wizara, Mikoa 26, Halmashauri 185 nchini;

(iv) Kufanya tathmini ya uanzishwaji wa *smart cities* katika Mikoa ya Dodoma, Arusha na Mbeya; *(Makofi)*

(v) Kuendelea na utaratibu wa uendelezaji wa mifumo ya Kitaifa nchini;

(vi) Kuandaa mkakati wa kuboresha matumizi ya tafiti za TEHAMA;

(vii) Kuendelea kuboresha usimamizi na uanzishwaji wa kampuni changa za TEHAMA kwa kuboresha mazingira ya kisera, kisheria na kikanuni na usimamizi;

(viii) Kuanzisha vituo vitano vya kanda vya kusaidia kukuza taaluma na ubunifu wa TEHAMA;

(ix) Kuunganisha taasisi za Serikali kwenye mtandao mmoja *(GoVNET);*

(x) Kuwezesha usimikaji wa vituo vya HudumaPamoja nchini;

(xi) Kujenga maabara tatu kwa ajili ya kufufua vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza;

(xii) Kujenga uwezo wa wataalamu wa TEHAMA 500 Serikalini katika maeneo yenye taaluma haba ikiwemo *artificial intelligence, big data analytics, machine learning augmented reality;* na

(xiii) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi *Data* Zanzibar na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha *Data* Dodoma pamoja na kusimamia uanzishwaji wa vyuo viwili vya TEHAMA, kimoja Nala na kingine Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuwezesha nchi kuelekea katika uchumi wa kidigitali, hususan kuhimiza mfumo wa kufanya biashara bila fedha taslimu *(cashless economy)* ambao unawezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Mpango mzima wa mwaka huu wa fedha tunaoombea fedha hapa tunataka tuipeleke nchi yetu kwenye *cashless economy.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha haya kwenye sekta zote za uchumi na kijamii, Wizara imepanga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye sekta ili kuendana na mageuzi

haya, ikiwemo kuharakisha ujenzi, uendelezaji na usimikaji wa miundombinu ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara itafanya mapinduzi kwenye taasisi za kisekta kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na sekta binafsi, kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA, ikiwemo uanzishwaji na uendelezaji wa kampuni changa *(start-ups),* kuwezesha sekta nyingine kuelekea kwenye mapinduzi haya ya kidigitali na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu itahakikisha uchumi wa kidigitali unawekewa mazingira bora ya kiudhibiti, lakini mtandao uwe salama kiuwekezaji ikiwemo kuandaa sera, miongozo, taratibu, lakini kikubwa kulinda maadili ya Kitanzania na kuhakikisha usalama mtandaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo kuhusiana na usalama mtandaoni:-

(i) Kufanya tathmini ya Mkakati wa Kitaifa wa Usalama Mtandaoni wa 2018 - 2023 ambao tunaumalizia, na kuandaa na kutekeleza mkakati mpya wa Usalama Mtandao wa 2023 - 2028;

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Elimu kwa Umma kuhusu Usalama Mtandaoni;

(iii) Kusimamia ukamilishwaji wa utekelezaji wa usimamizi wa Miundombinu Muhimu ya TEHAMA *(Critical ICT Infrastructures - CII);*

(iv) Kuimarisha muundo wa kiutawala na kiusimamizi wa ulinzi dhidi ya uhalifu wa mtandao; na

(v) Kuimarisha uwezo wa wakaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa mifumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga uwezo wa Wizara kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kazi zifuatazo zitafanyika:-

(i) Kuendeleza watalaam wa sekta na wa nje ya sekta kwa kutoa mafunzo ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya TEHAMA na elimu ya matumizi ya teknolojia mpya zinazoibukia kwenye sekta nyinginezo;

(ii) Kuwajengea uwezo waandishi wa Habari na Wahariri wa Vyombo vya Habari;

(iii) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi; na

(iv) Kuelimisha umma juu ya teknolojia mpya za kidijitali, kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi salama na yenye tija ya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zitakazotekelezwa na taasisi tisa zinazosimamiwa na Wizara, zimeainishwa kwenye ukurasa wa 74 na 82 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati, napenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee nawashukuru Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew, Mbunge na Naibu Waziri wangu; Mohammed Khamis Abdulla, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Ndugu Selestine Gervas Kakele, Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri za mchana na usiku kuhakikisha mambo yanakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naishukuru Menejimenti ya Wizara, Wenyeviti wa Bodi na ninashukuru leo nimewaona wote hapo, na Wakurugenzi wa Taasisi zinazosimamiwa na Wizara, Viongozi wa Taasisi, Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wadau wote wa sekta ya Habari, Waandishi wa Habari wa nchi hii, ahsanteni kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa mlionionesha katika kipindi cha utumishi wangu katika Wizara hii. Nawashukuru sana. Vile vile nawashukuru watoa huduma za makampuni ya mawasiliano kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuhakikisha tunawafikia Watanzania hasa vijijini, na hasa juzi tuliposaini mkataba wa kuwafikia Watanzania milioni nane kuwaunganisha na huduma za mawasiliano. Watoa huduma ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru wadau wote wa TEHAMA kwenye mitandao ya kijamii kote; *Instagram, Tweeter* na kwingine kote kwa kazi nzuri mnayofanya. Niwahakikishie yale mnayoyazungumza mtandaoni, tunayasikia, tunayasoma na tunayafanyia kazi. Niwahakikishieni, tuna ngozi ngumu ya kutosha, hayatukeri. Endeleeni kutusaidia tuiongoze Wizara yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue fursa hii kuwashukuru washirika wa maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Sekta ya Habari, Mawasiliano na teknolojia ya Habari. Baadhi ya washirika hao ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano, Shirika la Umoja wa Posta Duniani, Shirika la Umoja wa Posta Afrika, Benki ya Dunia kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzishukuru Jumuiya za Kikanda na Kimataifa za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, na Jumuiya ya Ulaya kwa ushirikiano katika masuala ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu Sekta hii. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia uchumi wa kati wa juu ifikapo Mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naomba kuwashukuru kwa dhati sana wananchi wangu wa Jimbo la Mtama, kuendelea kuniamini na wakati mwingine kunivumilia wakati natimiza majukumu yangu. Nawapenda, nawathamini sana, tuendelee kuchapa kazi kwa pamoja. Tukishirikiana inawezekana kubadilisha hali ya Jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kusahau upendo, uvumilivu na kunitia moyo kwa familia yangu wakiongozwa na binti yangu Jayla, wanangu; Jayda na Jayson na mama yao, mke wangu mpenzi Rhobi. Nawashukuru kwa upendo wao, kunivumilia hasa ninapokosekana kwa muda na namna wanavyonitia moyo katika kutimiza kazi zangu. Leo nimefurahi kwa mara ya kwanza mama yangu mzazi amekuja hapa. Ahsante sana mama, nakushukuru kwa malezi yako, nakushukuru kwa upendo wako kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 212,457,625,000.00 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha shilingi 30,503,685,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida, ambapo shilingi 18,522,155,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 11,981,530,000.00 ni za Matumizi Mengineyo. Kiasi cha shilingi 181,953,940,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi 146,777,440,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 35,176,500,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *http://www.mawasiliano.go.tz.* na pia kama ulivyotangaza, waki-*scan* kwenye hiyo *QR Code* ambayo imesambazwa unaweza kuipata hotuba yote kwenye simu yako, kwenye *smartphone* yako yoyote, tuanze wenyewe kwenda kidigitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

## A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa kumi na moja wa Bunge la kumi na mbili.

3. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka miwili ambacho kimekuwa na maendeleo na uwekezaji mkubwa kwa Sekta zote hususan kwa Sekta ya Habari, Mawasiliano na TEHAMA. Wizara inatambua matarajio makubwa waliyonayo wananchi ya kufikishiwa huduma za Habari na Mawasiliano kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025. Matarajio haya ndiyo yaliyomsukuma Mheshimiwa Rais kuanzisha Wizara hii mpya tarehe 12 Septemba, 2021 ili kuharakisha ufikishaji huduma kwa wananchi.

4. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa weledi, busara na hekima kubwa. Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.); Naibu Spika katika kukusaidia kuliongoza Bunge lako. Vilevile, Nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa kukusaidia kuliongoza Bunge lako Tukufu. Ninapenda kuwapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuaminiwa na kuchaguliwa katika kipindi kingine kusimamia Sekta zilizoko chini ya Kamati hizo.

5. Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao kwangu. Ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 68, kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika Hotuba hii. Maadam 'imani huzaa imani', nawaahidi mimi na wenzangu Wizarani, hatutawaangusha. Ninapenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu pamoja na wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa na ya mwananchi katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

6. Mheshimiwa Spika, Naomba kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Mtama kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kujiletea maendeleo kwenye Jimbo letu; bila kuisahau familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania.

7. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwako Mheshimiwa Spika na Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

8. Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndio inayosimamia Mapinduzi ya Kidijitali nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Katika uchumi wa kidigitali, Sekta zote hufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano na mwingiliano zikiwezeshwa na mazingira bora ya kidijitali. Mapinduzi haya yanawezeshwa na misingi muhimu ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Mifumo ya Mawasiliano ya simu, usambazaji

barua, vifurushi na vipeto kwa njia ya posta, uwepo wa vyombo vya upashanaji Habari pamoja na uimara wa uhuru husika. Aidha, Uchumi wa Kidijitali unawekewa mazingira bora ya kiudhibiti, kiuwekezaji na atamizi kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezaji wa kampuni changa (startups).

9. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kutunga na kusimamia Sera zinazohusiana na masuala ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari, Mawasiliano ya Posta na Simu; kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA; kuendeleza wataalam wa TEHAMA, na kuendeleza na kusimamia miundombinu ya Mawasiliano nchini. Utekelezaji wa majukumu haya kutaiwezesha Tanzania kuimarika kushiriki uchumi wa kidijitali katika kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4th Industrial Revolution) yanayowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA na pia kuwa na jamii inayopata taarifa sahihi kwa wakati ili wananchi waweze kushiriki maendeleo yao.

10. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inasimamia Taasisi tisa ambazo zimegawanyika kwenye umahsusi wa Huduma, mashirika ya kibiashara, udhibiti, mfuko na taasisi wezeshi. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL); Shirika la Posta Tanzania (TPC); Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC); Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN); Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); Tume ya TEHAMA (ICTC); Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC). Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala yanayotekelezwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Taasisi inazosimamia.

11. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu kuu la udhibiti wa huduma za Mawasiliano kama ilivyoainishwa kwa Sheria ya Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania Sura Na. 172 (Tanzania Communications Regulatory Act CAP. 172) ambapo pamoja na mambo mengine, Mamlaka imekabidhiwa majukumu ya:-

i) Kutoa leseni za watoa huduma za mawasiliano nchini;

ii) Kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayakufuatwa;

iii) Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa kama gharama za maunganisho kati ya mtandao mmoja na mwingine;

iv) Kulinda watumiaji wa huduma za mawasiliano;

v) Kusimamia rasilimali adimu za mawasiliano ikiwemo masafa, namba na majina ya vikoa;

a) Viwango vya uwekezaji;

b) Upatikanaji, ubora na viwango vya huduma;

c) Gharama za huduma; na d) Ufanisi wa uzalishaji na usambazaji wa huduma.

vi) Kufuatilia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na watoa huduma.

vii) Kukuza ushindani katika sekta;

viii) Kusambaza taarifa zinazohusu kazi na majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na

ix) Kushauriana na mamlaka nyingine za udhibiti katika kutekeleza majukumu sawa na yale ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

12. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania lilianzishwa kwa Sheria Sura Na. 303 na lilianza kazi rasmi tarehe 1 Januari, 1994 baada ya kuvunjwa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania. Baada ya kuvunjwa, iliundwa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania kwa mgawanyo wa mali wa asilimia 70 kwa 30 mtawalia. Shirika la Posta linamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Shirika lina majukumu makuu manne kama ifuatavyo:-

i) Kutoa huduma za Posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii) Kutosheleza mahitaji ya kitaifa ya huduma za Posta katika sekta za viwanda, biashara na jamii kwa ujumla kwa ufanisi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iii) Kutoa huduma za kutuma na kulipa fedha kwa njia ya hawala za Posta (Money Order na Postal Order), au kwa kutumia njia nyingine zinazoonekana zinafaa; na

iv) Kutoa huduma za Kaunta kwa ajili ya Shirika na Huduma za Serikali bila kuathiri majukumu mengine yaliyotajwa katika Sheria ya uanzishwaji wa Shirika.

13. Mheshimiwa Spika, Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation) ni Shirika la Umma lenye jukumu la kutoa huduma za mawasiliano kwa jamii na kusimamia uendeshaji wa Miundombinu ya Kimkakati kwa usalama wa nchi. Shirika lilianzishwa kupitia Sheria Na. 12 ya Bunge ya mwaka 2017 (Tanzania Telecommunications

Corporation Act, No. 12 of 2017). Kwa mujibu wa sheria hiyo, Shirika la Mawasiliano Tanzania lina majukumu ya msingi yafuatayo: -

i) Kuimarisha ulinzi na usalama wa huduma za mawasiliano ya simu nchini na utoaji wa huduma ya mawasiliano ya simu kibiashara na kiuchumi;

ii) Kutoa huduma za mawasiliano ya simu kwa mujibu wa Sheria;

iii) Kujenga na kuendesha miundombinu ya mawasiliano ya kimkakati kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana;

iv) Kutoa huduma ya miamala ya kifedha inayohusiana na mawasiliano ya simu;

v) Kuendesha mifumo na huduma ya mawasiliano ya simu ikiwemo mfumo wa TEHAMA ndani na nje ya nchi;

vi) Kutoa huduma za mawasiliano kwa njia ya sauti na picha;

vii) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu TEHAMA kwenye mashirika, Taasisi za umma na kwa wajasiriamali; na

viii) Kukuza uwekezaji wa huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya nchi.

14. Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni taasisi ya huduma kwa umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257 (2002). Kabla ya kuanzishwa TBC kupitia Tangazo la Serikali Na.186 la Mwaka 2007, taasisi hii ilijulikana kama Taasisi ya Utangazaji Tanzania (TUT) ambayo ilitokana na muungano wa iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na Televisheni ya Taifa (TVT). Shirika linatekeleza majukumu yake kupitia vyombo vyake vya habari vikiwemo:

a. Redio *(TBCTaifa, TBCFM, na TBCIntentational);*

b. Televisheni *(TBC1, TBC2, na TBC3 (au Tanzania Safari Chaneli);*

c. TBC Mtandao (Tovuti ya www.tbc.go.tz, Programu Tumizi ya TBC Live, *Facebook, Instagram na Twitter.* Shirika pia lina Tovuti na Programu Tumizi ya Tanzania Safari Channel *(www.tanzaniasafarichannel.go.tz);*

d. Studio za redio za Kanda (Magharibi – Kigoma; Kaskazini – Arusha; Makao Makuu – Dodoma; na Ziwa Nyasa - Songea).

15. Mheshimiwa Spika, Majukumu makuu ya TBC ni kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kutafakarisha kwa kuzingatia kaulimbiu ya 'Ukweli na Uhakika'.

Chombo cha Utangazaji cha Umma (Public Service Boradcaster - PSB) kina sifa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuwafikia wananchi wote nchini bila kujali umbali, idadi ya wakazi au gharama;

(ii) Kuandaa maudhui yanayohusu na kugusa maisha ya makundi yote ya jamii na kwa kuzingatia utamaduni;

(iii) Kuendesha huduma ya utangazaji kwa fedha zinazotokana na bajeti au vyanzo vingine;

(iv) Kulinda, kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Taifa;

(v) Kulinda, kutetea na kusimamia rasilimali za Taifa kama vile maliasili, madini, gesi, mafuta, mazingira na urithi wa kihistoria;

(vi) Kukuza na kudumisha uzalendo, kutetea na kusimamia maslahi ya Taifa; na

(vii) Kulinda, kutetea na kujenga taswira chanya ya Taifa.

16. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilianzishwa kwa Tamko la Rais la mwaka 1970 na imetokana na utaifishaji wa iliyokuwa Tanganyika Standard Newspapers Limited. Kampuni hii inasimamiwa na kuendeshwa chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Msajili wa Hazina inamiliki asilimia 99 ya hisa na Mhariri Mtendaji anamiliki asilimia 1 ya hisa kwa minajili ya kukidhi matakwa ya Sheria. Kampuni hii huchapisha magazeti mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Magazeti yanayochapwa kwa lugha ya Kiingereza ni Daily News na Sunday News na yale ya Kiswahili ni HabariLeo pamoja na gazeti la Michezo la Spotileo ambalo huchapishwa mara mbili kwa wiki. Pamoja na magazeti hayo, Kampuni pia hutoa vijarida mbalimbali vinavyolenga makundi maalum, kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. TSN pia inatumia njia ya mtandao kusambaza habari mbalimbali ndani na nje ya nchi kupitia tovuti pamoja na mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, Instagram na Youtube. Aidha, Kampuni inamiliki kiwanda cha uchapaji ambacho hutumika kwa ajili ya kuchapa magazeti yake na pia kufanya uchapaji wa kibiashara kwa kutumia mtambo mdogo wa kidijitali.

Kampuni lina majukumu makuu manne kama ifuatavyo: -

i) Kuwa chombo cha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi;

ii) Kuunga mkono sera na mipango ya Serikali na kuhabarisha na kuelimisha umma juu ya sera na mipango hiyo;

iii) Kutafuta na kuandika habari sahihi zenye michango mbalimbali katika sayansi, jamii, siasa, uchumi na utamaduni; na

iv) Kuwa kiini cha kutoa habari kwa lengo la kukuza uchumi na kueneza amani na mshikamano kwa Watanzania.

17. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ulianzishwa kwa Sheria Namba 11 ya Mwaka 2006, Sura ya 422, kwa lengo la kupeleka na kufikisha huduma ya mawasiliano kwa wananchi waishio katika maeneo ya mijini na maeneo ya vijijini yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano. Mwaka 2009 kanuni za Mfuko zilipitishwa na Mfuko na kuanza kazi tarehe 1 Julai, 2009.
Malengo ya Mfuko yaliyoainishwa na sheria ya uanzishwaji wake yamejikita katika maeneo yafuatayo:

i) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

ii) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na Serikali katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

iii) Kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;

iv) Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani;

v) Kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inapatikana vijijini na sehemu za mijini zenye mawasiliano hafifu kwa bei nafuu; na

vi) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

18. Mheshimiwa Spika, Tume ya TEHAMA ilianzishwa kwa Amri ya Rais kupitia Tangazo Namba 532 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 20 Novemba, 2015. Uanzishwaji wa Tume ya TEHAMA nchini ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2003 na maelekezo ya Baraza la Mawaziri yaliyotolewa mwezi Juni, 2012 kuhusu kuunda Tume ya Kitaifa ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini.

Kwa mujibu wa Amri iliyoanzisha Tume ya TEHAMA, majukumu yake ni pamoja na:-

i) Kukuza uwekezaji katika TEHAMA;

ii) Kujenga uwezo na kukuza utaalamu na viwango katika fani

iii) Kushauri na kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya tafiti na kuweka viwango na mwelekeo;

iv) Kuhifadhi na kuendeleza miundombinu na programu za TEHAMA; na

v) Kufanya kazi nyingine zozote zinazoainishwa na Sheria.

19. Mheshimiwa Spika, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, imeanzishwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Namba 11 ya Mwaka 2022. Tume ina majukumu yafuatayo:

(i) Kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa wakusanyaji na wachakataji;

(ii) Kusajili wakusanyaji na wachakataji kwa mujibu wa sheria;

(iii) Kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;

(iv) Kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;

(v) Kutoa elimu kwa umma kwa kadri itakavyofaa kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;

(vi) Kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa;

(vii) Kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za nchi nyingine zinazosimamia ulinzi wa taarifa binafsi na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hii; na

(viii) Kutekeleza majukumu mengine ya Tume kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

20. Mheshimiwa Spika, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limeanzishwa kwa Sheria ya Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania Sura Na. 172 (Tanzania Communications Regulatory Act CAP. 172) Kifungu cha 37. Kulingana na Sheria iliyoanzisha Baraza, Kifungu cha 38 kinalipa Baraza majukumu yafuatayo:

i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zinazosimamiwa kisheria kwa kushauriana na TCRA na Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano na watoa huduma.

ii) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni kuhusu masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano;

iii) Kuanzisha kamati za watumiaji katika ngazi za mikoa, wilaya na sekta na kushauriana na kamati hizo; na

iv) Kufanya mashauriano na wahusika katika sekta, Serikali na makundi mengine ya watumiaji wa huduma kuhusiana na masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma zinazosimamiwa kisheria.

## B. HALI YA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NCHINI



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa pamoja na Viongozi wengine wakati akishuhudia utiaji saini Mikataba ya kupeleka Huduma za Mawasiliano Vijijini kati ya Serikali na Makampuni ya Simu (TTCL, Vodacom, Airtel, Halotel, Tigo) iliyofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma*

### Hali ya Ukuaji wa Sekta ya Habari na Mawasiliano

21. **Mheshimiwa Spika**, kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2021, Sekta ya Habari na Mawasiliano imekua kwa asilimia 9.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2020. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano na kusambaa kwa huduma zitolewazo na vyombo vya habari. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Wizara Mwaka 2021 asilimia 69 ya ardhi ya Tanzania *(Geographical Coverage)* inafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani. Sekta hii huchangia katika uchumi moja kwa moja na kupitia sekta zingine zote kama nyenzo ya uwezeshaji katika kuongeza ufanisi wa utendaji kupitia Teknolojia ya Habari.

### Hali ya Upatikanaji wa Mawasiliano Nchini

22. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua, takwimu zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 55.7 Mwezi Aprili, 2022 hadi kufikia laini milioni 62.3

Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 11.8 Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka milioni 29.9 Mwezi Aprili, 2022 hadi kufikia milioni 33.1 Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka milioni 35.7 mwezi Aprili, 2022 hadi kufikia Milioni 44.3 mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 24.1. Aidha, Watoa huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano wamefikia 23 ukilinganisha na watoa huduma 22 Mwezi Aprili, 2022 (hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.5).

Watoa huduma wa huduma za ziada (Application Services and Value Added Services) wamefikia 141 ukilinganisha na watoa huduma 102 Mwezi Aprili, 2022 (ongezeko la asilimia 38).

### Hatua iliyofikiwa ya Mapinduzi ya Uchumi wa Kidijitali

23. **Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa uendeshaji wa Uchumi wa ulimwengu umeshabadilika kuelekea katika Uchumi wa Kidijitali unaoshehenezwa na kuendeshwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Tanzania hatujaachwa nyuma katika kuelekea katika mapinduzi haya. Pamoja na kuimarisha na kutanua miundombinu ya TEHAMA, Serikali inaendelea kuhanikiza matumizi ya miundombinu hii kwa tija ikiwemo kuimarisha usalama wake kwa mifumo ya kielektroniki ikiwemo Mfumo wa Anwani za Makazi. Pamoja na kuwezesha huduma nyingine Mfumo huu utawezesha Biashara mtandao. Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuiongezea uwezo minara (upgrade) inayotumia teknolojia ya 2G pekee ili iweze kutoa pia huduma ya intaneti kwa kiwango cha 3G na 4G na kuwawezesha wananchi kupata huduma za kidijitali. Kufikia mwezi Aprili, 2023 minara 227 imeongezwa uwezo huo.

Aidha, Serikali inaendelea na mradi wa kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo ya wazi yanayotumiwa na wananchi katika shughuli zao za kila siku ili kuongeza na kuhamasisha matumizi ya mtandao wa intaneti nchini. Serikali pia inakamilisha kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya Biashara Mtandao utakaosaidia kupata taarifa za watumiaji wa biashara mtandao Nchini na uratibu wa Biashara husika. Sambamba na hilo, kupitia Shirika la Posta Tanzania, Serikali imeingia mkataba na ASYAD Group ya Oman kwa ajili ya kujenga Kituo cha Kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao. Mradi huo utaimarisha mnyororo wa usafirishaji na Biashara Mtandao kimataifa.




24. Mheshimiwa Spika, Hatua nyinginezo zilizochukuliwa ni pamoja na kuandaa mpango wa miaka 10 wa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali (National Digital Economy Framework 2023-2033) utakaosaidia kuongeza matumizi ya kidijitali kwa huduma zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta binafsi. Aidha, kazi ya kuunganisha mifumo ya utoaji huduma ili iweze kuzungumza na pia kuwezesha huduma nyingi za Serikali kupatikana kwenye dirisha moja kwa kutumia mifumo ya kielektroniki. Vilevile, upembuzi yakinifu kuhusu kuanzishwa kwa Taasisi ya TEHAMA na vituo vya kanda nne vya Ubunifu wa TEHAMA (zonal soft centres) umekamilika. Lengo la Taasisi hii ni kukuza ubunifu wa TEHAMA nchini ili kuleta mapinduzi ya kidijitali. Kupitia vituo hivi vya kikanda, Serikali inaendelea kuboresha mazingira mazuri ya kuwezesha wabunifu mbalimbali ikiwemo mtu mmoja mmoja kutumia miundombinu hii kuboresha mawazo yao ya kibunifu.

25. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanza utaratibu wa kuanzisha Taasisi ya Anga za Juu, pamoja na mambo mengine Taifa linalenga kuwa na mfumo mahsusi wa uratibu wa masuala ya anga, kujenga uchumi wa anga *(space economy)* na hatimaye nchi yetu kurusha Seteliti yake angani. Hatua hii itarahisisha matumizi ya teknolojia ya anga inayochochea mapinduzi ya kiuchumi na kijamii.

## Hali ya Sekta ya Habari Nchini

26. Mheshimiwa Spika, Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 210 mwaka 2022 hadi kufikia vituo 215 Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 2.3 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo 56 mwaka 2022 na kufikia vituo 65 Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 16. Cable Television zimepungua kutoka 59 Mwezi Aprili, 2022 na kufikia 57 Mwezi Aprili, 2023 sawa na kupungua kwa asilimia 3.3 na magazeti yameongezeka kutoka 284 na kufikia 321 Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 13. Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za Utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana. Kufikia Mwezi Aprili,

2023 usajili wa televisheni mtandao zimepungua kutoka 663 hadi 413 sawa na kupungua kwa asilimia 34.7, hii ni kutokana na marekebisho ya kanuni za Huduma za Maudhui Mtandaoni ya mwaka 2022.

## Hali ya Kusikika kwa Redio na Televisheni za Umma

27. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF imeendelea kuboresha huduma za utangazaji hususani kwa redio jamii zilizopo katika maeneo ya vijijini kwa kujenga minara ambayo itatumika kwa pamoja na watoa huduma za utangazaji. Kwa kuanzia Serikali imeanza utekelezaji wa mradi huu katika mikoa saba. Lengo haswa la mradi huu ni kuzisaidia redio jamii zilizopo katika Halmashauri zetu kuweza kuongeza usikivu ili Watanzania waliopo katika maeneo hayo waweze kupata taarifa zinazowahusu kwa usahihi na kwa wakati. Aidha, Serikali kupitia UCSAF imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya kurushia matangazo na studio za redio ya Taifa katika maeneo ya kimkakati na mipakani. Maeneo ambayo miradi imekamilika ni pamoja na Mlimba mkoani Morogoro, Ngorongoro Mkoani Arusha, Ludewa mkoani Njombe, Ruangwa mkoani Lindi, Ngara mkoani Kagera, Mlele Mkoani Katavi pamoja na Kisaki mkoani Morogoro. Aidha, ujenzi unaendelea katika vituo vya Kyela Mkoani Mbeya, Makete Mkoani Njombe, Mbinga Mkoani Ruvuma, Uvinza Mkoani Kigoma, Lushoto Mkoani Tanga pamoja na Kyerwa mkoani Kagera.

Vilevile, taratibu za Ununuzi wa vifaa vya kurushia Matangazo mbashara ya Redio nje ya studio (Quantum - 9), Matangazo mbashara ya televisheni na mitandao ya kijamii nje ya studio zinaendelea ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kwa wakati.



Watoa huduma wamefikia **141** ukilinganisha na watoa huduma 102 Mwezi Aprili, 2022 (ongezeko la asilimia 38).



Kufikia mwezi Aprili, 2023 minara **227** imeongezwa uwezo huo

Ongezeko la vituo vya Radio

**210** mwaka 2022 hadi kufikia vituo **215** ngezeko la asilimia 2.3



Ongezeko la vituo vya Runinga **56** mwaka 2022 hadi kufikia vituo **65** ngezeko la asilimia 2.3

Magazeti yameongezeka kutoka **284** kufikia **321** Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 13

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23




### Hali ya Ukusanyaji wa Mapato

28. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 150.7** ambapo **Shilingi bilioni 99.5** ni fedha kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano; **Shilingi bilioni 50.7** kutokana na tozo ya kuongeza salio kwenye laini za simu; **Shilingi milioni 24** Vitambulisho vya Waandishi wa Habari; **Shilingi milioni 300** kutokana na mauzo ya picha za viongozi; **Shilingi milioni 30** kwa ajili ya Usajili wa magazeti; **Shilingi milioni 100** Ada ya Mwaka ya Magazeti; **Shilingi 1,000** Marejesho ya fedha za Umma; **Shilingi 1,000** Ukumbi wa Mikutano; na **Shilingi 1,000** Mapato kutoka vyanzo vinginevyo.

29. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Wizara imekusanya **Shilingi bilioni 13.4** kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambayo ni sawa na **asilimia 13.5** ya makadirio ya makusanyo, makusanyo haya yataongezeka baada ya kukamilika kwa mradi unaoendelea wa upanuzi wa Mkongo. Kiasi cha **Shilingi bilioni 11.4** kutokana na tozo ya kuongeza salio kwenye laini za simu sawa na **asilimia 22.5** ya lengo. Aidha, Idara ya Habari-MAELEZO imekusanya **Shilingi milioni 87.5** kutokana na mauzo ya picha za

Viongozi Wakuu wa nchi na picha ya Baba wa Taifa, vitambulisho, machapisho na ada ya mwaka ya magazeti sawa na asilimia 19.3 ya lengo.

### Hali ya Utekelezaji wa Bajeti

30. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Shilingi 282,056,786,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 26,279,346,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi 17,249,317,000 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 9,030,029,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Shilingi 255,777,440,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo Shilingi 215,777,440,000 ni fedha za ndani na Shilingi 40,000,000,000 ni fedha za nje.

### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

31. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Wizara imepokea na kutumia jumla ya Shilingi 12,785,953,117 sawa na asilimia 48.65 ya fedha zilizotengwa. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa Shilingi 8,328,338,858 ni za Mishahara na Shilingi 5,228,526,070.72 ni Matumizi Mengineyo.

### Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

32. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Wizara (Fungu 68) imepokea jumla ya Shilingi 112,318,781,171.98 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo ni asilimia 43.9 ya fedha zilizotengwa.




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe, Dkt. Hussein Ali Mwinyi akizindua mnara wa mawasiliano wa kampuni ya Tigo ikiwa ni sehemu ya uzinduzi wa minara arobaini na mbili (42) ya mawasiliano ya simu iliyojengwa Zanzibar kupitia ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).*

## Eneo la Habari - MAELEZO

33. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuratibu Mikutano 13 ya Msemaji Mkuu wa Serikali na kuainisha mafanikio ya utekelezaji wa Serikali pamoja na kutoa ufafanuzi wa masuala mabalimbali. Aidha, vipindi 25 vya Televisheni vinavyohusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo viliandaliwa na kurushwa TBC1, vipindi hivi vilihusu Kilimo na Umwagiliaji, Viwanda, Ujenzi, Madini na Upanuzi wa Bandari Tanga;

(ii) Kufanikiwa kujenga studio ya muda Jijini Dodoma kwa ajili ya uzalishaji wa vipindi vya kitaifa vya kimkakati ambavyo vitarushwa hewani kupitia vyombo vyote vya habari na mitandao ya kijamii;

(iii) Kufanikiwa kutoa leseni mpya 20 za magazeti hivyo kufanya Jumla ya magazetii yaliyosajiliwa kufikia 321;

(iv) Kutoa ufafanuzi wa mafanikio ya Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake na kutoa ufafanuzi wa hoja zilizoibuliwa na wananchi dhidi ya Serikali. Vyombo vya habari 10 yakiwemo magazeti, Redio, Televisheni na Mitandao ya Kijamii vilitumika kuhabarisha umma;

(v) Kufanikiwa kuratibu Kongamano la Kwanza la Maendeleo ya Sekta ya Habari

ambalo lilikutanisha wadau wa habari takriban 1,000 ambao walijadili njia za kuendeleza tasnia ya Habari, changamoto za vyombo vya habari na namna bora ya kuzitatua;

(vi) Kuhamasisha wananchi kushiriki Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ambapo Wizara kupitia njia za vipeperushi vya kielektroniki na vipindi vya sauti vya Mtandao kupitia chaneli ya Maelezo (Maelezo podcast); pamoja na kuwaratibu Mawaziri kuongea katika vipindi vya Televisheni na Redio kuhamasisha wananchi kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022;

(vii) Kuandaa na kuratibu Mikutano saba (7) ya Mawaziri na Mmoja wa Mkuu wa Taasisi kupitia jukwaa la Msemaji Mkuu wa Serikali (Clubhouse) ambayo imewakutanisha Viongozi hao wa Serikali na Wananchi waliopo ndani na nje ya Nchi na Serikali kupata fursa ya kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali katika Sekta zao na kupata michango na maoni toka kwa wananchi ya kuboresha katika baadhi ya masuala wanayoyasimamia;

viii) Kuandaa Makala 253 za JUVYO kupitia chaneli ya Youtube ya Maelezo TV;

(ix) Kuratibu uandaaji wa Mkakati wa Mawasiliano katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya vyombo vya ulinzi na usalama kuwa na mikakati ya mawasiliano;

(x) Kuratibu Kikao Kazi cha 18 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali kilichowakutanisha Maafisa Habari zaidi ya 500 kutoka Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar;

(xi) Kufanya mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ambapo muswada wa marekebisho ya Sheria hiyo umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza mwezi Februari, 2023;

(xii) Kukamilisha rasimu ya Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano ya Serikali kwa umma;

(xiii) Kuratibu Vyombo vya Habari katika matukio ya Kitaifa na ziara za Viongozi nchini; na

(xiv) Kutoa msaada wa kitaalamu kwa Wizara na Taasisi za Serikali.

### Eneo la Mawasiliano

34. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:



(i) Imefanya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 na Rasimu ya Sera ya Posta imewasilishwa kwa wadau kwa ajili kupata maoni. Kanuni za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote zimerejewa na Marekebisho ya Kanuni za Mfumo wa kusimamia na kuratibu Mawasiliano yapo katika hatua za ukamilishaji;

(ii) Kufanya maboresho ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 ambayo imeweka mazingira ya kuvutia uwekezaji na kuzingatia maslahi mapana ya wananchi;

(iii) Kufanikiwa kuratibu ushiriki wa Sekta katika shughuli za kikanda na kimataifa ikiwemo mikutano ya JPC, ATU, ITU, UPU, CTO, UPU, PAPU na kukuza mashirikiano na nchi za USA, China, Vietnam, DRC, Oman, Afrika Kusini na Malawi. Aidha, Tanzania imefanikiwa kupata kiti katika Baraza la Umoja wa Mawasiliano Afrika na Umoja wa Mawasiliano Duniani.

(iv) Kufanikiwa kuandaa Mkakati wa Sekta ya Mawasiliano wa kuimarisha ushiriki kikanda na kimataifa.

(v) Kufanikiwa kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi nchini ambapo hadi Mwezi Aprili, 2023 jumla ya Anwani za Makazi 12,669,718 zimetolewa nchini. Ni dhahiri kuwa hatua hii sasa itawezesha wananchi kupatiwa huduma majumbani lakini pia kuharakisha biashara mtandao. Hadi sasa Wizara inaendelea na zoezi la uhakiki wa taarifa zilizokusanywa kwenye Operesheni Anwani za Makazi;



(vi) Kuboresha Mfumo wa kidijitali wa NaPA kwa kuwezesha Mfumo kutambua zilipo huduma za Kijamii na Kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuwezesha kufikiwa kirahisi kupitia moduli ya uelekeo ya Mfumo wa NaPA, Aidha, Wizara imeweza Kuratibu majadiliano na wadau kwa ajili kufungamanisha Mfumo na mifumo mingine ya Serikali, kama vile TRA kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia Mfumo wa NaPA; na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kuimarisha makusanyo ya kodi ya ardhi; na

(vii) Kuratibu na kufanikisha jitihada za ufikishaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya vijijini ikiwa ni pamoja na maeneo ya kimkakati ikiwemo kufikisha huduma za Mawasiliano ya simu katika Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Julius Nyerere na ufikishwaji wa mawasiliano ya simu, posta na redio katika eneo la Msomera – Handeni.

## Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

35. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kukamilisha kutungwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Data Protection Act, 2022) iliyosainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Novemba, 2022 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali tarehe 02 Disemba, 2022. Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa Kanuni za kuwezesha utekelezaji wa Sheria hii na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imeanza kufanya kazi rasmi;



(ii) Kuwajengea uwezo wataalamu 500 wa Jeshi la Polisi kwenye nyanja ya usalama mtandao na kutoa vitendea kazi kuhakikisha mazingira ya kudhibiti usalama wa mtandao kwa pamoja;

(iii) Kufanya Makongamano manne ya Kisekta ndani na nje ya nchi;

(vi) Kufanikiwa kuboresha mfumo wa *'case management'* kwa ajili ya kurekodi matukio ya uhalifu wa mtandao katika Jeshi la Polisi kwa kufanya ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA Desktops - 184, Kompyuta mpakato - 210, Scanners - 50 na TTCL modems 200;



(iv) Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Program);

(v) Kufanikiwa kuandaa Kongamano la Kimataifa kati ya Tanzania na nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mwezi Oktoba, 2022 ambapo jumla ya washiriki 300 kutoka Tanzania na DRC walihudhuria, na pia Kongamano la 'Connect to Connect' ambapo wahiriki 365 kutoka nchi 28 walishiriki;

(vii) Kufanikiwa kutafsiri Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Mitandao kwa lugha ya Kiswahili; na

(viii) Kushiriki kwenye ujenzi wa Mkongo wa Baharini unaounganisha Tanzania na mabara ya Ulaya na Asia kutoka Kampuni ya 2Africa kupitia Kampuni ya Airtel. Kukamilika kwa mradi huu kutaifanya Tanzania kuwa na mikongo mitatu inayounganisha Tanzania kimataifa.

## Masuala Mengine

36. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kuratibu maandalizi ya Kuhuisha Sera zinazosimamiwa na Wizara ikiwemo Sera ya Posta ya mwaka 2003 na Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003; kuwezesha utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, 2022; kuendelea kusimamia maandalizi ya utungaji wa Sheria ya TEHAMA, kuhuisha Sheria ya Huduma ya Habari na Sheria ya TBC;

(ii) Kutungwa kwa Kanuni za Usajili wa Laini za simu, kanuni za The Electronic and Postal Communication (Radio and Televisions Broadcasting Content (Amendment) Regulation, 2022 na kurekebisha Kanuni nyingine sita za usimamizi wa Sekta ya Habari na mawasiliano. Wizara inaendelea kuboresha Kanuni za Usajili wa laini za Simu, Tozo za Muda wa Maongezi wa simu, Kanuni za Masafa na Kanuni za Kushirikiana katika Miundombinu ya Mawasiliano;

(iii) Mpango kazi wa elimu kwa umma kuhusu usalama mtandao umeandaliwa. Vipindi maalumu 12 vya televisheni na redio vya kuelimisha umma kuhusu usalama mtandao vimeandaliwa;

(iv) Mpango wa Usimamizi wa Vihatarishi wa Wizara na rejesta ya vihatarishi vimeandaliwa na usimamizi wake unaendelea;

(v) Mpango wa ukaguzi wa ndani uliandaliwa na unaendelea kutekelezwa ambapo maeneo yenye changamoto yameendelea kuainishwa na kufanyiwa maboresho stahiki;

(vi) Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na mifumo ya kimenejimenti kwa kufanya ukaguzi wa ndani kila robo mwaka na taarifa kuwasilishwa mamlaka husika;

(vii) Muundo mpya wa Wizara umeandaliwa baada ya kuanzishwa kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kukamilisha kujaza nafasi kulingana na Muundo mpya wa Wizara;

(viii) Kukamilisha kujaza Bodi za Wakurugenzi za Taasisi nane;

(ix) Usimamizi wa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara – Mtumba, lenye ghorofa saba ambapo hivi sasa limefikia asilimia 62;

(x) Wizara iliwapatia mafunzo ya kujengewa uwezo Watumishi wote kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi. Aidha, viongozi wa Wizara na Taasisi walipatiwa mafunzo maalum (retreat) ya kujengewa uwezo Jijini Arusha;

(xi) Wizara imewashirikisha watumishi katika vikao vya maamuzi kama vile Baraza la Wafanyakazi. Aidha, imewezesha Watumishi kushiriki michezo ya Mashindano ya Wizara/Taasisi (SHIMIWI), Mei mosi na Mabonanza ya kila mwezi ambayo huwashirikisha viongozi wa Wizara; na

(xii) Kufanikiwa kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi salama ya Mtandao kwa vijana na watumishi wa umma katika maeneo ya Arusha, Dar es Salaam na Zanzibar na pia kupitia vipindi maalumu vya Televisheni na redio.



# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

## C. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

37. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Miradi inayotekelezwa na Wizara ni Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uliotengewa **Shilingi bilioni 149.7,** kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 149** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 7** ni fedha za nje. Mfumo wa Anwani za Makazi wenye jumla ya **Shilingi bilioni 40**, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali uliotengewa **Shilingi bilioni 39.3** ambazo ni fedha za nje. Mradi wa Elimu kwa Umma uliotengewa jumla ya **Shilingi milioni 940** ikiwa ni fedha za ndani, Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA **Shilingi bilioni 3.3** ambazo ni fedha za ndani; Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) **Shilingi bilioni 13.1** ambazo fedha za ndani; na Mradi wa Kufunga Mtambo mpya wa Kisasa wa Uchapaji Shilingi **bilioni 9.4** ambazo ni fedha za ndani.

### Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

38. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umekusudiwa kuongeza wigo wa mawasiliano ya simu na intaneti nchini na nchi jirani katika kuharakisha mapinduzi ya kidijitali. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa mkongo wa mawasiliano, vituo vya utoaji huduma na vituo vya kutunzia data. Katika kipindi kinachoishia Mwezi Aprili, 2023 kazi zifuatazo zimefanyika:




(i) Ununuzi wa mitambo kwa ajili ya vituo **112** vya kutolea Huduma (transmission and power equipment) umekamilika ambapo usimikaji umefanyika kwenye vituo **61** vya kutolea huduma (Point of

Presence-POPs and Optical Line Amplifiers OLA) kwenye maeneo ya Dar es Salaam (TTCL House na Kijitonyama), NIDC DSM, Chalinze Tanesco, Chalinze TTCL, Manga, Hale TANESCO, Hale TTCL, Tanga mjini, Horohoro, Mkomazi, Same, Mwanga, Moshi,Arusha mjini, Makuyuni, Babati, Namanga, Morogoro mjini, Kidatu, Ifakara, Kihansi, Iringa mjini, Mtera, Dodoma mjini, Manyoni, Singida mjini, Katesh, Igunga, Mabuki, Shinyanga, Nzega, Tabora, Mwanza, Nassa, Sirari, Musoma, Geita, Biharamulo, Bukoba, Mtukula, Rusumo, Kabanga, Muleba, Manyovu, Kasulu, Kigoma, Mpanda, Sumbawanga, Tunduma, Mbeya, Tukuyu, Kasumolo, Chimala, Makambako, Njombe, Songea, Tunduru, Masasi, Tandahamba, Lindi na Mtwara. Usimikaji pamoja na uunganishaji wa mawasiliano katika vituo vingine 50 unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023;

(ii) Marekebisho ya vyumba vya mitambo 39 vya mkongo wa Taifa wa mawasiliano ili kuongeza ubora wa huduma katika maeneo ya Bariadi, Tukuyu, Miangalua, Kizi, Uvinza, Kibondo, Kabanga, Rusumo, Mutukula, Mabuki, Nassa, Ikwiriri, Mikumi, Kidatu, Ifakara, Njombe mjini, Makambako, Mafinga, Iringa mjini, Hulia, Tunduru, Michiga, Masasi, Tandahimba, Lindi mjini, Mitole, Somanga, Kimanzichana, Chalinze, Bagamoyo, Chunya, Horohoro, Igunga, Kahama, Kilosa, Manga, Nzega, Namanga na Chimala;

(iii) Kufanikiwa kusimika nguzo za zege (OFC Poles and Accessories) 10,624 kati ya nguzo 19,915 zitakazotumika kujenga mkongo wa juu kwenye maeneo ya njia za Mkongo. Nguzo hizi pia zitatumika pia na TANESCO kwa ajili ya kupitisha nyaya za umeme kwenye maeneo ambayo hayana umeme;

(iv) Uendelezaji wa Ujenzi wa njia mpya za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye jumla ya Kilomita 4,442 mradi ambao umewezesha ajira 1,315 kwa wananchi;

(v) Kukamilisha taratibu za zabuni ya kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa Kituo cha Kuhifadhi Data Zanzibar;

(vi) Kujengea uwezo wataalamu 114 wa usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa nchini; pamoja na wataalamu wengine 817 katika eneo la usalama mtandao; na

(vii) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa jumla ya vijiji 2,212 vyenye changamoto ya mawasiliano nchini. Taarifa ya upembuzi yakinifu imeandaliwa kwa ajili ya kupata fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ili kuwezesha ujenzi wa jumla ya minara 758.

## Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi

39. **Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa Anwani za Makazi ni miundombinu inayotambulisha mahali halisi ambapo kitu, mtu au huduma inapopatikana pamoja na kuwezesha urahisi wa ufikiwaji wake. Mfumo unarahisisha utoaji na ufikishaji wa huduma za kiuchumi na kijamii hadi mahali alipo mwananchi sambamba na kuwezesha biashara mtandao (e-Commerce). Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:




Kufanya uhakiki wa taarifa za Anwani za Makazi kwenye Halmashauri 23, ambazo ni Majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha, Mbeya na Tanga, Manispaa za Moshi, Kindondoni, Temeke, Ubungo, Kigamboni, Ilemela, Mjini, Magharibi A, Magharibi B; na Halmashauri za Kaskazini A, Kaskazini B, Chakechake, Meru, Mtwara Mikindani, Micheweni, Kusini na Kati. Kupitia zoezi hili Anwani za Makazi katika maeneo hayo zimehakikiwa pamoja na Anwani mpya 283,762 ambazo zimeongezeka kutoka 12,385,956 zilizokusanywa wakati wa operesheni na hivyo kuwa na jumla ya Anwani za Makazi 12,669,718 sawa na ongezeko la asilimia 2.2;

(ii) Kuratibu matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi ambapo baadhi ya Taasisi zimeanza kutumia Mfumo huo kama vile Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuboresha taarifa za wamiliki wa viwanja, pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuboresha tarifa za walipa kodi. Taasisi nyingine zilizounganishwa au kuwa kwenye hatua za mwisho za kuunganishwa ni NIDA, LATRA, TANESCO na BRELA.Majadiliano na TANAPA yanaendelea ya namna ya Mfumo husika kutumika kwa ajili ya kusaidia shughuli za utalii. Aidha, Wizara imetoa miezi sita kuanzia tarehe 01 Mei, 2023 kwa taasisi zote zinazotoa huduma kwa wananchi (Sekta ya Umma na Binafsi) kuhakikisha zinatumia mfumo wa Anwani na Makazi;

(iii) Kuboresha Mfumo wa kidijitali wa Anwani za Makazi unaojulikana kwa jina la NaPA ili kuimarisha shughuli za ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya taarifa. Maboresho haya yanalenga kuziwezesha Taasisi zote za Serikali na binafsi kutumia taarifa hizo katika kutoa na kupokea huduma, pamoja na kuwawezesha wananchi kutafuta, kuona na kuifikia sehemu mahsusi katika kutekeleza shughuli zao za kila siku kwa kutumia NaPA;

(iv) Kuandaa Mpango wa miaka mitano wa kuendeleza Mfumo wa Anwani za Makazi;

v) Kufanya mapitio ya baadhi ya sheria, Kanuni na Matamko (Establishment order) zinazoguswa na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ambazo ni pamoja na; The Electronic and Poastal Communication Act CAP 306; The Roads Act CAP 167; The National Housing CooporationAct CAP 295; Electronic and Postal Communication (Postal) Regulations 2018; Kanuni za Anwani za Makazi katika mamlaka za miji za mwaka 2022; Kanuni za Anwani za Makazi katika Halmashauri za Wilaya za mwaka 2022; Tanzania Buildings Agency (Establishment) Order, 2003; The Executive Agencies (The Tanzania National Roads Agency) (Establishment) Order, 2000; na The Executive Agencies (Tanzania Rural and Urban Roads Agency) Establishment Order, 2017. Kazi hii itakamilika katika mwaka wa fedha 2023/24;

(vi) Kufanikiwa kutoa elimu kwa umma kwa Makundi mbalimbali ya wadau wakiwemo, Watumishi wa Umma, Wafanyabiashara, wajasiriamali, na washereheshaji kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi na matumizi yake; na

(vii) Kufanikiwa kutunga Kanuni ndogo za usimamizi wa Anwani za Makazi ambazo zimetumika katika kutekeleza mradi huu.

## Mradi wa Tanzania ya Kidijitali

40. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianza kutekelezwa rasmi Mwezi Novemba, 2021 baada ya Serikali na Benki ya Dunia kusaini Mkataba wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 150. Mradi huu unalenga kuboresha na kukuza maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kufikisha huduma za mawasiliano na utoaji wa huduma za kidijitali kwa Wananchi. Vilevile, mradi huu unalenga kuboresha ubunifu pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini. Kazi zilizotekelezwa ni:-



(i) Kupata mtaalam mwelekezi wa uandaaji wa upembuzi yakinifu kuhusu kuanzishwa kwa Taasisi ya TEHAMA na vituo vinne vya Ubunifu wa TEHAMA. Mkataba kati ya Wizara na Mshauri Mwelekezi umesainiwa Mwezi Disemba, 2022 na kazi hiyo itakamilika Mwezi Juni, 2023;

(ii) Kufanyika upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sera na Sheria zinazosimamia TEHAMA. Taarifa ya awali imewasilishwa na Mshauri Mwelekezi na kazi hiyo inarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023;

(iii) Upembuzi yakinifu kuhusu Utengenezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (NISMIS) kazi hiyo inarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023;

iv) Kuandaa Mpango Mkakati wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (NISMIS) unaojumuisha viashiria vya TEHAMA;

(v) Kuhuisha ununuzi wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali (Extension of Government Internet Bandwidth) wenye kasi ya 5Gbps kwa kipindi kinachoishia mwezi Mei, 2023 kwa ajili kuongeza ubora wa upatikanaji wa huduma za Kidijitali zinazotolewa na Serikali. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali wenye kasi ya 50Gbps kwa kipindi cha miaka 15 ijayo upo katika hatua ya tathmini ya zabuni na Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Mei, 2023;

(vi) Kufanyika kwa upembuzi yakinifu wa Teknolojia ya TV White Space itakayosaidia kuongeza huduma ya mawasiliano kwa watumiaji wa intaneti kwenye maeneo ya vijijini na pembezoni mwa nchi kazi hiyo inarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023;

(vii) Kukamilika kwa taratibu za Manunuzi ya vifaa kwa ajili ya upanuzi wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali (Bandwidith Termination Equipment) kuboresha uwezo wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali;

(viii) Daftari la huduma za Serikali kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi (Government Service Directory) limeandaliwa kwa kazi kufanyika kwenye Taasisi 57 za Serikali;

(ix) Kufanyika upembuzi yakinifu kwa ajili ya vituo vya huduma pamoja utakaosaidia kurahisisha utendaji kazi wa vituo hivyo (Business Process re-engeering) kazi hiyo inarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023;

(x) Kukamilika kwa Mpango Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali (Digital economy Framework 2023-2033) utakaosaidia kuongeza matumizi ya kidijitali kwa huduma zinazotolewa na Serikali pamoja na Sekta binafsi. Rasimu ya mkakati

huo inatarajiwa kujadiliwa kweye kikao cha Kamati Kuu Tendaji ya Taifa mwezi Mei, 2023;

(xi) Kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya Mpango wa uendeshaji (Business Operation Model) wa vituo vya Huduma Pamoja utakaosaidia kurahisisha utendaji kazi wa vituo hivyo Mkataba kati ya Wizara na Mshauri Mwelekezi umesainiwa mwezi Oktoba, 2022 na kazi hiyo itakamilika mwezi Mei, 2023;

(xii) Kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya Biashara Mtandao (e-commerce redness) utakaosaidia kupata taarifa za watumiaji wa biashara mtandao nchini na uratibu wa Biashara husika. Mkataba kati ya Wizara na Mshauri Mwelekezi umesainiwa mwezi Novemba, 2022 na kazi hiyo itakamilika mwezi Mei, 2023;

(xiii) Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa minara mipya 763 ilifunguliwa tarehe 31 Januari, 2023 na mikataba imesainiwa tarehe 13 mei, 2023;

(xiv) Maandalizi ya uongezaji wa kasi ya Mawasiliano Vijijini Minara 488, na Mikataba imesainiwa tarehe 13 mei, 2023;

(xv) Wataalam 17 wa Serikali walipatiwa mafunzo ya usalama wa mifumo (Certified Information System Security Professional);

(xvi) Ununuzi wa vifaa vya upanuzi wa Mtandao wa Serikali wa Mawasiliano (Active and passive Equipment for GovNet) kazi hii ipo hatua ya tathmini na tunatarajia kusaini Mkataba mwezi Juni, 2023; na

(xvii) Ununuzi wa vifaa vya kuboresha vituo mahiri vya kuhifadhi Data (National Internet Data Center - NIDC na Government Data Center - GDC) kazi hii ipo hatua ya tathmini na tunatarajia kusaini Mkataba mwezi Juni, 2023.

## Mradi wa Habari kwa Umma

41. **Mheshimiwa Spika,** Mradi una lengo la kuwezesha ukusanyaji, uchakataji, uandaaji na usambazaji wa habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo Sera, Mikakati, Programu na Miradi zinazotekelezwa na Serikali. Vilevile, kukusanya taarifa za mrejesho kutoka kwa wananchi kwa lengo la kupata maoni ya wananchi katika utekelezaji wa shughuli zake. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kuzalisha vipindi 25 vya Televisheni vya KAZI IENDELEE vinavyoelezea utekelezaji wa miradi ya maendeleo na namna inavyowanufaisha wananchi na kurushwa katika televisheni ya

TBC1. Vipindi hivyo vilihusu Sekta za Kilimo cha umwagiliaji, Viwanda, Ujenzi, Madini, Upanuzi wa Bandari ya Tanga Reli, miradi ya maji na Afya;

(ii) Kuchapisha na kusambaza nakala 5,000 za jarida la NCHI YETU linaloelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ya kimkakati;

(iii) Ununuzi wa Magari matatu kwa ajili utekelezaji wa shughuli za Idara ya Habari-MAELEZO. Aidha, taratibu za manunuzi ya kifaa cha kurushia matangazo mbashara katika vyombo vya Habari na mitandao zimekamilika;

(iv) Kuratibu Mikutano ya Taasisi za Serikali na vyombo vya habari kwa lengo la kutoa taarifa za utekelezaji kupitia vyombo vya habari. Jumla ya Taasisi 48 ziliratibiwa na kutoa taarifa kwa umma kuhusu utekelezaji wa shughuli zake.

### Mradi wa Upanuzi wa Usikivu TBC

42. **Mheshimiwa Spika,** lengo la mradi huu ni kufanya upanuzi wa Usikivu wa redio na televisheni za TBC kwenye maeneo yasiyokuwa na usikivu nchini kwa kununua mitambo, vifaa vya utangazaji, ujenzi wa jengo la Makao Makuu, ununuzi wa Magari na vifaa vya kurusha matangazo mbashara, na kufanya ukarabati, uhifadhi na uboreshaji wa studio za Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika.

#### Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kukamilika kwa taratibu za manunuzi za kuwapata wazabuni kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi wa Usikivu redio za TBC katika maeneo 9 na Mikataba yote imeshasainiwa. Aidha miradi ya upanuzi inaendelea katika maeneo 34 nchini kama yalivyoainishwa katika Kiambatisho Na. 10;

(ii) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa michoro na mifumo kwa ajili ya jengo la Kituo cha Taifa cha Televisheni (TVT) - Mikocheni Dar es Salaam litakalotumika kwa ajili ya Chaneli ya Utalii na utawala;

(iii) Kukamilika kwa taratibu za manunuzi kwa ajili ya Kuimarisha muonekano wa Televisheni kwa kuongeza ung'aavu wa picha (improvement of Television Channels Outlook) – awamu ya pili, ambapo mkataba umeshasainiwa;

(iv) Kukamilika kwa taratibu za manunuzi ya mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring);

(v) Kukamilika kwa taratibu za manunuzi ya kumpata Mzabuni kwa ajili ya ukarabati wa majengo na mifumo ya umeme wa studio za redio na Televisheni;

(vi) Taratibu za Ununuzi wa vifaa vya kurushia Matangazo mbashara ya Redio nje ya studio (Quantum - 9) zimeshakamilika;

(vii) Kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa vifaa vya kurushia Matangazo mbashara ya televisheni na mitandao ya kijamii nje ya studio;

(viii) Ujenzi wa ukuta wa Makao Makuu ya TBC eneo la Vikonje - Dodoma umefikia zaidi ya asilimia 50; na

(ix) Kukamilika kwa taratibu za manunuzi ya kumpata Mzabuni kwa ajili ya Ufungaji wa Mitambo ya redio na TEHAMA katika studio za redio barabara ya Nyerere pamoja na jengo la TBC2 awamu ya pili.

### Mradi wa Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji

43. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unakusudiwa kununua na kufunga mitambo mipya ya uchapaji katika Kampuni ya Magazeti ya Serikali. Kazi zilizotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni:

(i) Ununuzi na upokeaji wa mtambo wa uchapaji wa magazeti na machapisho mengine (Hybrid Web Offset machine) wenye vipande (units) 12;

(ii) Kuendelea na taratibu za ujenzi wa kiwanda ambapo Mkandarasi ameshapatikana na mkataba wa kazi hiyo umeshapata idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Kampuni inaendelea na maandalizi mengine ikiwa ni pamoja na utafutaji wa mali ghafi; na

(iii) Ununuzi wa magari saba, baada ya vibali kwa ajili ya ununuzi wa magari kupatikana kutoka ofisi ya Waziri Mkuu.

### Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA

44. **Mheshimiwa Spika,** lengo la mradi huu ni kujenga Kituo cha Kuendeleza Wataalam, utafiti na ubunifu wa TEHAMA, kuendeleza Vituo vya Kanda vya Kampuni Changa za TEHAMA nchini, Kuwezesha uanzishaji wa vituo vya majaribio vya ubunifu TEHAMA katika Wilaya zote nchini; Kuanzisha kituo cha kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA; na kutengeneza mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu wa TEHAMA nchini. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Aprili, 2023 ni:

i. Kukamilika kwa usanifu wa Kituo kitakachotumika kwa shughuli za Kampuni changa za TEHAMA cha Kanda ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kusaini mkataba na kukabidhi eneo kwa mkandarasi kwa ajili ya kufanya matengenezo na maboresho ya jengo. Kituo hiki kinatarajiwa kuanza shughuli zake mwezi Julai, 2023;

ii. Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa kuainisha mahitaji ya vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya uundwaji wa bidhaa za TEHAMA hapa nchini;

iii. Kufanikiwa kutengeneza mfumo jumuishi utakaowezesha kuwa na taarifa zote za wabunifu wa TEHAMA nchini, kampuni za TEHAMA, Wawekezaji katika huduma na bidhaa za ubunifu katika TEHAMA, Vituo atamizi vya TEHAMA, Vituo vya uendelezaji bunifu za kidijitali pamoja na Taasisi za kifedha zinazotoa mitaji kwa wabunifu wa TEHAMA. Lengo la mfumo huu ni kutambua bunifu hizi ili kupanua wigo wa ukuzaji kwa lengo la kukuza pato la Taifa na kuongeza fursa za ajira kupitia TEHAMA; na

iv. Wabunifu na watengeneza wa bidhaa za TEHAMA Kanda ya Dar es Salaam na Arusha walikutanishwa na kushirikishwa kuhusu azma ya Serikali ya kuanzisha vituo vya ubunifu TEHAMA vya Kanda. Aidha, majadiliano ya namna ya kutengeneza bidhaa zinazokidhi mahitaji ya soko ili ziweze kutoa ajira na kuchangia pato la Taifa yamefanyika ikiwa ni pamoja na kubaini changamoto wanazokumbana nazo na kujadili namna ya kuzitatua kwa pamoja. Jumla ya wabunifu TEHAMA 165 walishiriki kwenye warsha hizi.

# UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

*Jengo la Makao Makuu ya PAPU Arusha Tanzania*

# UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

46. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 469.03. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Taasisi zimekusanya jumla ya Shilingi bilioni 655.5 sawa na asilimia 139.8 ya lengo. Ongezeko la makusanyo hayo limetokana na mauzo ya masafa ambayo ni kiasi cha Dola za Marekani 140,622,200.96 (sawa na Shilingi 327,101,301,653.06) ambayo hayakuwa sehemu ya bajeti ya mwaka 2022/23.

46. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

## Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

47. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 155.9 kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrahaba, ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya mawasiliano, ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA na makusanyo kutokana na mtambo wa Teletraffic Management System (TTMS). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 TCRA imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 476.01 sawa na asilimia 305 ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka. Ongezeko la makusanyo hayo limetokana na mauzo ya masafa ambayo ni kiasi cha Dola za Marekani 140,622,200.96 (sawa na Shilingi 327,101,301,653.06), ambayo hayakuwa sehemu ya bajeti ya mwaka 2022/23.

48. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia huduma za mawasiliano ya Simu, Intaneti, Utangazaji, Huduma za Posta na Usafirishaji wa vipeto kama ifuatavyo:

### Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti

49. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kuboresha usimamizi wa huduma za mawasiliano ya simu nchini ambapo jumla ya laini za simu 997 zilizokuwa zikitumika kwenye mawasiliano ya ulaghai wa mawasiliano ya simu za kimataifa zilisitishwa matumizi yake. Usitishwaji wa laini hizi uliwezesha kubaini matukio mawili ambapo wahusika walikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi. Kutokana na hatua za udhibiti zinazoendelea kuchukuliwa matukio ya ulaghai wa mawasiliano yameendelea kupungua. Aidha, Mamlaka imeendelea kudhibiti vifaa vya kielektroniki vinavyotumika kwenye mawasiliano ya

simu ili kulinda maslahi ya watumiaji. Katika kipindi kinachoishia tarehe 30 Aprili, 2023, jumla ya namba tambulishi 92,643 za vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vilifungiwa baada ya kubainika kuhusika kwenye vitendo vya udanganyifu, wizi au kupotea.

50. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kusimamia zoezi la usajili na uhakiki wa laini za simu nchini ambapo hadi tarehe 30 Aprili 2023, jumla ya laini zinazotumika kwenye mitandao ya simu zimefikia 62,317,168, zote zikiwa zimesajiliwa kwa alama za vidole ikilinganishwa na laini za simu 55,735,114 zilizokuwa zimesajiliwa kwa alama za vidole hadi tarehe 30 Juni, 2022 sawa na ongezeko la laini za simu 6,582,054. Aidha, Serikali kupitia TCRA imeendelea kufuatilia ukuaji wa huduma za kutuma fedha kwa njia ya mitandao ya simu ambapo idadi ya miamala ya fedha kupitia mitandao ya simu imeongezeka kutoka milioni 376.3 kwa mwezi Julai, 2022 hadi kufika milioni 451.0 kwa mwezi Aprili 2023 sawa na ongezeko la asilimia 19.9.

51. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TCRA imeendelea kushirikiana na wadau wakiwemo waingizaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki nchini ili kuweka utaratibu utakaowezesha usimamizi wa vifaa hivyo pale vinapofika mwisho wa matumizi ili kupunguza athari zinazoweza kutokea kwenye mazingira kutokana na uwepo wa vifaa hivyo. Kufuatia utekelezaji wa mpango huu vifaa vyote vya mawasiliano ya kielektroniki hukaguliwa kabla ya kuingia nchini ili kuhakikisha kuwa vifaa vyote vinavyoingia havijafika mwisho wa matumizi. Utekelezaji wa ukaguzi wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinavyoingia nchini unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2023.

52. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na usimamizi wa miundombinu ya Mawasiliano (minara ya Simu, Redio na Televisheni), ili kuwalinda watumiaji wa huduma za mawasiliano na wananchi wanaoishi karibu na miundombinu hiyo. Upimaji wa kuhakiki kiwango cha mionzi itokanayo na minara/vifaa vya mawasiliano (Radio Frequency Electro Magnetic Field radiations - EMF) ilifanyika katika mikoa tisa. Matokeo ya upimaji huo yanaonyesha kuwa kiwango cha juu kilikuwa 3.676 V/m (Volt per Meter) ambacho ni chini ya kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP) ambacho ni 41.98 V/m. Hali hii inaashiria kuwa, kiwango cha mionzi kutoka kwenye minara ya mawasiliano iliyopimwa hakijavuka kiwango cha juu cha mionzi kama ilivyoelekezwa na ICNIP hivyo kuwa salama kwa watumiaji wa mawasiliano.

53. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na jukumu la kukagua na kuhakiki ubora wa viwango wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki hapa nchini kwa lengo la kulinda usalama na afya za wananchi. Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2023 TCRA ilipokea maombi ya ukaguzi wa vifaa vya kielektroniki 512 kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi. Maombi 423 sawa na asilimia 83 yalikidhi vigezo na kuidhinishwa kwa matumizi, maombi 76 sawa na asilimia 15 yapo kwenye hatua mbalimbali za ukaguzi na maombi 13 sawa na asilimia 2 yalikataliwa kwa sababu ya kutokidhi vigezo.

54. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia usalama mtandaoni kwa kufanya tathimini ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa lengo la kubaini madhaifu ya kiusalama na kushauri juu ya hatua za kurekebisha na kujilinda na matishio ya usalama mtandaoni. Kufikia mwezi Aprili, 2023, TCRA ilifanya uchambuzi wa anwani za kompyuta zenye viashiria vya kushambuliwa na kutoa mashauri ya usalama mtandaoni (Security Advisories) kwa Taasisi za Umma na binafsi ambapo mashauri 658 yalichambuliwa ukilinganishwa na mashauri 920 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/22 ili hatua stahiki ziweze kuchukulia kuimarisha usalama wa mifumo yao.

55. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kukagua ubora wa huduma za mawasiliano zinazotolewa na watoa huduma. Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2023, TCRA ilipima ubora wa huduma za mawasiliano ya simu inayotolewa na makampuni ya simu hapa nchini. Katika uhakiki huo wa ubora wa mawasiliano kutoka kwa watoa huduma za simu, ilibainika kuwa kuna mapungufu ya muunganisho usioridhisha, ubora hafifu wa huduma za sauti na data na kukatika kwa simu kabla haijaunganishwa. Aidha, TCRA ilifanya ukaguzi kwa watoa huduma za intaneti 38 kati ya 44 pamoja na miundombinu yao ili kubaini endapo kuna ukiukwaji katika utoaji wa huduma za intaneti pamoja na huduma za simu za ndani na nje ya nchi. TCRA ilibaini katika ukaguzi huo kuwa kuna baadhi ya watoa huduma wamesimika mikongo ya mawasiliano kwa wateja wa mwisho (Last mile connectivity) bila kuwa na leseni inayowaruhusu kusimika mikongo hiyo (Network Facility Licence). Tayari TCRA imeshachukua hatua kwa kuwaagiza watoa huduma kuchukua hatua za haraka kurekebisha mapungufu yaliyobainika ikiwemo kufanya maombi ya leseni ndani ya mwezi mmoja tangu kupokea maagizo hayo.

56. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2023, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea na upangaji wa masafa kwa Huduma za Mawasiliano, Mamlaka ilifanya mnada wa masafa tarehe 11 Oktoba, 2022 kwenye

bendi za 700 MHz, 2300 MHz, 2600 MHz na 3500 MHz ambayo yanatumika kwa ajili ya mawasiliano ya simu na intaneti katika kuwezesha huduma za 4G na 5G nchini. Makampuni manne ya ndani yalifanikiwa kushinda na kupata leseni za masafa kwenye bendi za 700 MHz, 2300 MHz, 2600 MHz na 3500 MHz. Thamani ya mauzo hayo ni Dola za Marekani 187,496,267.94, ambapo yalifanyika malipo ya awali kiasi cha Dola za Marekani 93,748,133.97 sawa na Shilingi 218,067,534,427.62 ambazo ni asilimia 50. Tarehe 25 Aprili, 2023, makampuni yote manne yalikuwa yamekamilisha malipo ya awamu ya pili kiasi cha Dola za Marekani 46,874,066.98 sawa na Shilingi 109,033,767,202.18 ambazo ni asilimia 25 kwa mujibu wa masharti ya leseni zao.

57. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2023 matumizi ya anwani za kikoa cha kitaifa (dot tz) yameongezeka kutoka 24,749 Mwezi Julai, 2022 na kufikia 27,771 Mwezi Aprili, 2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.2.

### Usimamizi wa Huduma za Maudhui Nchini

58. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa huduma za utangazaji, kumekuwa na ongezeko la vituo vitano vya Utangazaji wa maudhui ya ndani ya kulipia ukilinganisha na ongezeko la kituo kimoja kwa kipindi kama hiki mwaka uliopita. Ongezeko hili limetoa fursa ya ajira kwa wasanii wa ndani kwenye maudhui yenye muktadha wa filamu, michezo ya kuigiza, tamthilia na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania kwenye michezo ya ligi ya mpira ya ndani na ngumi za kulipwa. Vituo vya Utangazaji vinaaswa kuendelea kuhabarisha Umma kwa kuzingatia maadili, weledi, Sheria na Kanuni za Utangazaji.

59. Mheshimiwa Spika, TCRA imeendelea kusimamia maudhui kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utangazaji. Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la makosa kwa asilimia 5 ukilinganisha na kipindi kama hiki mwaka uliopita. Makosa ambayo yamekuwa yakijirudiarudia ni lugha zisizo na staha kwa baadhi ya watangazaji, hasa kwenye vipindi vya uchambuzi wa masuala ya kijamii, siasa, elimu na vipindi vya mahojiano. Vilevile, Watangazaji kutozingatia maadili ya utangazaji ikiwa ni pamoja na kutokuwa na mizania ya Habari na kurusha tamthilia na vipindi vya miziki ambavyo havijapata kibali kutoka BASATA au Bodi ya Filamu. Makosa mengi yamesababishwa na vituo kuajiri watangazaji kwa vigezo vya vipaji zaidi kuliko elimu ya uandishi. Utaratibu wa kuwaendeleza watangazaji wenye vipaji kupitia mafunzo ya muda mfupi unaandaliwa kwa kushirikiana na vyuo vya uandishi wa Habari.

60. Mheshimiwa Spika, TCRA imeendelea kutoa elimu kwa watangazaji, waandaaji wa vipindi *(producers)* na Wahariri wa vipindi vya Utangazaji kama hatua ya kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Mamlaka iliratibu mafunzo mara nane kwa ajili ya kutoa elimu ya Sheria na Kanuni za Utangazaji kwa watoa huduma za maudhui mtandaoni na vituo vya utangazaji hii ikiwa ni asilimia 80 ya lengo. Mafunzo haya yanakusudiwa kukabiliana na tatizo la kutofahamu Sheria na Kanuni za Utangazaji. Vilevile, kwa kipindi cha mwaka huu kumekuwa na wimbi la michezo ya kubahatisha kwenye vituo vya Utangazaji. TCRA kwa kushirikiana na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha iko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Matangazo ya biashara ili kupunguza wimbi la michezo hii kwenye vyombo vya Utangazaji.

61. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia Sheria na kuboresha mfumo wa utoaji leseni unaowezesha kutoa leseni kwa njia ya mtandao. Katika kipindi kinachoishia tarehe 30 Aprili, 2023 jumla ya Leseni 448 zimetolewa ikilinganishwa na leseni 657 zilizotolewa kwa kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2021/22. Leseni zilizotolewa za maudhui ya redio na televisheni 18, leseni za Maudhui Mtandaoni *(Online Content Services)* 67, leseni ndogo za madaraja mbalimbali *(Class Licences)* 354, na leseni za Huduma za Mawasiliano *(Application Service Licences)* tisa. Aidha, Mfumo wa Tanzanite Portal umewezesha kuwa na dirisha moja la utoaji leseni na nambari za Mawasiliano, utoaji wa vyeti vya uhakiki na kanzidata ya taarifa za wateja.

## Usimamizi wa Huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto

62. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu utendaji kazi wa Sekta ya Posta ili kuhakikisha ufanisi na ubora katika huduma zinazotolewa ili kutoa mchango chanya katika maendeleo ya Taifa letu. Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili 2023, TCRA imetoa leseni kwa Watoa Huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto 26 na hivyo kufanya jumla ya leseni hai kuwa 96. Baada ya kukamilika kampeni ya uwekaji wa anwani za makazi, TCRA imeendesha kampeni kabambe ya kuelimisha taasisi, watoa huduma za posta na wananchi ili kufahamu matumizi sahihi ya mfumo wa anwani za makazi. Mkazo mkubwa umekuwa ni kuhimiza matumizi ya anwani za makazi katika kufanikisha biashara – mtandao *(e-commerce)* hasa kwa wakati huu ambapo nchi yetu inaendesha uchumi wa kidijitali.

63. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilifanya kaguzi za mara kwa mara kwa kuzingatia masharti ya leseni na kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ili kubaini mapungufu yaliyopo na kuchukua hatua stahiki. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 jumla ya ofisi 49 za posta na watoa huduma wote wa usafirishaji wa vifurushi katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita, Mara, Bukoba, Mbeya, Iringa, Njombe, Rukwa na Dodoma walifikiwa na kukaguliwa. Aidha, hatua stahiki za kiudhibiti zilichukuliwa kwenye maeneo yaliyobainika kuwa na mapungufu. Jumla ya wasafirishaji wa vipeto 19 walibainika kutokuwa na leseni za TCRA ambapo walipewa barua za onyo na kuelekezwa utaratibu wa kuomba leseni stahiki.

64. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia mfumo wa kupanga, kugawa na kuhuisha Postikodi nchini, ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa postikodi kwa wananchi kupitia mfumo wa jumbe fupi (SMS). Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2023 jumla ya SMS zote 178,602 zilijibiwa kwa wananchi kuhusu kupata postikodi za maeneo yao. Aidha, TCRA imetoa postikodi kwa taasisi za Serikali na inaratibu kazi ya kuhuisha viwango vya anwani za makazi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

65. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa elimu kwa umma kuhusu huduma za mawasiliano, uhakiki wa laini za simu za kiganjani kwa njia ya semina na vipindi vya redio na runinga katika mikoa mbalimbali ya Tanzania bara na Visiwani. Katika kuelimisha umma, TCRA ilifanya vipindi 40 vya Mawasiliano kwa Maendeleo, vipindi 40 vya Bambo la Mtaa ambavyo vilifikia hadhira ya watu takribani milioni 30. Pia Mamlaka ilifanya semina katika makundi tofauti, ambapo ni wadau wa Televisheni mtandao, Wahariri, Walemavu, watangazaji wa redio jamii, Semina kwa washawishi mtandaoni *(Social media Influencers)* na Watangazaji wa redio za Kitaifa. Aidha, Mamlaka ilitoa Elimu kwa Umma kupitia maonesho ambapo TCRA ilifanikiwa kushiriki maonesho 10 yaliyofanyika Tanzania Bara na Zanzibar yakiwemo Maonesho ya Sabasaba, Nanenane, na Wiki ya Huduma za Fedha.

### Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

#### (a) Mradi wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kieletroniki (National Public Key Infrastructure)

66. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kielektroniki (National Public Key Infrastratucture - NPKI). Mradi huu utakapokamilika

utawezesha uhakika wa usalama kwenye utumaji na upokeaji wa taarifa kwa njia ya kielektroniki kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine. Aidha, Zabuni ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu ilishatangazwa na kupata maombi ya wazabuni saba na utaratibu wa kutoa zabuni unaendelea.

### (b) Ujenzi wa Maabara ya Uidhinishaji Vifaa vya Mawasiliano (Type Approval Laboratory)

67. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na mradi wa ujenzi wa Maabara ya uidhinishaji vifaa vya mawasiliano. Kwa kuanzia, TCRA inaanzisha maabara ya kupima mionzi inayotokana na simu za mkononi *(Specific Absorption Rate Lab)* na Maabara ya kupima Masafa ya kifaa *(Radio Frequency Lab)*. Maabara hizi zinalenga kuwa na vifaa salama vya mawasiliano na kuhakikisha hakuna muingiliano wa mawasiliano na hivyo kuwa na huduma bora zaidi za mawasiliano nchini. Mradi huu unaendelea kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2023.

### (c) Ujenzi wa Jengo la PAPU na TCRA (PAPU House Building)

*68.* **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kusimamia ujenzi wa Jengo la Umoja wa Posta Afrika *(Pan African Postal Union - PAPU)* Jijini Arusha. Mradi huu unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania (asilimia 40) na Umoja wa Posta Afrika (asilimia 60). Jengo hili litatumika kama Makao Makuu ya Shirika la Posta la Afrika na Ofisi za Kanda ya Kaskazini za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 98. Mradi unarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023 na kuzinduliwa rasmi mwezi Agosti, 2023.

### (d) Ujenzi wa Jengo la Ofisi za TCRA Dodoma

69. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ipo katika utekelezaji wa ujenzi wa jengo la ofisi katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma. TCRA imekamilisha utayarishaji wa mahitaji ya awali ya Jengo *(Inception Report)* na imeendelea kusimamia kazi ya usanifu wa ujenzi wa Jengo. Kwa sasa taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

## Shirika la Posta Tanzania (TPC)

70. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 Shirika la Posta Tanzania lilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 40,943,300,000. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Shirika lilikusanya jumla ya Shilingi 23,989,637,391 sawa na asilimia 59 ya lengo la mwaka kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni usafirishaji wa barua, Usafirishaji wa

nyaraka kwa njia ya haraka (EMS), fedha na uwakala, Biashara ya kubadili fedha za Kigeni, biashara mtandao pamoja na miliki.

71. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Shirika lilipanga kuzalisha faida kabla ya kodi ya Shilingi bilioni 3.1. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2023 Shirika limefanikiwa kuzalisha faida kabla ya kodi Shilingi bilioni 1.7 ikiwa ni asilimia 54 ya lengo.

72. Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuboresha huduma kwa kutumia teknolojia za kisasa, Shirika limeboresha miundombinu ya mtandao wa eneo mahsusi *(Local Area Network – LAN)* katika ofisi kuu za Posta 12 ikiwemo Dar es Salaam GPO, Mwanza, Dodoma, Arusha, Singida, Kijangwani, Mororgoro, Mbeya, Lindi, Tanga, Kagera na Kigoma. Pia Shirika linaendelea kukamilisha kuboresha mtandao wa ofisi 14 za Posta za Mzizima, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Mpanda, Songwe, Shinyanga, Tabora, Geita, Mara, Kilimanjaro, Chakechake, Iringa na Njombe.

73. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania limeendelea kufanya maboresho ya kiufundi ya mfumo wa Ramani ya Kidijitali *(Postal Digital Map)* na kufanya majaribio tayari kwa kuanza matumizi. Mfumo huu utaongeza ufanisi na kuboresha ufikishaji wa huduma za Posta kwa wananchi kwa kupitia Mfumo wa Anwani za Makazi.

74. Mheshimiwa Spika, katika kuwasogezea wananchi Huduma za Serikali, Shirika limeendelea kusimamia vituo viwili vya Huduma Pamoja *(Dar es Salaam na Dodoma)* na kufanikiwa kuanzisha vituo vitatu vipya vya Tanga, Mbeya na Mwanza. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2023 Shirika limehudumia jumla ya wananchi 86,934 tangu kuanzishwa kwa huduma hizi mwezi Julai, 2021.

75. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania limefanikiwa kuingia mkataba na ASYAD Group ya Oman kwa ajili ya kujenga kituo cha kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao. Mradi huo utaimarisha mnyororo wa usafirishaji na Biashara Mtandao kimataifa;

76. Mheshimiwa Spika, Katika kuboresha mahusiano ya Kitaifa na Kimataifa katika utoaji wa huduma za Posta, Shirika la Posta Tanzania limefanikiwa kuanzisha ofisi ya Usimamizi wa miradi na shughuli za Umoja wa Posta Duniani kwa Kanda ya Afrika Mashariki iliyopo Ofisi za Shirika la Posta Tanzania, Jijini Dar es Salaam. Aidha, Ofisi hii inasimamiwa na Mtanzania na itasaidia kukuza ushirikiano kati ya Tanzania na Umoja wa Posta Duniani.

77. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania limefanikiwa kuzindua stempu ya pamoja *(Joint Stamp)* na Posta ya Oman ambayo imeendelea kuuzwa katika soko la

stempu kimataifa. Aidha, uzinduzi wa stempu hiyo utasaidia kuitangaza nchi katika nyanja za utalii, kupanua wigo wa masoko, kukuza utamaduni wa nchi ya Oman na nchi nyingine za Ghuba ya Uajemi.

78. Mheshimiwa Spika, Shirika limefanikiwa kupata mradi wenye thamani ya Dola za Marekani 120,000 kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa utumaji na upokeaji fedha kwa njia ya kielektroniki *(posta cash e-wallet)*. Mradi umelenga kuwezesha upatikanaji wa huduma za malipo kwa wananchi katika huduma za Posta na kuwahudumia wananchi wa kipato cha chini haswa wanaoishi vijijini. Mradi huu unaratibiwa na Mfuko wa Usaidizi wa Kiufundi wa Huduma Jumuishi za Fedha *(Financial Inclusion Technical Assistance Facility)* wa Umoja wa Posta Duniani.

79. Mheshimiwa Spika, Itakumbukwa kwamba nchi yetu ilifanya zoezi la Sensa ya watu na makazi Mwezi Agosti, 2022 katika zoezi hilo, Shirika la Posta Tanzania lilishiriki kikamilifu katika zoezi hilo kwa kusafirisha na kusambaza vishikwambi na vifaa vingine vya sensa nchi nzima.

80. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania linaendelea kuboresha ofisi zake kote nchini. Kufikia mwezi Aprili, 2023 Shirika limeandaa michoro sanifu, makadirio ya gharama za ukarabati na kuanza manunuzi ya kumpata mkandarasi wa ukarabati wa majengo sita ya ofisi za Posta Libya, Sokoine, Meru, Pamba Road, Makambako na Mpwapwa.

### Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

81. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 202,851,880,319. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2023 Shirika limefanikiwa kukusanya Shilingi 104,037,521,796.63 sawa na asilimia 51.3 ya lengo. Makusanyo hayo yametokana na huduma zinazotolewa na Shirika ambazo ni simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

82. Mheshimiwa Spika, Shirika limeboresha usambazaji wa muda wa maongezi kwa kujikita katika usambazaji wa njia ya kielektroniki ambayo inamuwezesha mteja kujinunulia muda wa maongezi mwenyewe muda wowote anapokuwa na mahitaji. Mpaka sasa wateja wa Shirika wana uwezo wa kununua muda wa maongezi wa TTCL kwa kutumia T-Pesa, M-Pesa, Airtel Money, Tigo Pesa na Halo Pesa. Pia wateja wana uwezo wa kununua muda wa maongezi kwa kupitia huduma za "sim banking" katika benki za CRDB, NMB na Bando App. Shirika pia limewezesha wateja wake kununua muda wa maongezi katika mawakala wote wanaotoa huduma za kidijitali za Selcom.

83. **Mheshimiwa Spika,** Shirika lilifanikiwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa vocha kwa kuongeza idadi ya Mawakala wa vocha na SIM Card kufikia 177 ambapo ni ongezeko la asilimia 22 ya mawakala 145 waliokuwapo mwezi Aprili, 2022. Kutokana na mabadiliko ya hali ya soko, pia mkakati wa kuwafikia wateja wote mahali walipo, Shirika kwa sasa limejikita katika kuhakikisha usambazaji wa muda wa maongezi unafanyika kidijitali na kielektroniki. Tafiti za kibiashara zimethibitisha kuwa njia ya usambazaji ya kidijitali ni njia mahususi na inayoweza kuwafikia wateja wengi kwa haraka na gharama nafuu.

84. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kujenga, kusimamia na kuendesha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) na Kituo cha Taifa cha Kutunza Data (NIDC). Mwezi Novemba, 2022 Shirika lilikabidhiwa jukumu la kutekeleza mradi wa mkongo kwa mwaka 2022/23 ambapo hadi tarehe 31 Disemba, 2022 Shirika lilikamilisha tathmini ya kiufundi kwenye vituo vipya vya Halmashauri 31 ambavyo vilipangwa kuhusika kwenye miradi. Taratibu za manunuzi zimekamilika na mkataba huo umesainiwa tarehe 17 Aprili, 2023 na utahusisha vituo 23 pamoja na upanuzi wa njia kuu ya Kaskazini na Magharibi kutoka 800Gbps hadi 2,000Gbps.

### Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (National Internet Data Centre - NIDC)

85. **Mheshimiwa Spika,** Kituo kilianzishwa mwaka 2015 ikiwa ni sehemu ya mradi wa Mkongo wa Taifa na kina hadhi ya daraja la tatu (tier 3) kwenye viwango vya Kimataifa. Huduma zinazotolewa na kituo ni upangishaji wa vifaa *(colocation)*, upangishaji wa nafasi kwenye mashine *(virtual servers)*, kutunza data kwa matumizi ya baadae *(storage)* na huduma za kuweka tovuti za wateja ili zipatikane kwenye wavuti ulimwengu *(web hosting)*.

86. **Mheshimiwa Spika,** Kituo kimekuwa kikiendelea kufanya maboresho na usimamizi wa mfumo wa ukusanyaji kodi kwa njia ya kieletroniki ujulikanao kama e-RCS *(Electronic Revenue Collection System)*. Mfumo huu unakusanya kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Ushuru wa Bidhaa *(Excise Duty)* kutoka kwenye miamala inayofanywa na Kampuni za simu nchini. Mfumo wa e-RCS umekuwa ni msaada mkubwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwani umeondoa ile dhana ya mfanyabiashara kujifanyia makadirio ya kiwango cha kulipa kodi *(Self Assessment)* katika eneo la ulipaji kodi.

87. **Mheshimiwa Spika,** kituo kimeunganisha wateja **240** ambao kinaendelea kuwahudumia toka kuanzishwa kwake. Kati ya hao wateja **120** ni Taasisi za Serikali na wateja **120** ni taasisi binafsi. Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2023 kiasi cha **Shilingi bilioni 4.41** zimekusanywa sawa na **asilimia 78.5** ya lengo.

## Kampuni Tanzu ya T-Pesa

88. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendesha kampuni tanzu ya TTCL Pesa (T-Pesa), Shirika limetekeleza mambo yafuatayo:

(a) Kufanikiwa kuongeza idadi ya mawakala wa T-Pesa kutoka **14,399** waliosajiliwa *(Biometric registered)* mwezi Aprili, 2022 hadi kufikia mawakala **15,739** mwezi Aprili, 2023 ambapo ni ongezeko la **asilimia 9**, pia ni sawa na **asilimia 87** ya lengo; na

(b) Kupanua wigo wa uwakala wa kuuza muda wa maongezi, matumizi ya N-CARD na huduma za tiketi mtandao kwa kushirikiana na wadau. Hadi sasa Shirika linashirikiana na makampuni ya simu (MNOs) kama vile Tigo, Airtel, na Vodacom katika kuuza muda wa maongezi na matumizi ya N-card. Pia Shirika linashirikiana na mabenki kama vile CRDB, NMB na NBC kufikisha huduma kwa urahisi kwa wateja, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 huduma ya N-Card imefikisha jumla ya mawakala **89** na wateja **2,571,828** kutoka mawakala na wateja **1,500,000** waliokuwepo mwezi Aprili, 2022 ambapo ni ongezeko la **asilimia 37** na **42** mtawalia.

## Miradi ya Maendeleo

89. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Shirika limetekeleza miradi ifuatayo:

(i) Usimikaji wa njia mbadala ya Mkongo yenye ukubwa wa 100Gbps kwenda Zanzibar. Njia hii inatumiwa na ZICTIA kwa upande wa Zanzibar kwenye uimarishaji wa utoaji huduma za mawasiliano za uhakika kupitia maunganisho yaliyofanywa baina ya Mkongo wa Taifa (NICTBB) na Mkongo wa Zanzibar;

(ii) Ufikishwaji wa huduma za Mkongo kwenye Wilaya ya Handeni pamoja na kijiji cha Msomera wenye jumla ya urefu wa Kilomita **94.1** pamoja na ufikishwaji wa huduma za 2G/4G kwenye kijiji hicho;

(iii) Ufikishwaji wa huduma za Mkongo kwenye Wilaya ya Rorya wenye urefu wa Kilomita **21** kutokea kijiji cha Mika kwenda Ingilijuu ambayo ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya;

(iv) Ufikishwaji wa huduma za Mkongo kwenye Mbuga ya Serengeti eneo la Sasakwa umbali wa Kilomita 87 kwa ajili ya kuboresha huduma za mawasiliano kwenye hoteli za kitalii zilizopo kwenye maeneo hayo;

(v) Kufungua kituo kipya cha utoaji huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) mjini Tarime;

(vi) Upanuzi wa njia za kimataifa za mawasiliano ya Intaneti kutoka kiwango cha 18.7Gbps hadi 67.5Gbps sawa na ongezeko la asilimia 261. Upanuzi wa njia umelenga kuboresha huduma za intaneti zinazotolewa na Shirika kwa taasisi za Serikali na wateja binafsi;

(vii) Usimikaji wa miundombinu ya mawasiliano kwenye eneo la mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Julius Nyerere lililopo Rufiji pamoja na maeneo jirani yanayozunguka eneo la mradi. Jumla ya vituo vipya 12 vya mawasiliano ya 2G/4G vimejengwa kwenye maeneo hayo; na

(viii) Usimikaji wa miundombinu ya mawasiliano kwenye vituo 87 chini ya miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote nchini (UCSAF).

## Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

90. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) lilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi 15,809,165,000 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato vya ndani, ambavyo ni matangazo ya biashara, udhamini wa vipindi na matangazo mubashara kupitia vyombo vyake vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 TBC ilikusanya jumla ya Shilingi 9,334,521,635.76 sawa na asilimia 59 ya lengo.

91. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imendelea kupanua usikivu wa redio hasa maeneo ya mpakani kwa kujenga mitambo ya masafa FM. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2023 ;

Miradi iliyokamilika kwa asilimia 100 na kuzinduliwa tarehe 27 Aprili, 2023 kama sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Unguja katika Wilaya sita za: Same (Kilimanjaro), Kahama (Shinyanga), Bunda (Mara), Nkasi (Rukwa), Kasulu (Kigoma) na Karagwe (Kagera) uzinduzi wake unatarajiwa kufanyika Mwezi Aprili, 2023. Miradi mingine iliyokamilika ujenzi wake asilimia 100 kwa ushirikiano kati ya TBC na UCSAF ni katika Wilaya sita za Kyela (Mbeya), Uvinza (Kigoma), Makete (Njombe), Ngorongoro (Arusha), Mlele (Katavi) na Mbinga (Ruvuma). Uzinduzi wa miradi katika Wilaya za Mlele na Mbinga ulifanyika tarehe 10 Januari, 2023.

92. Mheshimiwa Spika, Miradi mingine inayoendelea na utekelezaji katika hatua mbalimbali ni katika maeneo saba ya: Serengeti - Mara (85%), Bariadi – Simiyu (85%), Ileje -Songwe (90%), Njombe (90%), Kilwa – Lindi (90%), Unguja (90%) na Pemba (90%) ambayo inatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2023. Fauka ya hayo TBC inaendelea na Upanuzi wa Usikivu wa redio katika Wilaya tisa za: Kalambo – Rukwa, Liwale – Lindi, Rufiji – Pwani, Kakonko – Kigoma, Mufindi – Iringa, Kaliua – Tabora, Igunga – Tabora, Manyoni – Singida na Karatu – Manyara. Miradi ya upanuzi wa Usikivu redio za TBC inayotekelezwa kwa ushirikiano na UCSAF ni katika Wilaya tano za: Chunya – Mbeya, Kiteto – Manyara, Chemba – Dodoma, Kyerwa –Kagera na Mkinga – Tanga. Miradi hii inatarajia kukamilika mwezi Agosti, 2023.

93. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TBC imeendelea na ufungaji wa mitambo na vifaa vya kisasa vya kidijitali katika studio tisa za redio Barabara ya Nyerere. Awamu ya kwanza imekamilika Mwezi Septemba, 2022 kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.03 ambapo studio tano za TBCTaifa, TBCFM na TBCInternational zimeunganishwa na mifumo ya TEHAMA hivyo kutumika kupokea na kutangaza matangazo mubashara kidijitali na kuwezesha kuwafikia wasikilizaji wengi zaidi kupitia mitandao ya kijamii. Awamu ya pili ya ufungaji wa mitambo na vifaa vya kidijitali inaendelea kwa studio nne.

94. Mheshimiwa Spika, TBC pia imeendelea na maboresho ya studio za televisheni kwa kufunga mitambo ya kidijitali (Full HD) ili kuongeza ung'aavu na ubora wa picha. Kazi ya kufunga mitambo na mifumo ya TEHAMA imefikia asilimia 95. Maeneo mengine ya studio za televisheni yanayofungwa mitambo, vifaa na mifumo ya kidijitali ni katika studio za televisheni Makao Makuu – Dodoma, Studio za chaneli ya Kiingereza na TBC mtandao Mikocheni Dar es Salaam. Wakati huo huo, TBC imeendelea na maboresho ya mazingira ya kazi maeneo ya chumba cha habari, ofisi za TBConline kwa kufunga samani mpya za ofisi.

95. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kuwa maeneo ya mitambo na studio za TBC yanalindwa na uvamizi pamoja na usalama wa mitambo, TBC imeendelea na ujenzi wa ukuta kuzunguka studio za redio barabara ya Nyerere jijini Dar Es Salaam na eneo la mitambo ya kurushia matangazo barabara ya pugu. Ujenzi wa ukuta huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

96. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TBC imekamilisha ufungaji wa mfumo wa kurushia matangazo mubashara (Backup uplink system for radio and television), kununua mitambo, vifaa na vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za utangazaji ambavyo ni Magari tisa, vifaa vya kurushia matangazo ya redio mubashara nje ya studio (Quantum)

tisa, mfumo wa kuchanganya picha za televisheni studio (Tricater system), mfumo wa kurushia matangazo mubashara kwa njia ya Satelaiti (FLY AWAY), mitambo ya kurushia matangazo mubashara ya televisheni kwa njia ya mtandao (LIVE U) tisa, kamera za kisasa, mashine za kuhariri picha na sauti, laptop na kamera maalum kwa ajili ya habari za uchunguzi na matumizi ya chaneli ya utalii. Mitambo, vifaa na vitendeakazi hivi viko katika hatua mbalimbali za ununuzi. Uwepo wa mitambo, vifaa na vitendeakazi hivi vitawezesha TBC kutekeleza dhima yake kwa umma kwa weledi na katika mfumo wa kisasa katika upashanaji wa habari.

97. Mheshimiwa Spika, TBC imeboresha maudhui yanayorushwa kwenye redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Ubunifu wa kimaudhui na uwasilishaji umeongeza mvuto kwa vyombo vya habari vya TBC. Mathalani, tarehe 22 Mei, 2022 TBC iliandaa tamasha lijulikanalo kama TUKUTANE KWETU ambapo wasanii na wanamuziki wakongwe walishiriki na kupatiwa tuzo maalum kutambua mchango wao kwa Taifa. Masuala mengine ambayo TBC imetekeleza ni kuendesha mafunzo kwa waandaaji wa vipindi vya elimu kwa umma. TBCTaifa na TBC1 zimeendelea na dhima yake ya kuhabarisha, kuelimisha, kutafakarisha na kulinda maslahi ya nchi kwa kuandaa vipindi vyenye maudhui kutoka maktaba za TBC (Mizani, Tafakuri, Wosia wa Baba, Ndivyo ilivyokuwa, Nyota wa wiki na Lulu za Kiswahili). TBC imeendelea kutangaza na kuonesha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita na kuibua changamoto zinazowakabili wananchi ili zifanyiwe kazi na mamlaka husika ndani ya Serikali. Mathalani kampeni malum inayoendeshwa na TBC kwa sasa ni usafi wa mazingira na upandaji miti nchi nzima. TBC imekuwa ikitangaza mubashara matangazo kuonesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali na ile inayoshirikisha wadau wa sekta binafsi wa ndani na nje ya nchi huku ikitekeleza kaulimbiu yake ya Ukweli na Uhakika.

98. Mheshimiwa Spika, TBC ilifanikiwa kununua haki za kutangaza michuano ya Kombe la FIFA la Dunia nchini Qatar, ambapo jumla ya michezo 28 (TBC1) na michezo yote 64 (TBCTaifa na TBConline) ilirushwa. Kwa upande mwingine, TBC imeendelea kurusha matangazo ya mpira wa miguu Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara msimu wa pili ambapo haki hizo ni kwa kipindi cha miaka kumi mfululizo (2021/22 – 2030/31) kupitia redio na mitandao ya kijamii.

99. Mheshimiwa Spika, Mwezi Novemba, 2022, TBC ilianza rasmi kurusha taarifa ya habari kwa lugha ya Kiingereza, hivyo kupanua wigo wa habari zake na kuwafikia watazamaji wanaotumia lugha hiyo ndani na nje ya nchi na kutekeleza jukumu lake la kuitangaza nchi kimataifa. Aidha, TBC imeendelea kuboresha maudhui

yanayorushwa na Tanzania Safari Chaneli ambayo ni mahsusi kutangaza vivutio vilivyopo nchini kwa kufasiri maudhui ya Chaneli hiyo katika lugha tano za kimataifa za Kiingereza, Kichina, Kifaransa, Kireno na Kiarabu. Maudhui yanayorushwa katika lugha hizi yamekuwa na mchango mkubwa katika kutangaza fursa za utalii zilizopo nchini kimataifa.

100. Mheshimiwa Spika, TBC imeendelea kuwajengea uwezo watumishi waliopo, kuboresha maslahi yao na kuongeza watumishi wapya. Kutokanajitihada hizo, watumishi nane wa TBC wamepata tuzo mbalimbali za uandishi na utangazaji bora ndani na nje ya nchi. Mathalani, mtangazaji wa kipindi cha PAPASO cha TBCFM Bwana D'jaro Deus Arungu (maarufu kama Baba Mzazi au Papaso Master) amepata tuzo za Mtangazaji Bora wa kiume Afrika zilizotolewa nchini Zambia (ZIKOMO MUSIC AWARDS Novemba, 2022), Tuzo za mtangazaji bora wa redio (BONGO MUSICS AWARDS - Mwezi Disemba, 2022) na Tuzo za Mtangazaji Bora wa kiume Afrika ya Mashariki zilizotolewa jijini Nairobi, Kenya Mwezi Machi, 2023. Tuzo hizi ni ishara wazi kuwa TBC ina watumishi wenye weledi na ubunifu unaokonga hadhira katika tasnia ya habari ndani na nje ya nchi.

## Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

101. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilikadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 16,506,945,000 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya matangazo, nakala za magazeti, uchapaji kibiashara, kodi za pango, ushauri katika tasnia ya Habari na majukwaa ya kibiashara. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Kampuni imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 11,537,746,491.14 sawa na asilimia 70 ya lengo.

102. Mheshimiwa Spika, Katika kuendeleza, kukuza, kuimarisha na kuanzisha biashara mpya, Kampuni imekuwa ikichukua hatua mahsusi ikiwepo kuingia makubaliano ya maelewano (MoU) pamoja na mikataba na makampuni na Taasisi zingine. Makubaliano na mikataba hii ina malengo ya kupanua wigo wa biashara wa kampuni ili kuongeza vyanzo vya mapato na kuiwezesha kumudu gharama za uendeshaji. Jumla ya mikataba saba ilisainiwa na MoU nne zilijadiliwa na kuafikiwa kwa ajili utekelezaji.

103. Mheshimiwa Spika, Kampuni imeendelea na uchapaji wa kibiashara kwa kutumia mtambo wake mdogo wa kidijitali na pia kwa kutumia wachapaji binafsi (outsourcing) pale ilipopata kazi kubwa za uchapaji ambazo zilihitaji mashine kubwa. Moja ya kazi kubwa kwa kipindi hiki ilikuwa ni machapisho ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika tarehe 23 Agosti, 2022. Kazi nyingine ni pamoja na zile

za Mahakama, Wizara ya Kilimo, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Mamlaka ya Bandari Tanzania ambazo kwa pamoja zimewesha Kampuni kuingiza zaidi ya Shilingi bilioni 5. Kazi za uchapaji kwa ujumla zimeonyesha matumaini makubwa ya mapato kutokana na mwitikio chanya wa wateja.

104. Mheshimiwa Spika, kupitia magazeti ya Daily News, HabariLEO na Habari Mtandao *(Daily News Digital),* Kampuni iliendelea kutekeleza Mpango wake mahususi - "Editorial Transformational Plan' kwa kuandika habari za kina za uchambuzi zenye sauti za Mamlaka pamoja na Wananchi. Iliongeza sauti za wananchi/wanufaika wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikiali hasa katika maeneo ya mafanikio, faida na matarajio. Aidha, iliongeza pia sauti za wachambuzi na wataalamu kuelezea umuhimu wa Miradi, Sera na Mipango inayotekelezwa na Serikali. Vilevile, ubunifu katika utengenezaji wa kurasa zake kwa kuwa na 'infographics' na takwimu ili kutoa tafsiri halisi kwa habari zake, hii ikiwa ni pamoja kuweka mkazo kwenye habari zenye takwimu na majawabu kwa changamoto za wananchi kwa kuhusisha mamlaka, wachambuzi na wataalamu katika Sekta zote.

105. Mheshimiwa Spika, kufuatia maboresho ya tovuti za habari za TSN, watu takriban milioni 19 wametembelea tovuti za TSN katika kipindi hiki ikilinganishwa na watu milioni 12.4 waliotembelea tovuti hizo kati ya Januari na Juni, 2022. Vilevile, katika majukwaa ya mtandaoni, idadi ya watu walioona na kusoma habari ilifikia milioni 380 kufikia mwezi Aprili, 2023 kutoka watu milioni 324.3 mwezi Juni, 2022. Katika kipindi hiki, Kampuni imeanza utaratibu wa kuchapisha habari za kina mtandaoni *(Exclusive In-depth Reports)* zinazoandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza ambazo huambatana na picha kadhaa na sauti ya mtu anaesoma habari yenyewe.

Kwa utaratibu huu, msomaji hana haja ya kusoma bali anaweza kubonyeza kitufe na akaweza kusikia habari yote ikisomwa. Wasomaji wanaweza kuendelea na shughuli nyingine huku wakiendelea kupata habari kwa njia ya sauti. Vilevile, TSN imeanza kufanya vipindi vya mahojiano ya moja kwa moja na viongozi wa Serikali ili kuongeza nafasi ya viongozi kuzungumza na wananchi na pia kupata mrejesho kutoka kwa wananchi. Vipindi hivi vinarushwa kupitia majukwaa ya mtandaoni na pia kuchapishwa katika magazeti ya Daily News na HabariLEO.

106. Mheshimiwa Spika, TSN pia ilihabarisha umma kupitia matoleo maalumu yaliyoandaliwa kutokana na ziara za Kitaifa/ Kimataifa za Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar

Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, kumbukumbu ya Miaka 23 ya Kifo cha Baba wa Taifa, Mwl. Julius Nyerere, Miaka 61 ya Uhuru, miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mikutano ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na la Baraza la Wawakilishi.

### Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

107. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, UCSAF ilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi 34,760,583,156 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni Ruzuku toka Serikalini, Tozo ya huduma, ruzuku toka TCRA na fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo. Kufikia tarehe 30 Aprili, 2023, UCSAF ilifanikiwa kukusanya Shilingi 31,127,404,082 sawa na asilimia 89.5 ya makadirio ya mwaka.

### Miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano ya simu vijijini

108. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2022/23, UCSAF iliendelea na mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano kwa kujenga minara katika kata 364 zenye vijiji 715 na wakazi 4,062,237. Mpaka kufikia tarehe 30 Aprili, 2023, ujenzi wa minara katika Kata 295 zenye vijiji 616 ulikamilika na wakazi 3,368,738 wanapata huduma za mawasiliano. Aidha, ujenzi wa minara katika Kata 69 zilizobaki unaendelea ambapo watoa huduma wako katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajia kufikia mwezi Juni, 2023 utakamilika.

### Mradi wa Kupeleka Huduma za Mawasiliano Zanzibar

109. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia UCSAF iliendelea kutekeleza mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo 42 Zanzibar. Kupitia mradi huu minara 42 imejengwa katika Shehia 38 zilizoko Pemba na Unguja na kukamilika na kuzinduliwa tarehe 26 Oktoba, 2022 na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hivyo kufanya eneo lote la Zanzibar kuwa na mawasiliano ya simu..

### Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Minara ya Simu

110. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza matumizi ya intaneti nchini kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025, Serikali kupitia UCSAF imeendelea kutekeleza mradi wa kuiongezea uwezo (upgrade) minara 227 iliyokua katika teknolojia ya 2G pekee ili iweze kutoa pia huduma ya intaneti kwa kiwango cha 3G na 4G. Minara 176 imekwisha ongezewa nguvu na minara 51 iliyobaki utekelezaji wake unaendelea ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

### Mradi wa Kupeleka Vifaa Vya TEHAMA Mashuleni

111. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF iliendelea kutekeleza mradi wa kupeleka vifaa vya TEHAMA katika shule za umma 150 kwa ajili ya kukuza matumizi ya TEHAMA katika shule hizo. Katika utekelezaji wa mradi huu kila shule itapata Kompyuta 5, Printa moja na Projekta moja. Mpaka kufikia tarehe 30 Aprili, 2023, Serikali kupitia UCSAF imekamilisha manunuzi ya awamu ya kwanza ya kompyuta 650 kati ya kompyuta 950 pamoja na Projekta. Aidha ununuzi wa Printer 150 umekamilika na zinatarajiwa kupokelewa kutoka kwa wazabuni mwishoni mwa mwezi Mei, 2023. Kwa upande wa ununuzi wa Komputya 300 zilizobaki mzabuni amepatikana na anatarajiwa kukabidhi kompyuta hizo UCSAF ifikapo mwishoni mwa mwezi Mei, 2023 na baadae kukabidhiwa katika shule zilizokusudiwa.

112. **Mheshimiwa Spika,** UCSAF imeendelea kutekeleza mradi wa kupeleka vifaa vya TEHAMA vya kujifunzia kwa shule za watoto wenye mahitaji maalum. Kupitia mradi huu shule nane zitapewa vifaa vya TEHAMA kulingana na mahitaji yao. Shule hizo zitakazonufaika ni pamoja na Shule ya Sekondari ya Mpwapwa (Mpwapwa-Dodoma), Sekondari ya Mkolani (Mwanza), Sekondari ya Kashaulili (Mpanda-Katavi), Sekondari ya Morogoro (Morogoro), Sekondari ya Shinyanga (Kishapu-Shinyanga), Sekondari ya Wavulana Songea (Songea), Sekondari ya Kazima (Tabora) na Sekondari ya Haile Selassie (Mjini Magharibi). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 vifaa husika vilikwishapokelewa tayari kukabidhiwa shule hizo.

113. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imetekeleza mradi Kutoa vifaa 250 vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha huduma za Posta. Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Posta Tanzania (TPC). Hadi sasa, Serikali imetangaza zabuni ya kuleta vifaa vya TEHAMA (250 barcode scanners) na vifaa husika vitawasili mwezi Mei, 2023.

### Mradi wa Kuboresha Huduma za Utangazaji Katika Mikoa Saba

114. **Mheshimiwa Spika,** UCSAF ilipanga kuboresha huduma za utangazaji hususani kwa redio jamii zilizopo katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa kuanzia UCSAF imeanza utekelezaji wa mradi huu katika maeneo saba. Lengo la mradi huu ni kuzisaidia redio jamii zilizopo katika Halmashauri zetu kuweza kuongeza usikivu ili Watanzania waliopo katika maeneo hayo waweze kupata habari za kijamii na kiuchumi kwa wakati. Utekelezaji wa mradi umeshaanza. Maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni Halmshauri ya Wilaya ya Kasulu, Kondoa, Mbulu, Same, Kilindi, Rufiji na Mtama.

### Miradi ya Kuboresha Usikivu wa Redio ya Taifa TBC

115. Mheshimiwa Spika, Kutokana na changamoto iliyokuwepo ya usikivu wa Redio ya Taifa (TBC) kwa baadhi ya maeneo nchini hususani maeneo ya mipakani mwa nchi, UCSAF kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) imeanza mradi wa kujenga na kuboresha miundombinu ya kurushia matangazo na studio za redio ya Taifa ili kuongeza ubora wa matangazo. Maeneo ambayo miradi imekamilika ni pamoja Ngorongoro Mkoani Arusha na Mlele Mkoani Katavi. Aidha, ujenzi unaendelea katika vituo vya Kyela Mkoani Mbeya, Makete Mkoani Njombe, Mbinga Mkoani Ruvuma, Uvinza Mkoani Kigoma, Lushoto Mkoani Tanga pamoja na Kyerwa mkoani Kagera.

### Mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu

116. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Serikali kupitia UCSAF imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa jumla ya Walimu 635 katika vituo vya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST). Kati ya walimu 635 walimu 576 walitoka Tanzania Bara na walimu 59 walitoka Zanzibar. Lengo la mradi huu wa mafunzo ya TEHAMA ni kuwajengea uwezo Waalimu kuhusu matumizi ya Teknolojia ili wawe na ufahamu na uelewa katika taaluma ya TEHAMA ili waweze kufundisha wanafunzi. Katika mafunzo hayo ya TEHAMA Waalimu hupata fursa ya kujifunza matumizi ya vifaa hivi vya TEHAMA ikiwa ni pamoja na namna ya kuvifanyia matengenezo ya msingi vifaa vya TEHAMA yaani "Basic troubleshooting skills" vinapopata hitilafu ndogo ndogo.

### Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha TEHAMA Zanzibar

117. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia UCSAF ilikamilisha ujenzi wa kituo kimoja cha TEHAMA katika eneo la Fumba, Mkoa wa Mjini Magharibi Wilaya ya Mjini, ambapo ujenzi wa kituo ulikamilika na kuzinduliwa tarehe 26 Oktoba, 2022 na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kukamilika kwa kituo hiki kumefanya Wilaya zote 11 zilizopo Pemba na Unguja kila moja kuwa na kituo cha TEHAMA. Vituo hivi vinasaidia kutoa mafunzo ya TEHAMA na huduma za intaneti kwa wananchi.

### Mradi wa mawasiliano kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

118. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma za mawasiliano, Serikali imetenga fedha kiasi cha Dola za Marekani Milioni 30 kwa ajili ya kupeleka huduma za mawasiliano katika maeneo 763 pamoja na kuongeza nguvu za minara kutoka

teknolojia ya 2G hadi kuwa na teknolojia ya 3G/4G. Mpaka kufikia tarehe 30 Aprili, 2023, yafuatayo yamefanyika:- zabuni ilitangazwa tarehe 24 Oktoba, 2022 na kurejeshwa tarehe 31 Januari, 2023 kufuatiwa na tathmini, Idhini ya Benki ya Dunia kutolewa ambapo mpaka sasa jumla ya minara 758 itajengwa kupitia mradi huu wa Tanzania ya Kidijitali. Aidha, sehemu ya kwanza ya mradi huo ambayo ni kuiongezea nguvu minara 488 ili kutoa huduma kwa kiwango cha 2G/3G/4G zabuni ilitangazwa wiki ya mwisho ya mwezi Agosti, 2022 ambapo taarifa ya tathmini ilishawasilishwa Benki ya Dunia na idhini ya kuendelea na utekelezaji wa mradi kutolewa kwa ujenzi wa minara 304.

## Uanzishwaji wa Vituo vya Wazi vya Intaneti

119. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia UCSAF iliendelea kutekeleza mradi wa kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo sita ya wazi ili kuongeza na kuhamasisha matumizi ya mtandao wa intaneti nchini. Maeneo yaliyoainishwa na kufaidika na mradi huu ni pamoja na Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Lungemba (Mafinga), eneo la Nyerere Square (Dodoma), Ndaki ya Habari na Elimu Angavu (CIVE, Chuo Kikuu cha Dodoma), Soko la Tabora (Tabora), Kiembesamaki (Unguja) na Soko la Buhongwa (Mwanza). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023, mradi umekwisha kukamilika katika vituo vyote 6 na kuanza kutoa huduma.

## Mradi wa Tiba Mtandao (Telemedicine)

120. **Mheshimiwa Spika,** UCSAF inatekeleza mradi wa Tiba Mtandao. Ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za Serikali kuziunganisha hospitali za Mikoa kwenye mfumo wa tiba na Hospitali Taifa ya Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI). Serikali imepanga kuziunganisha Hospitali za Rufaa za Mnazi Mmoja iliyopo Unguja na Hospitali ya Rufaa ya Abdalla Mzee iliyopo Pemba. Mkataba na mkandarasi wa Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) umeshatiwa saini na manunuzi ya vifaa vya TEHAMA yamekamilika. Vifaa vya TEHAMA vimeshafungwa katika hosipitali hizo mbili na kuunganishwa kwenye mfumo wa Tiba Mtandao. Kwa sasa wataalamu wanaendelea na kuunganisha mfumo wa kusafirisha picha (PACS) pamoja na kuunganisha machine za X-ray.

## Tume ya TEHAMA (ICTC)

121. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya TEHAMA ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 5,468,105,000 zikiwa ni mgao kutoka Serikalini na makusanyo kutoka vyanzo vya Tume. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Tume ilifanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 1,854,358,184.61 sawa na asilimia 35 ya makadirio ya mwaka.

122. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza ubunifu katika TEHAMA nchini, Tume imeendelea na uratibu wa programu ya kukuza kampuni changa za TEHAMA (ICT Startups) ili kuwezesha bidhaa za TEHAMA kuingia katika soko na kuchangia katika kukuza uchumi na kutengeneza ajira kwa vijana. Tume imewezesha kampuni changa tisa kuanza kutoa huduma na kampuni hizo ziko katika hatua ya mwisho ya ukuzaji ili ziweze kuingia sokoni. Kampuni hizo ni Scancode (ina mfumo wa kutambua uhalali wa bidhaa kupitia bar code endapo ni halali au imeghushiwa), Kimbweta, Seto, TSSFL, Seluu, Angaza Directory, Niajiri, Ngasmake na Soshub. Aidha, mkutano wa kisekta wa mjadala kuhusu ubunifu katika utengenezaji wa Sera ya Bunifu za TEHAMA (Innovative Policy Making Dialogue) umefanyika ambapo wadau 106 walishiriki mjadala huu.

123. **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza TEHAMA nchini, Tume imewezesha wabunifu na wadau wa bidhaa za TEHAMA kuonyesha bidhaa zao katika Kongamano la mwaka la TEHAMA lililofanyika Zanzibar mwezi Oktoba, 2022. Kongamano hili lilishirikisha wawekezaji na wadau wa TEHAMA kutoka ndani na nje ya nchi wapatao 1,200 ikilinganishwa na wadau 800 walioshiriki katika Kongamano la mwezi Agosti, 2021 lililofanyika Jijini Arusha. Ongezeko hili linadhihirisha kuwa matumizi na uwekezaji katika TEHAMA ni mkubwa na unachangia kukuza uchumi kwa kasi. Kampuni 12 za wabunifu wa TEHAMA zilipata Tuzo ya mwaka ya TEHAMA katika kongamano hili. Kampuni na wabunifu hao ni Mapindi, Midtec Engineering Company, Atlas, Silabu, Seto, Niajiri, Agripoa, Mzinga Mtandaoni, Hack IT, Bizzyn, Smart Girls na Lyfplus. Kampuni hizi zitasaidiwa kupata mikopo isiyo na riba ili ili kukuza bidhaa zao.

124. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Kongamano la TEHAMA, Tume imeingia makubaliano ya uwezeshaji katika TEHAMA na mashirika na taasisi mbalimbali za ndani na nje kama ifuatavyo:-

i) Tume ya TEHAMA na CRDB wameingia makubaliano ya kuendeleza Wabunifu wa Kampuni ndogondogo za TEHAMA kupitia programu ya Imbeju, ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 5 imetolewa kama mtaji wa uwezeshaji kampuni changa za TEHAMA kwa mwaka 2023 na kiasi hiki kitakuwa kinatolewa kila mwaka;

i) Tume ya TEHAMA na CRDB wameingia makubaliano ya kuendeleza Wabunifu wa Kampuni ndogondogo za TEHAMA kupitia programu ya Imbeju, ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 5 imetolewa kama mtaji wa uwezeshaji kampuni changa za TEHAMA kwa mwaka 2023 na kiasi hiki kitakuwa kinatolewa kila mwaka;

ii) Tume ya TEHAMA na UNCDF imeingia makubaliano ya utekelezaji wa Mwongozo wa wabunifu katika TEHAMA (ICT Regulatory Sandbox Framework);

iii) Tume ya TEHAMA na UNDP zimeingia makubaliano ya kuibua na kuendeleza kampuni changa za TEHAMA ( ICT Startups);

iv) Tume ya TEHAMA kwa kushirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali ya Digital Opportunity Trust - DOT zimeingia makubaliano katika kuwezesha vijana kushiriki katika fursa zitokanazo na maendeleo ya kidijitali;

v) Serikali ya Tanzania kupitia Tume ya TEHAMA imefanya mashirikiano na nchi ya Estonia katika suala la Tafiti na utafiti utafanyika ili kuandaa "Digital Transformation Road Map" inayolenga kuongeza mchango wa sekta binafsi katika uchumi wa kidijitali;

vi) Tume ya TEHAMA na UNESCO zimesaini mkataba wa ushirikiano kwenye kufanya utafiti unaotathmini maendeleo ya intaneti Tanzania; na

vii) Tume ya TEHAMA na Aron Group yenye makao makuu nchini Korea Kusini zimesaini mkataba wa ushirikiano wa uendelezaji wa ubunifu TEHAMA katika huduma za kifedha (ICT Startup – payment solutions).

125. Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kusajili Wataalam wa TEHAMA nchini kwa lengo la kuwatambua na kuwaendeleza. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 wataalam wapya wa TEHAMA 554 walisajiliwa ikilinganishwa na wataalam 546 waliokuwa wamesajiliwa kwa kipindi kama hiki katika mwaka wa fedha 2021/22. Idadi ya usajili imeongezeka kwa asilimia 1.5. Hadi sasa idadi ya wataalam wa TEHAMA waliosajiliwa nchini ni 1,515. Tume ya TEHAMA inaendelea kufanya uchambuzi ikiwemo kukusanya maoni ya wadau na wataalamu wa TEHAMA nchini kuona uwezekano wa Serikali kuweka utaratibu wa kisheria utakaohamasisha zaidi wataalamu wa TEHAMA kujisajili pamoja na kuongeza ufanisi wa usajili na uendelezaji wa wataalamu wa TEHAMA nchini. Hatua hii inalenga kuiwezesha Tanzania kuwa na wataalamu wa kuaminika, wenye weledi na utaalamu unaokidhi mahitaji ya uchumi wa kidijitali.

126. Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kuratibu mafunzo ya utaalam wa TEHAMA kwenye maeneo yenye uhitaji kulingana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda na ongezeko la uhitaji wa matumizi ya Teknolojia kwenye uchumi wa Tanzania. Kwa kipindi kinachoishia Mwezi Aprili, 2023, wataalam 16 walishiriki mafunzo yaliyotolewa katika maeneo ya Big Data Analytics and Cybersecurity Specialist Maeneo yanayopewa vipaumbele katika mpango ujao wa mafunzo ni: Artificial Intelligence, Big Data Analy tics, Cybersecurity , Cryptography, Cloud Computing, Blockchain, Computer Forensics, Software Development, Mobile Application Development, Robotics, pamoja na ICT Project Management. Aidha, Tume ya TEHAMA imekuwa ikishirikiana na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kuhakikisha mitaala mipya ya TEHAMA au ile inayohuishwa inajumuisha maeneo ya kitaalamu ya kipaumbele na yenye uhitaji mkubwa katika soko la uchumi wa kidijitali ndani na nje ya nchi.

127. Mheshimiwa Spika, Tume ya TEHAMA kwa kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu vya Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Kilimo Cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) imesaini Hati ya Makubaliano na Chuo cha Turku (UTU) kilichopo Finland kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Uhimilivu (Resilience Academy) hapa nchini. Kituo hiki kitasaidia katika kujenga uwezo na kuongeza ujuzi katika masuala ya TEHAMA hususani sekta ya elimu, tafiti, uendelezaji wa miji, mazingira na uhifadhi wa takwimu za TEHAMA.

## Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Tanzania (TCRA CCC)

128. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kufanya mashauriano na wadau ikiwemo Serikali, Mamlaka ya Mawasiliano na Watoa huduma. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Baraza limepokea kiasi cha Shilingi 710,000,000 sawa na asilimia 100 ya tengeo la bajeti la Shilingi milioni 710 toka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Chanzo kikuu cha fedha za uendeshaji wa Baraza ni tengeo la bajeti kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

129. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kuanzisha Kamati za Watumiaji na kushauriana nazo. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 Baraza limeanzisha Kamati za Watumiaji katika Mikoa ya Simiyu, Ruvuma na Pwani na kufanya Kamati zilizoanzishwa hadi mwezi Aprili, 2023 kuweza kufikia 18. Baraza limeendelea kushauriana na Kamati za watumiaji katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Kigoma, Tabora, Rukwa Iringa, Mwanza,

Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharibi, Dodoma na Kusini Pemba. Aidha, Baraza limeendelea kuzijengea uwezo Kamati za Watumiaji kutekeleza majukumu ya kutoa elimu, kuhamasisha na kupokea maoni ya watumiaji kwa lengo la kupunguza changamoto za watumiaji na kuboresha huduma za mawasiliano.




130. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kupokea na kusambaza taarifa muhimu zinazohusu masuala ya watumiaji kupitia mikutano na wawakilishi wa watumiaji kutoka makundi ya watu wenye mahitaji maalum, wajasiriamali, wanawake, vijana, viongozi wa dini, Serikali za Mitaa na Waandishi wa Habari katika Mikoa tisa ambayo ni Simiyu, Pwani, Ruvuma, Dar es Salaam, Mjini Magharibi - Zanzibar, Lindi, Tabora, Mbeya na Dodoma.

131. Mheshimiwa Spika, Baraza kupitia vyombo vya habari ikiwemo; redio, magazeti, blogu, runinga, tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii limeendelea kutoa elimu, kuhamasisha na kupokea maoni kutoka kwa watumiaji. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Baraza limeendesha vipindi 13 kupitia redio na runinga kwa lengo la kuelimisha, kuhamasisha na kuhabarisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu fursa mbalimbali zilizo katika sekta na njia bora ya kutumia huduma za mawasiliano. Aidha, Mfumo wa e-mrejesho umetumika kupokea maoni ikiwa ni pamoja na changamoto za watumiaji pamoja na kutoa mrejesho kwa watumiaji. Kurasa za Mitandao ya kijamii ya Facebook, Instagram na Twitter zimehuishwa kwa kuwekwa taarifa mbalimbali za kuelimisha na kuhamasisha na kufikia watumiaji takriban 5,568,023. Aidha, Baraza linaendelea kukamilisha utengenezaji wa Programu Tumizi (Mobile application) itakayowasaidia watumiaji kujua na kuhakiki taarifa za matumizi ya data na kuwasilisha malalamiko endapo hawataridhika na taarifa za matumizi yao.


Cyber Security

# MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

# D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

## Makadirio ya Mapato ya Wizara

132. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inakadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 150,700,000,000 ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, tozo itokanayo na kuongeza salio la simu, usajili wa Magazeti, ada ya mwaka ya Magazeti, vitambulisho vya Waandishi wa Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida.

# Malengo Ya Bajeti Ya Wizara Ya Habari, Mawasiliano Na Teknolojia Ya Habari

133. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inasimamia Mapinduzi ya Kidijitali yanayowezeshwa na TEHAMA na pia kuimarisha mfumo wa kupashana habari kwa kusimamia uhuru wa vyombo vya habari nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka Msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA.

Ili kuwezesha mageuzi na mapinduzi haya kwenye Sekta zote za Uchumi na Kijamii, Wizara imepanga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye Sekta ili kuendana na mageuzi kwa kuharakisha uendelezaji na usimamiaji miundombinu ya TEHAMA, Mawasiliano, Posta na Habari. Baadhi ya miundombinu hiyo ni Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, anwani za makazi, mitambo ya utangazaji kwa lengo la kuchochea mfumo mpya wa uendeshaji wa uchumi wa kidijitali. Vilevile, kufanya mapinduzi kwenye Taasisi za Sekta; kuimarisha mashirikiano na Sekta binafsi, kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA, kuwajengea uwezo watumishi kuendana na mapinduzi haya, kuwezesha Sekta nyingine kuelekea kwenye mapinduzi ya kidijitali na kuweka mazingira ya kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari. Aidha, Wizara imekusudia kufanya mageuzi kwenye taasisi zake ili ziweze kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi. Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ili kuharakisha mapinduzi ya kidijitali na kuboresha mazingira ya wanahabari na vyombo vya habari katika maeneo yafuatayo:

## Eneo la Habari – MAELEZO

134. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kufanya mapitio ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 ili kuifanya iendane na mabadiliko katika Sekta ya Habari;

(ii) Kuendelea kutekeleza Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2017.

(iii) Kuratibu utungaji wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC);

(iv) Kuanzisha redio ya Afrika itakayotangaza kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuhimiza matumizi ya Kiswahili na kujenga umoja wa Afrika;

(v) ukusanya na kusambaza habari ikiwemo kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Programu na Miradi inazotekeleza;

(vi) Kuanzisha vyombo vilivyotajwa katika Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ambavyo ni Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari;

(vii) Kuchapa nakala 12,794 za Picha za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakala 12,794 za Picha za Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere, nakala 4,000 za Jarida la Nchi Yetu na nakala 2,000 za Bango la Baraza la Mawaziri (Cabinet posters);

(viii) Kuchapa na kutoa leseni 50 za magazeti na vitambulisho 1,000 vya Waandishi wa Habari nchini;

(ix) Kutoa miongozo ya mfumo bora wa taasisi za Serikali kutoa taarifa kwa umma na kufanya tathmini ya utendaji wa kila taasisi katika kutoa Taarifa kwa Umma;

(x) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 kuhakikisha maadili na uzingatiwaji wa Sheria katika Tasnia ya Habari;

(xi) Kuratibu mkutano wa mwaka wa Maafisa Mawasiliano Serikalini;

(xii) Kuratibu Vyombo vya habari katika matukio mbalimbali ya kitaifa na ziara za viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(xiii) Kuhamasisha Vyombo vya Habari vya nje katika kuitangaza Tanzania kwa kuandaa Makala fupi zenye kuonesha shughuli mbalimbali za maendeleo nchini;

(xiv) Kuanza Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano (National Communication Strategy-NCS);

(xv) Kuboresha Vipindi Maalum vya Ongea na Waziri;

(xvi) Kujenga Studio maalum kwa ajili ya vipindi vya moja kwa moja vya Redio na Televisheni;

(xvii) Kuratibu Kongamano la Pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari ambalo litajadili maendeleo ya Sekta ya Habari na kuweka mikakati ya namna ya kusukuma maendeleo ya nchi; na

(xviii) Kuratibu na kuandaa Siku ya Uhuru wa vyombo vya Habari Duniani, Siku ya Redio Duniani na Siku ya Haki ya Kupata Taarifa kwa kushirikiana na wadau. Maadhimisho haya huipa nafasi Serikali na wadau wa ndani na nje ya nchi kushauriana na kuweka mikakati ya kuhakikisha Uhuru wa Vyombo vya Habari na haki ya kupata taarifa sahihi vinaboreshwa.

## Eneo la Mawasiliano

135. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

(i) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997 na Sera ya Posta ya mwaka 2003;

(ii) Kuratibu uimarishaji wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya Simu na posta kote nchini;

(iii) Kuanzisha utaratibu mahsusi wa kugawa masafa kwa ajili ya Redio za Utangazaji za Kidijitali (Digital Sound Broadcasting)

(iv) Kutekeleza Mkakati wa Kuimarisha Ushiriki wa Tanzania Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Mawasiliano ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa makubaliano na mikataba ya kimataifa katika Sekta ya Mawasiliano, pia kushiriki na kutoa michango kuwezesha maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano Duniani;

(v) Kuratibu utungwaji wa Sheria ya kuimarisha matumizi na kuhakikisha uendelevu wa Mfumo wa Anwani za Makazi;

(vi) Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa Anwani za Makazi kwa kuhakiki taarifa zilizokusanywa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi pamoja na kuongeza matumizi ya mfumo huo kwa taasisi za Serikali na Sekta Binafsi;

(vii) Kuratibu uanzishaji wa shughuli za Anga la Juu nchini ikiwemo kufanya maandalizi ya kurusha setelite katika kuwezesha urahisi na unafuu katika upatikanaji wa huduma za mawasiliano nchini na huduma nyingine;

(viii) Kuandaa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano (Sector Investment Profile);

(ix) Kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Huduma Pamoja nchini kuongeza ufanisi katika upatikanaji na utoaji wa huduma za Serikali kwa Serikali, wananchi na wadau wengine kwa wakati na kwa gharama nafuu;

(x) Kusimamia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watoa huduma za mawasiliano ya simu na Posta; na

(xi) Kusimamia utekelezaji wa matokeo ya upembuzi yakinifu utakaowezesha biashara Mtandao (e-Commerce).

## Eneo la Uendelezaji wa Mifumo na Huduma za TEHAMA

136. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuendelea na uratibu wa kutungwa kwa Sheria ya TEHAMA;

(ii) Kuendelea kuboresha Usimamizi na uanzishwaji wa Kampuni Changa za TEHAMA kwa kuboresha mazingira ya kisera, Kisheria na Kikanuni na kuweka miongozo stahiki;

(iii) Kuratibu na kuwezesha matumizi ya Mfumo wa Mikutano ya Video (video conference) kwa ngazi ya Wizara, Mikoa 26 na Halmashauri 185 nchini;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Program);

(v) Kusimamia uanzishwaji wa Vyuo viwili vya TEHAMA vya Nala na Kigoma ikiwa ni pamoja na uundaji wa mitaala na muundo wa utawala na kazi za Taasisi hizo;

(vi) Kuwaendeleza wataalam wa TEHAMA 20 kwenye programu za muda mrefu kwa ngazi ya uzamilli na wataalam 200 kwenye mafunzo ya muda mfupi kwenye maeneo yenye uhaba;

(vii) Kufanya mapitio ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016;

(viii) Kuratibu na kuandaa Mikutano miwili ya Kitaifa na Mikutano miwili ya Kimataifa ya TEHAMA;

(ix) Kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na taasisi binafsi ili kutumia bunifu za kidijitali zilizopo kwa ajili ya kuleta maendeleo katika sekta nyingine za kiuchumi;

(x) Kufanya tathmini ya uanzishwaji wa 'smart cities' katika Mikoa ya Dodoma, Arusha na Mbeya;

(xi) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali;

(xii) Kujenga mfumo wa takwimu wa kielektroniki kwa ajili ya taarifa za TEHAMA;

(xiii) Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwenye masuala ya TEHAMA;

(xiv) Kuendelea na uratibu wa uendelezaji wa Mifumo ya Kitaifa nchini; na

(xv) Kuandaa Mkakati wa kuboresha matumizi ya Tafiti za TEHAMA nchini.

## Eneo la Miundombinu ya TEHAMA

137. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Ukamilishaji wa shughuli za ujenzi wa Kilometa 1742 za Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(ii) Kujenga Mikongo ya kuunganisha watumiaji ambao ni taasisi 50 kwenye maeneo ya uwekezaji, vituo vya afya na elimu ili kuharakisha Taifa kushiriki katika uchumi wa kidijitali;

(iii) Kuandaa Mpango wa Kitaifa wa maendeleo ya miundombinu ya TEHAMA (National ICT Infrastructure Development Plan);

(iv) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Brodibandi wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy);

(v) Kuratibu ujenzi wa Kilometa mpya 1,600 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma ya Mkongo kwenye Wilaya nyingine 14;

(vi) Kuratibu utekelezaji wa mradi wa miundombinu ya mawasiliano ya simu, redio na televisheni vijijini;
(vii) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa Miundombinu ya mtandao wenye kasi (broadband);

(viii) Kuratibu mafunzo kwa watumishi 72 wanaohusika na usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA; na

(ix) Kuandaa mwongozo wa ujenzi na mfumo wa usimamizi wa miundombinu ya kitaifa ya TEHAMA.

## Eneo la Usalama Mtandao

138. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuwezesha uanzishwaji wa Ofisi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

(ii) Kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Usalama Mtandaoni (2018 - 2023) na kuandaa na kutekeleza Mkakati mpya wa Usalama Mtandao (2023 - 2028);

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Elimu kwa Umma kuhusu Usalama Mtandao (2021/22 - 2025/26);

(iv) Kusimamia ukamilishwaji na utekelezaji wa usimamizi wa Miundombinu Muhimu ya TEHAMA (Critical ICT Infrastructures - CII);

(v) Kuimarisha muundo wa kiutawala na kiusimamizi wa ulinzi dhidi ya uhalifu wa mtandao nchini;

(vi) Kuandaa sera, miongozo na taratibu za kumlinda mtoto mtandaoni dhidi ya ukatili na uhalifu wa mtandao (Child Online Protection);

(vii) Kuimarisha uwezo wa wakaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa mifumo (Information Security Auditing capabilities);

(viii) Kufanya mapitio ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya usalama mtandao ili kuandaa Taifa kuwa katika mazingira mazuri ya Uchumi wa Kidijitali;

(ix) Kufanya tathmini na usanifu wa ujenzi wa mifumo ya kiusalama (security surveillance system) kwa malengo ya kuanzishwa 'smart cities' kwa kuweka katika miji ya Dodoma, Arusha na Mbeya;

(x) Kuratibu programu za kuwajengea uwezo wataalam wa Serikali ndani na nje ya nchi katika masuala ya usalama mtandao kwa kushirikiana na wadau; na

(xi) Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na vyombo vya Usalama.



# MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA

# MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA

139. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha Serikali inaharakisha kuwa na Jamii yenye habari sahihi na iliyowezeshwa Kidigitali kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii, Wizara inakusudia kutekeleza miradi tisa ikiwa na dhima ya Kuwezesha utoaji wa huduma za uhakika na za gharama nafuu za Habari, Teknolojia ya Habari, Mawasiliano ya simu na Posta kwa kuweka mazingira yanayokuza ubunifu katika kuibadilisha Tanzania kuwa na Uchumi wa Kidigitali, miradi hiyo ni:



## I. Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

140. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara imekadiria kutumia Shilingi 80,000,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Fedha hizi zitatumika kukamilisha ujenzi wa Kilomita 1,600 za Mkongo na Vituo vipya 15 vya kutolea huduma za Mkongo ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi ngazi za Wilaya nchini. Shughuli nyingine zitakazotekelezwa kwenye Mradi huu ni:

(i) Ujenzi wa Mikongo ya Mwisho (last mile connectivity) kwenye taasisi 50 za Kimkakati;

(ii) Ujenzi wa mkongo kupitia Ziwa Tanganyika kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo kiasi cha Kilomita 60;

(iii) Kuanza ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Zanzibar na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Data Dodoma;

(iv) Kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama;

(v) Kuelimisha umma kuhusu Mkakati wa Usalama Mtandaoni; na

(vi) Kukamilisha maandalizi ya Kanuni na kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022.

## II: Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu

141. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umelenga kuboresha na kuimarisha uwezo wa watalaam ndani ya Wizara katika matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, kutoa elimu kwa wananchi kutambua Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na matumizi ya TEHAMA pamoja na matumizi sahihi na salama ya TEHAMA yanayozingatia Sheria, Taratibu na Kanuni.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Shilingi 4,500,000,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendeleza watalaam wa Sekta na wa nje ya Sekta kwa kutoa mafunzo ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya TEHAMA na matumizi ya teknolojia mpya zinazoibukia kwenye sekta nyinginezo;

(ii) Kuwajengea uwezo waandishi wa Habari na Wahariri wa Vyombo vya Habari; iii) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi; na

(iv) Kuelimisha umma juu ya teknolojia mpya za kidijitali, kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi salama na yenye tija ya TEHAMA huku wakilinda haki za watoto, wanawake, makundi maalum na vijana.

### III: Mfumo wa Anwani za Makazi

142. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara imekadiria kutumia Shilingi 24,000,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Shughuli zitakazotekelezwa ni:

(i) Kuhakiki taarifa zilizokusanywa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi katika Halmashauri 80 na kuratibu uwekaji wa miundombinu ya Anwani za Makazi kwa kutumia fedha za ndani na za nje katika Mradi wa Tanzania ya Kidijitali;

(ii) Kuratibu uunganishaji wa mifumo ya taasisi nyingine kwenye mfumo wa NaPA na kuhimiza matumizi ya taarifa za mfumo huu ili kuharakisha utoaji huduma na kuongeza mapato ya Serikali;

(iii) Kuboresha programu tumizi ya NaPA kulingana na mahitaji ya watumiaji

(iv) Kuanza taratibu za kutungda sheria Mahsusi ya Anwani za Makazi ambayo itasimamia na kuongoza shughuli zote za utekelezaji wa Mfumo nchini;

(v) Kujenga uelewa kuhusu namna ya kusimamia, kuendeleza na kutumia mfumo wa anwani za makazi;

(vi) Kuratibu matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi ya taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi;

(vii) Kuratibu uanzishwaji wa maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao; na

(viii) Kuboresha Sera ya Posta ya Mwaka 2003.



## IV: Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA

143. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kuimarisha na kuendeleza ujuzi kwa wabunifu katika masuala ya TEHAMA nchini kwa lengo la kukuza vipaji na kuongeza wigo wa vijana kujiajiri katika shughuli mbalimbali za TEHAMA.
Kwa mwaka 2023/24 Shilingi 8,477,440,000 fedha za ndani zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kusimamia ujenzi wa Kituo cha Kitaifa cha Kuendeleza Watalaam, Tafiti na Ubunifu wa TEHAMA jijini Dodoma na Chuo cha TEHAMA Kigoma;

(ii) Kuanzisha vituo atamizi vya TEHAMA katika vyuo vikuu vya umma na maeneo maalum ya kiuchumi kote nchini; na

(iii) Kujenga uwezo kwa wataalam 40 watakaosimamia programu za anga za juu.



## V: Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Project)

144. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unalenga kuleta mabadiliko ya Kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya Kijiditali ya Kikanda na Kimataifa na hatimaye kukuza Uchumi wa Kidijitali. Matokeo ya mradi huu ni pamoja na kuongeza na kubuni ajira zitakazotokana na ubunifu wa TEHAMA, ukuzaji wa viwanda vidogo vidogo (SMEs na SMMEs); kukuza ustadi wa wataalamu wa ndani ya Serikali na waliopo nje ya Serikali; na kuongeza uwezo wa utoaji wa Huduma za Serikali kwa kuwezesha uwepo wa intaneti bora ya bei nafuu na ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya Serikali ili kumnufaisha mwananchi.

145. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 35,176,500,000 ikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuanzishwa kwa Taasisi ya TEHAMA na vituo vya Ubunifu wa TEHAMA;

(ii) Kuanzishwa kwa vituo vitano vya kanda vya kusaidia kukuza Taaluma ya TEHAMA;

(iii) Utengenezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (NISMIS);

(iii) Utengenezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (NISMIS);

(iv) Kuunganisha Taasisi za Serikali kwenye mtandao mmoja (GoVNET);

(v) Usimikaji wa vituo vya Huduma Pamoja nchini;

(vi) Kujenga maabara tatu kwa ajili ya kufufua vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza;

(vii) Kuboresha uwezo na Mifumo ya Vituo vya kuhifadhia Data nchini;

(viii) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa Tanzania ya kidijitali;

(ix) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu matumizi bora ya teknolojia mpya za kidijitali; na

(x) Kujenga uwezo kwa wataalam wa TEHAMA 500 Serikalini.

## VI: Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA

146. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara inakadiria kutumia Shilingi 3,300,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Ujenzi wa vituo vitatu vya Kanda vya watengenezaji wa bidhaa za TEHAMA;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa kituo cha kuwezesha uanzishwaji wa kampuni changa za TEHAMA (ICT startups) cha Dar es Salaam (Soft center);

(iii) Kuendelea na programu ya mafunzo ya kuendeleza wataalam wa TEHAMA waliosajiliwa;

(iv) Kutengeneza mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu wa TEHAMA; na

(v) Kufanya tafiti za TEHAMA ili kuiwezesha nchi kupiga hatua katika matumizi ya teknolojia mpya za kidijitali katika mazingira ya Kitanzania.

## VII: Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

147. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) unalenga kuboresha upanuzi wa usikivu wa Shirika nchi nzima. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara inakadiria kutumia Shilingi 15,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuendelea kujenga na kufunga miundombinu ya utangazaji katika Wilaya tisa kati ya Wilaya 21 ambazo hazina usikivu au usikivu wake ni hafifu;

(ii) Kununua gari moja ya kurushia matangazo mubashara (Televisheni) kwa ajili shughuli za utangazaji;

(iii) Kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya TBC Jijini Dodoma pamoja na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA; na

(iv) Ununuzi wa mitambo na vifaa vya utangazaji wa redio, Televisheni na Mitandao ya kijamii kuunganisha studio tano za Mikocheni, Zanzibar, Barabara ya Nyerere, Dodoma na Arusha.


TBC SIKONGE -TABORA


TBC KISAKI - MOROGORO


TBC NKASI - RUKWA


TBC KASULU - KIGOMA


TBC KARAGWE - KAGERA


TBC BUNDA - MARA

## VIII: Mradi wa Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji

148. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kuwezesha Kampuni ya Magazeti Tanzania (TSN) kufunga mtambo mpya wa kisasa wa uchapaji. Katika mwaka wa fedha 2023/24 kiasi cha Shilingi 10,000,000,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha uchapaji;

(ii) Kukamilisha ufungaji wa mitambo ya kisasa ya uchapaji; na

(iii) Ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari kwa ajili ya kuongeza uzalishaji.

## IX: Mradi wa Habari kwa Umma

149. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kukusanya, kuchakata, kuandaa na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo Sera, Sheria, Mikakati, Programu na Miradi zinazotekelezwa na Serikali. Vilevile, mradi unakusanya taarifa za mrejesho kutoka kwa wananchi kwa lengo la kupata maoni ya wananchi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Shilingi 1,500,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuandaa makala maalumu, kukusanya na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kupitia vipindi maalum katika televisheni na redio, makala katika magazeti pamoja na mitandao ya kijamii kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa programu na miradi ya Serikali;

(ii) Ununuzi wa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya ukusanyaji, uchakataji na uandaaji wa taarifa vikiwemo magari, kamera na visaidizi vyake na vifaa vya Kurushia Matangazo Mubashara; na

(iii) Kuanzisha mchakato wa ujenzi wa Kituo cha Habari (Press Centre) ambacho kitajumuisha Chaneli ya Televisheni ya Serikali, studio kwa ajli ya kuzalisha maudhui, vyumba vya mikutano, eneo maalum litakalotumiwa na waandishi wa habari kufanya kazi pamoja na mifumo ya kufuatilia habari zinazotokea duniani

# MIPANGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA NA WIZARA

150. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zimekadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 535,007,705,050.62 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Mchanganuo wa makusanyo na shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:

## Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

151. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inakadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 221,167,037,333.62 ambazo zitatokana na ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrabaha (asilimia 1 ya pato ghafi ya watoa huduma za mawasiliano), ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya mawasiliano, ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA na makusanyo yatokanayo na mtambo wa TTMS.

152. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuimarisha upimaji na kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano ili kutoa huduma za udhibiti kwa usahihi zaidi;

ii) Kudhibiti ulaghai katika mitandao ya mawasiliano ili kuhakikisha upatikanaji wa mapato ya Serikali kutoka kwenye miamala ya simu za kutoka nje ya nchi (International Incoming traffic);

iii) Kuimarisha ukaguzi wa ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinatolewa kwa mujibu wa sheria, kanuni na kwa kuzingatia masharti ya leseni;

iv) Kuimarisha usimamizi wa Mfumo wa utoaji leseni na rasilimali za mawasiliano;

v) Kutoa elimu kwa watumiaji na wadau wengine wa huduma za mawasiliano ili kuongeza uelewa juu ya haki na wajibu wao;

vi) Utekelezaji wa Miundombinu ya Kitaifa ya Mawasiliano ya Mtandao wa Umma (NPKI) ili kuhakikisha usalama wa miamala ya kieletroniki nchini;

vii) Kujenga Maabara ya kukagua na kuhakiki viwango vya vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki nchini;

viii) Kuendelea kuboresha na kuimarisha Mifumo ya ndani ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

ix) Kufuatilia, kujibu na kuripoti matukio ya usalama wa kimtandao ili kupunguza mashambulizi;

x) Kuendelea kuboresha Kanzidata ya usajili wa wateja (Know Your Customer Database) ili kuwa na taarifa kamili na sahihi za wateja kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za udhibiti;

xi) Kuendelea kuwapa wafanyakazi wa TCRA mafunzo endelevu ili kukuza uwezo wao kwa utekelezaji wa kazi za udhibiti;

xii) Kukamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi na kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya TCRA - Dodoma na Zanzibar;

xiii) Kuhamasisha uanzishwaji wa Vikundi vya Kidijitali (Digital Clubs) Mashuleni na Vyuoni kwa ajili ya kujenga uwezo wa nchi yetu kushiriki kikamilifu kwenye uchumi wa kidijiti; na

xiv) Kuendelea kushirikiana na taasisi za kikanda na kimataifa zinazosimamia Mawasiliano. Taasisi hizi ni pamoja na EACO, CRASA, ATU, CTO, PAPU, UPU, na ITU.

## Shirika la Posta Tanzania (TPC)

153. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Shirika la Posta Tanzania linatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 39,476,613,000 kutokana na biashara za Usafirishaji wa Barua kwa njia ya kawaida, Usafirishaji wa Barua kwa njia haraka (EMS), Fedha na Uwakala, Biashara ya kubadilisha fedha za kigeni (Bureau de Change), Miliki na Biashara Mtandao.

154. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Shirika la Posta Tanzania limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

i) Kujenga kituo cha kikanda kitakachojumuisha maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao;

ii) Kuimarisha utoaji wa huduma za Posta kidijitali kwa;

(a) Kusimika na kuendesha masanduku matatu ya kielektroniki ya vifurushi (parcel e-Lockers) Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma;

(b) Kusimika na kuendesha mashine tatu za Virtual Teller Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma;

(c) Kuanzisha vituo 15 vya kukusanya na kusambaza mizigo, vifurushi na vipeto (Nyegezi - Mwanza; Jamuhuri -

Dodoma; Uyole- Mbeya; Gungu -Kigoma; Ipogoro - Iringa; Ngangamfumuni - Moshi; Sumbawanga - Rukwa; Sanawari - Arusha; Jangwani, Kariakoo, Temeke, Libya, Tegeta, Kigamboni na Mbezi - Dar es Salaam) na masanduku ya kupokea vifurushi katika Wizara na Ofisi Maalum 36;

(d) Kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa huduma za kifedha (Posta cash e-wallet) kupitia ufadhili wa Umoja wa Posta Duniani;

(e) Kuimarisha mifumo na miundombinu ya TEHAMA ikiwemo mfumo wa Posta Kiganjani, kutengeneza mfumo wa utoaji wa taarifa, mfumo wa huduma kwa wateja, mfumo wa kudhibiti majanga ya kimtandao na mfumo wa ukaguzi;

iii) Kuwezesha na kusimamia utoaji wa huduma za Serikali kupitia vituo vya Huduma Pamoja kwa kutumia mtandao wa ofisi za Posta zilizoenea nchi nzima kwa kuanza na vituo 10 vya Huduma Pamoja vinavyoanzishwa kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali na kuendelea nchi nzima;

iv) Kutekeleza Muundo wa Shirika ulioidhinishwa kwa kuwa na uboreshaji endelevu wa hali ya kazi, mipango ya ustawi wa wafanyakazi na kuimarisha ufanisi katika utendaji. Hili litaambatana na;

(a) Kuanzisha na kuhudumia mikoa mipya sita ya posta ya Katavi, Manyara, Songwe, Njombe, Bariadi (Simiyu) na Pwani;

(b) Kuanzisha Jengo la Utawala na kituo cha kutolea huduma za Posta katika Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma;

(c) Kuimarisha utoaji wa programu muhimu za mafunzo kwa wafanyakazi; na

(d) Kuboresha huduma kwa kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Ubora wa huduma.

v) Kushirikisha wadau wa Sekta binafsi katika uwekezaji na utoaji wa huduma bora ili kuongeza tija na ufanisi katika huduma za usafirishaji wa nyaraka, barua, vifurushi, vipeto na mizigo kwa njia ya kawaida na haraka ndani na nje ya nchi, huduma za fedha na uwakala na biashara mtandao.

## Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

155. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 204,952,454,212 kutokana na huduma za Shirika ambazo ni simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

156. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Shirika la

Mawasiliano Tanzania limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuendeleza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kuufikisha katika Wilaya na Halmashauri Mpya nyingine 30;

(i) Kuunganisha huduma za faiba (Broadband) kupitiana kauli mbiu ni 'Fiber Mlangoni Kwako' ambapo makazi 20,000 yenye takriban ya watumiaji 200,000 yatafikiwa;

(iii) Kuwezesha maeneo 50 muhimu ya umma katika miji yote mikuu na Wi-Fi ya umma

(iv) Kufungua kampuni tanzu za huduma za mawasiliano katika nchi jirani

(v) Kuboresha huduma kwa lengo la kuongeza Mauzo;

(vi) Kufanyika kwa utafiti wa huduma za Shirika na kuridhika kwa wateja;

(vii) Kutekeleza mpango wa kila mwaka wa mafunzo ya ukuzaji uwezo kwa watumishi wa Shirika;

(viii) Kujenga Mfumo wa utoaji huduma za kuhifadhi data kielektroniki (Data e-Services Platform) itakayowezesha jamii na taasisi za kibiashara zaidi ya 2,000,000 kunufaika na huduma za uhifadhi data kimtandao kwa gharama nafuu;

(ix) Shirika limepanga kutoa huduma ya N-card kwa jumla ya watu 3,271,828 Kupitia kituo cha data center;

(x) Kusajili wateja 500,000 wapya wa T-PESA kwa ajili ya kutumia huduma za Kifedha za T-PESA;

(xi) Kuunganisha watoa huduma wa kibiashara kielektroniki kupitia (mini-apps) kwenye APP ya T-PESA ili kuwasogezea wateja wetu huduma zilizopo kwenye mfumo mmoja wa Super App; na

(xii) Kuunganisha Taasisi tano za Serikali na Binafsi kwa ajili ya huduma za malipo ya mkupuo (Bulk Disbursement).

### Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)

157. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Shirika la Utangazaji Tanzania linakadiria kutumia Jumla ya Shilingi 46,860,319,000 ambapo Shilingi 16,968,980,000 ni makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani ambavyo ni matangazo ya biashara, udhamini wa vipindi na matangazo mubashara kupitia vyombo vyake vya redio, runinga na mitandao ya kijamii. Aidha, TBC imetengewa kiasi cha Shilingi 29,891,339,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida.

158. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Shirika la Utangazaji Tanzania limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Upanuzi wa Usikivu redio za TBC katika Wilaya saba nchini: Kongwa (Dodoma), Mpwapwa

(Dodoma), Kilolo (Iringa), Hanang' (Manyara), Ulanga (Morogoro), Iramba (Singida) na Pangani (Tanga);

(ii) Kuendelea kukarabati jengo la ofisi, ununuzi wa mitambo na vifaa vya utangazaji vya chaneli ya Tanzania Safari;

(iii) Ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya TBC jijini Dodoma;

(iv) Kununua vifaa na mifumo kwa ajili ya kuimarisha muonekano wa Televisheni kwa kuongeza ung'aavu wa picha (improvement of Television Channels Outlook);

(v) Ununuzi na ufungaji wa mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring);

(vi) Ujenzi na ukarabati wa majengo na Ofisi za TBC Dar es salaam kwenye Kanda nane;

(vii) Ununuzi wa magari tisa ya shughuli za utangazaji;

(viii) Ununuzi wa gari maalum moja la kurushia matangazo mubashara- televisheni;

(ix) Ununuzi wa vifaa vya kurushia matangazo mubashara ya redio nje ya studio kwenye Kanda nane;

(x) Ununuzi wa mitambo na vifaa vya kurushia matangazo mbashara ya Televisheni (TBC1, TBC2 na Ofisi za Kanda);

(xi) Ukarabati wa studio za redio (Awamu ya tatu), uhifadhi, uhamishaji na uboreshaji wa studio za Ukombozi kwa ajili ya Makumbusho ya maktaba ya TV (picha jongefu) na (Sauti) na ufungaji wa mitambo kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu;

(xii) Ununuzi na ufungaji wa mitambo, vifaa na mifumo mitatu ya TEHAMA kwa ajili ya shughuli za utangazaji nchini; na

(xiii) Ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya TBC Mtandaoni na televisheni mtandao ya Kiingereza.

### Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

159. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/24 Kampuni ya Magazeti ya Serikali imepanga kuzalisha na kukusanya kiasi cha Shilingi 17,332,292,250 kutokana na mauzo ya bidhaa na huduma zake za asili ikiwa ni ongezeko la asilimia 5 kutoka bajeti ya mwaka 2022/23.

160. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Magazeti ya Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika Mwaka wa Fedha 2023/24:

(i) Kuboresha ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa madeni kwa kuwashirikisha na kuwawezesha wakusanyaji wa

ndani na nje ili kuongeza ukwasi wa Kampuni kwa asilimia 10;

(ii) Kujenga kiwanda cha uchapaji jijini DSM na kusimika mitambo mipya ya uchapaji kibiashara ili kuweza kuongeza mauzo ya magazeti na machapisho mengine;

(iii) Kuongeza wauzaji/mawakala wa magazeti katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kilimanjaro, Tanga na Mbeya;

(iv) Kuongeza Idadi ya wasomaji wakubwa waliojisajili mtandaoni na wanunuzi wakubwa wa gazeti mtandao hadi kufikia 200;

(v) Kufanya majukwaa ya kutangaza fursa za biashara na uwekezaji nchini.

(vi) Kuongeza mauzo ya matangazo kwa angalau asilimia 5 au zaidi;

(vii) Kutoa huduma za ushauri kwenye Tasnia ya Habari kwa wateja wasiopungua nane;

(viii) Kukuza mauzo ya bidhaa na huduma zote kwa kuhudhuria hafla za Serikali na Taasisi za umma na kutoa ufahamu wa bidhaa na huduma za TSN kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

(ix) Kuanzisha studio ya kisasa (Multimedia Digital Studio) jijini Dar es Salaam;

(x) Kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi vikiwemo vyombo vingine vya habari, Balozi na Taasisi za Kimataifa na kutia saini Mikataba ya Makubaliano (MoU) isiyopungua minne; na

(xi) Kuongeza ubora wa bidhaa na huduma za kihabari zinazotolewa na Kampuni kwa kurudisha uchapaji wa magazeti wenye tija na kuongeza maudhui ya ndani kufikia asilimia 80 ya maudhui yote.

## Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

161. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) unatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 35,102,688,605 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni Tozo ya huduma na tengeo toka TCRA.

162. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendelea kutekeleza mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano kwa kujenga minara 758 katika kata 7163 kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali;

(ii) Kuboresha Huduma za matangazo ya TBC Redio katika maeneo matatu ya mipakani;

(iii) Kuboresha Redio Jamii katika Halmashauri moja;

(iv) Kuboresha upatikanaji wa matangazo ya redio katika mikoa minne;

(v) Kuiongezea nguvu minara 100 kutoka 2G kwenda 2G/3G na 4G;

(vi) Kutoa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za kiposta;

(vii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi katika minara 438;

(viii) Kuratibu maadhimisho ya siku ya Wasichana na TEHAMA;

(ix) Kufanya tathmini ya kusimika na kuunganisha Maabara za Kompyuta kwa shule zote za Sekondari nchini;

(x) Kupeleka vifaa vya TEHAMA katika shule 160;

(xi) Kutoa vifaa vya TEHAMA kwa watoto wenye mahitaji maalum katika shule 6;

(xii) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu 650;

(xiii) Kuunganisha Hospitali 5 na Tiba Mtandao;

(xv) Kufanya utafiti wa kuangalia pengo la Kidijitali nchini Tanzania; na

(xiv) Kufunga mtandao wa intaneti katika maeneo ya wazi 20.

## Tume ya TEHAMA (ICTC)

163. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/24, Tume ya TEHAMA inatarajia kutumia Jumla ya Shilingi 5,284,725,000 ambapo Shilingi 861,828,000 ni makusanyo ya ndani na Shilingi 4,422,897,000 kutoka Mfuko mkuu wa Serikali. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,984,725,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 3,300,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

164. **Mheshimiwa Spika,** ili kuharakisha mapinduzi ya kidijitali, Mwaka wa Fedha 2023/24 Tume ya TEHAMA imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kufanya tafiti za maendeleo ya TEHAMA nchini na kufanya tathmini ya kitaifa ya hatua za utekelezaji wa mikakati ya kuendeleza TEHAMA nchini;

(ii) Kuratibu na kuandaa matukio ya kuvutia uwekezaji na kutangaza masoko ya bidhaa za TEHAMA ndani na nje ya nchi;

(iii) Kushirikiana na washirika wa maendeleo na kampuni za kimataifa katika kuendeleza bunifu za TEHAMA ikiwemo kuwezesha utengenezaji wa bidhaa za TEHAMA hapa nchini;

(iv) Kuwezesha mafunzo maalum ya wataalam wa TEHAMA 500 ili kukuza na kuendeleza ujuzi wa TEHAMA nchini;

(v) Kukuza soko la bidhaa na huduma za kampuni ndogondogo "startups" kwa kushiriki maonyesho na makongamano

| 650 | Tabora | Sikonge | DTP PH1 | MIC |
| 651 | Tabora | Sikonge | PHASE 8 | Vodacom |

| MAENEO YANAYOTARAJIWA KUJENGWA MINARA YA MAWASILIANO KUPITIA MRADI WA TANZANIA YA KIDIJITALI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NA | MKOA | WILAYA | MRADI | OPERETA |
| 652 | Tabora | Sikonge | PHASE 8 | TTCL |
| 653 | Tabora | Sikonge | PHASE 8 | Airtel |
| 654 | Tabora | Sikonge | PHASE 8 | TTCL |
| 655 | Tabora | Sikonge | DTP PH1 | MIC |
| 656 | Tabora | Sikonge | PHASE 8 | TTCL |
| 657 | Tabora | Tabora Urban | DTP PH1 | MIC |
| 658 | Tabora | Tabora Urban | PHASE 8 | TTCL |
| 659 | Tabora | Tabora Urban | DTP PH1 | MIC |
| 660 | Tabora | Urambo | DTP PH1 | AIRTEL |
| 661 | Tabora | Urambo | DTP PH1 | AIRTEL |
| 662 | Tabora | Urambo | PHASE 8 | Halotel |
| 663 | Tabora | Uyui | DTP PH1 | AIRTEL |
| 664 | Tabora | Uyui | PHASE 8 | Halotel |
| 665 | Tabora | Uyui | PHASE 8 | TTCL |
| 666 | Tabora | Uyui | PHASE 8 | Airtel |
| 667 | Tabora | Uyui | DTP PH1 | AIRTEL |
| 668 | Tabora | Uyui | PHASE 8 | TTCL |
| 669 | Tabora | Uyui | PHASE 8 | TTCL |
| 670 | Tabora | Uyui | PHASE 8 | TTCL |
| 671 | Tabora | Uyui | PHASE 8 | TTCL |
| 672 | Tanga | Handeni | PHASE 8 | TTCL |
| 673 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 674 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 675 | Tanga | Handeni | PHASE 8 | Airtel |
| 676 | Tanga | Handeni | PHASE 8 | MIC |
| 677 | Tanga | Handeni | PHASE 8 | TTCL |
| 678 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 679 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 680 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 681 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 682 | Tanga | Handeni | PHASE 8 | Airtel |
| 683 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 684 | Tanga | Handeni | PHASE 8 | Airtel |
| 685 | Tanga | Handeni | DTP PH1 | MIC |
| 686 | Tanga | Kilindi | DTP PH1 | AIRTEL |
| 687 | Tanga | Kilindi | DTP PH1 | MIC |
| 688 | Tanga | Kilindi | DTP PH1 | AIRTEL |
| 689 | Tanga | Kilindi | PHASE 8 | Airtel |

| MAENEO YANAYOTARAJIWA KUJENGWA MINARA YA MAWASILIANO KUPITIA MRADI WA TANZANIA YA KIDIJITALI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| NA | MKOA | WILAYA | MRADI | OPERETA |
| 690 | Tanga | Kilindi | PHASE 8 | TTCL |
| 691 | Tanga | Kilindi | DTP PH1 | AIRTEL |
| 692 | Tanga | Kilindi | DTP PH1 | AIRTEL |
| 693 | Tanga | Korogwe | PHASE 8 | TTCL |
| 694 | Tanga | Korogwe | DTP PH1 | AIRTEL |
| 695 | Tanga | Lushoto | PHASE 8 | Airtel |
| 696 | Tanga | Lushoto | PHASE 8 | TTCL |
| 697 | Tanga | Lushoto | DTP PH1 | AIRTEL |
| 698 | Tanga | Lushoto | DTP PH1 | AIRTEL |
| 699 | Tanga | Mkinga | PHASE 8 | TTCL |
| 700 | Tanga | Mkinga | DTP PH1 | MIC |
| 701 | Tanga | Muheza | PHASE 8 | TTCL |
| 702 | Tanga | Muheza | PHASE 8 | TTCL |
| 703 | Tanga | Muheza | PHASE 8 | Vodacom |
| 704 | Tanga | Muheza | DTP PH1 | AIRTEL |
| 705 | Tanga | Muheza | DTP PH1 | AIRTEL |
| 706 | Tanga | Muheza | DTP PH1 | MIC |
| 707 | Tanga | Muheza | PHASE 8 | MIC |
| 708 | Tanga | Pangani | DTP PH1 | MIC |
| 709 | Tanga | Pangani | DTP PH1 | VODACOM |
| 710 | Tanga | Pangani | DTP PH1 | AIRTEL |
| 711 | Tanga | Pangani | DTP PH1 | AIRTEL |
| 712 | Tanga | Pangani | DTP PH1 | MIC |
| 713 | Tanga | Tanga M. | DTP PH1 | MIC |

# Kiambatisho Na.07

## VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA KWA WATEJA WA TTCL KWA NCHI NZIMA

| NA | MKOA | WILAYA | MAHALI | JINA LA DUKA | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Arusha | Boma Road | Arusha | 272545033/272544735 |
| 2 | Arusha | Meru | Duluti stand CDTI Road | Tengeru | 272553216 |
| 3 | Arusha | Meru | Moshi Arusha Road | Usariver | 272541070 |
| 4 | Arusha | Babati | Babati town-Dodoma Singida road | Babati | 272510048/272531028 |
| 5 | Arusha | Monduli | Monduli town | Monduli | 272538045 |
| 6 | Arusha | Karatu | Karatu town | Karatu | 272534577/272534004 |
| 7 | Arusha | Hanang | Katesh CCM Building | Katesh | 272531600 |
| 8 | Arusha | Mbulu | Bomani | Mbulu | 272533005 |
| 9 | Arusha | Kiteto | Kiteto | Kiteto | 272552094 |
| 10 | Coast | Kibaha | Maili Moja -Mkoani area | Kibaha | 023-2402200 |
| 11 | Coast | Kibaha | Jengo la NMB | Mlandizi | 0232935319/20 |
| 12 | Coast | Bagamoyo | Bagamoyo Town -Adjacent Post Office | Bagamoyo | 023-2440081 |
| 13 | Dar es Salaam | Ilala | Nyerere Road | Pugu Road | 022-2142662 |
| 14 | Dar es Salaam | Ilala | Uhuru Road | Ilala | 022 - 2203254 |
| 15 | Dar es Salaam | Ilala | Tabata Magengeni | Tabata | 022 - 2807401, 022 - 2807410 |
| 16 | Dar es Salaam | Ilala | Airport compound | Airport | 022-2844093 |
| 17 | Dar es Salaam | Ilala | Airport near JWTZ shop | Wageni | 022-2843800 |
| 18 | Dar es Salaam | Temeke | Kurasini Near Wapo Radio | Kurasini | 022-2850520 |
| 19 | Dar es Salaam | | | Mafia | 023-2440081 |
| 20 | Dar es Salaam | Rufiji | Behind- -Post Office | Ikwiriri | 023-2011016 |
| 21 | Dar es Salaam | Ilala | Extelecomms Building - Samora Avenue | Metro | 022 2142107 |

| NA | MKOA | WILAYA | MAHALI | JINA LA DUKA | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 22 | Dar es Salaam | Ilala | Upanga Exchange - Maliki road | Upanga | 022 2151424 |
| 23 | Dar es Salaam | Ilala | Mafia Str | Kariakoo | 022 2183220 |
| 24 | Dar es Salaam | Kinondoni | Watumishi House | Magomeni | 022 2928585/6 |
| 25 | Dar es Salaam | Kinondoni | Ali Hassan Mwinyi /Rose garden | Kijitonyama | 022-2144359/022-2144363 |
| 26 | Dar es Salaam | Kinondoni | Haile selasie Road Opposite Osyterbay Primary school. | Oysterbay | 022-2667668/2668898 |
| 27 | Dar es Salaam | Kinondoni | Tegeta - Kibo Complex | Kibo complex | 022-2926321/2 |
| 28 | Dar es Salaam | Kinondoni | Morogoro Road/Ubungo plaza | Ubungo | 022-2461150 |
| 29 | Dar es Salaam | Ubungo | UDSM -Changanyikeni Road Karibu na Jengo la Utawa la Chuo | UDSM | 022- 2410071 |
| 30 | Dar es Salaam | Ubungo | Mlimani city | Mlimani | 0222411026 / 0222411027 |
| 31 | Dar es Salaam | Ubungo | Classi Mall Tangi Bovu | Mbezi | 0222618442/2618443/4 |
| 32 | Dodoma | Dodoma Mjini | Railway Rd | Dodoma | 026 2324036 |
| 33 | Dodoma | Dodoma Mjini | Tembo Str | Nyerere Square | 026 2324411 |
| 34 | Dodoma | Dodoma Mjini | Kilimo kwanza - Capital Mall | Kisasa | |
| 35 | Dodoma | Kongwa | Posta | Kongwa | 026 2320413 |
| 36 | Dodoma | Mpwapwa | Posta | Mpwapwa | 026 2320787 |
| 37 | Dodoma | Kondoa | Posta | Kondoa | 026 2360046 |
| 38 | Iringa | Iringa | Telephone House | Iringa | 262702000/ 262702047 |
| 39 | Iringa | Mufindi | Post Office Mafinga | Mafinga | 262772221 |
| 40 | Iringa | Njombe | Ubena Makambako | Makambako | 262730055 |
| 41 | Iringa | Ludewa | Post Office Ludewa | Ludewa | 262790010 |
| 42 | Iringa | Njombe | Post Office | Njombe | 262782024 |
| 43 | Kagera | Bukoba | Uganda Rd | Bukoba | 028 2220600, 0767 200154 |
| 44 | Kagera | Muleba | Biharamulo Rd | Muleba | 028 2224066 , 0784 624660 |
| 45 | Kagera | Ngara | Posta Str | Ngara | 028 2226041, 0764 748477 |
| 46 | Kagera | Chato | Simu Str | Chato | 028 2982500, 0766 122561 |
| 47 | Kagera | Biharamulo | Karume Str | Biharamulo | 028 2225055, 0767 143112 |
| 48 | Kagera | Karagwe | Bomani | Kayanga | 028 2227204, 0787 356144 |
| 49 | Kigoma | Kigoma Urban | Kiezya Road | Kigoma CSC | 0282803599, 0282802600 |
| 50 | Kigoma | Kasulu District | Kigoma Road | Kasulu CSC | 0282810408, 0282810098/9 |

| NA | MKOA | WILAYA | MAHALI | JINA LA DUKA | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 51 | Kigoma | Kibondo District | UNCHR Road | Kibondo CSC | 0282820090, 0282820232 |
| 52 | Kilimanjaro | Moshi | Moshi/market street | Moshi | 027 2752106 |
| 53 | Kilimanjaro | Same | Same town | Same | 027 2720000 |
| 54 | Kilimanjaro | Mkuu | Mkuu wilayani | Rombo | 027 2790000 |
| 55 | Kilimanjaro | Hai | Boma ng'ombe | Hai | 027 2974378 |
| 56 | Kilimanjaro | Moshi Rural | Marangu Mtoni | Maragu | 027 2756537 |
| 57 | Kilimanjaro | Mwanga | Mwanga town | Mwanga | 027 2757673 |
| 58 | Lindi | Lindi | Baraza street Lindi. | Lindi | 232202720 |
| 59 | Lindi | Nachingwea | Posta street | Nachingwea | 232201045 |
| 60 | Lindi | Kilwa | Kivinje Road | Kilwa Masoko | 232013029 |
| 61 | Lindi | Masasi | Mkuti Sabasaba Street | Masasi | 023 2510122 |
| 62 | Mara | Bunda | Posta Rd | Bunda | 2621146 |
| 63 | Mara | Musoma | Majita Rd | Musoma | 2622827 |
| 64 | Mara | Tarime | Ngombe Rd | Tarime | 2690190 |
| 65 | Mara | Serengeti | Arusha Rd | Mugumu | 738262113 |
| 66 | Mbeya | Mbeya Mjini | Lupa Way | Mbeya | 252502000 |
| 67 | Mbeya | Rungwe | Bomani Area | Tukuyu | 252552000 |
| 68 | Mbeya | Kyela | Mbugani Area | Kyela | 252540033 |
| 69 | Mbeya | Mbarali | Ihanga Str | Rujewa | 252590000 |
| 70 | Mbeya | Mbozi | Vwawa Ichenzezya | Mbozi | 252580002 |
| 71 | Mbeya | Momba | Sikanyika Str | Tunduma | 252530074 |
| 72 | Mbeya | Ileje | Itumba Str | Ileje | 252570000 |
| 73 | Mbeya | Chunya | Kibaoni B Street | Chunya | 252520010 |
| 74 | Morogoro | Morogoro | Old dsm rd | Morogoro CSC | 232614310 |
| 75 | Morogoro | Kilombero | Kilosa rd | Ifakara | 232641000 |
| 76 | Morogoro | Kilombero | Ifakara rd | Kidatu | 232626069 |
| 77 | Morogoro | Kilosa | Green Area | Mikumi | 232620453 |
| 78 | Morogoro | Kilosa | Uhindini rd | Kilosa | 232623100 |
| 79 | Morogoro | Gairo | Dodoma rd,Unguu street | Gairo | 738262323 0232930000 |
| 80 | Mtwara | Mtwara | Shangani Tanu Rd Telephone House | Mtawara | 023 2333555/ 0232334329 0232333568/ |
| 81 | Mtwara | Newala | Majengo Boma Rd | Newala | 023 2410318 |
| 82 | Mwanza | Geita | Posta Street | Geita | 282520122 |
| 83 | Mwanza | Magu | Nyalikungu Street | Magu | 282530132 |
| 84 | Mwanza | Ukerewe | Posta Street | Nansio | 282515076 |

| NA | MKOA | WILAYA | MAHALI | JINA LA DUKA | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 85 | Mwanza | Sengerema | Ibisabageni Street | Sengerema | 282590092 |
| 86 | Mwanza | Nyamagana | Posta Road | Mwanza | 282501027 |
| 87 | Mwanza | Nyamagana | Buzuruga | Buzuruga | 282570571 |
| 88 | Mwanza | Kwimba | Nyambiti Road | Ngudu | 282983112 |
| 89 | Pemba | Chachake | Madungu Street | Chakechake | 242452323/242452057 |
| 90 | Pemba | Wete | Wete Posta | Wete | 242454680 |
| 91 | Rukwa | Sumbawanga | Bomani area | Sumbawanga csc | 252802255 |
| 92 | Rukwa | Mpanda | Buzogwe area | Mpanda csc | 252820115 |
| 93 | Rukwa | Nkasi | Nkomolo area | Namanyere csc | 252830074 |
| 94 | Ruvuma | Songea | Sokoine Road | Songea | 0252602808, 0252602322 |
| 95 | Ruvuma | Mbinga | Boma area | Mbinga | 252640034 |
| 96 | Ruvuma | Tunduru | Posta Building Boma road | Tunduru | 252680180 |
| 97 | Shinyanga | Shinyanga | Mwanza Rd | Shinyanga | 282762571 |
| 98 | Shinyanga | Kahama | Igalimi Str | Kahama | 282710138 |
| 99 | Shinyanga | Bariadi | Nyerere Rd | Bariadi | 282700100 |
| 100 | Shinyanga | Maswa | Uhuru Rd | Maswa | 282750365 |
| 101 | Shinyanga | Meatu | Mwanhuzi | Meatu | 282795099 / 0282795002 |
| 102 | Singida | Singida | Boma Road | Singida | 026 2502777 |
| 103 | Singida | Manyoni | Manyoni Town Centre | Manyoni | 026 2540039 |
| 104 | Singida | Iramba | Bomani | Iramba | 026 2533040 |
| 105 | Singida | Itigi | Itigi Town | Itigi | 026 2540177 |
| 106 | Tabora | Tabora | Jamhuri | Tabora | 262604738/262604555 |
| 107 | Tabora | Nzega | Nzega | Nzega | 262692140 FAX 262692150 |
| 108 | Tabora | Igunga | Igunga | Igunga | 262650034 FAX 262650000 |
| 109 | Tanga | Tanga | Independent road | Tanga | 272646464/0653699936 |
| 110 | Tanga | Korogwe | Manundu Moshi road | Korogwe | 272650088/0655362646 |
| 111 | Tanga | Muheza | Muheza town | Muheza | 272647311/0712783888 |
| 112 | Tanga | Lushoto | Lushoto town (Chake chake) | Lushoto | 272660057/0786261194 |
| 113 | Tanga | Handeni | Bomani | Handeni | 272977405/0764949967 |
| 114 | Tanga | Pangani | Kumba | Pangani | 272630042/0652764054 |
| 115 | Unguja | Mjini | Kijangwani | Kijangwani | 2222144702/10/39 |

Chanzo: Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation)

## Kiambatisho Na.08

# ORODHA YA OFISI ZA POSTA TANZANIA HADI MWEZI APRILI,2023

| MKOA | HPO | DPO /SDO | FRANCHISED PO | MDC | SUB PO |
|---|---|---|---|---|---|
| ARUSHA | Arusha | Babati<br>Karatu<br>Katesh<br>Kibaya<br>Loliondo<br>Mbulu<br>Meru<br>Namanga<br>Uhuru Rd<br>Usa River | A.I.C .C<br>Nelson Mandela<br>Hydom<br>Duluti<br>Monduli<br>Technical College | Ngaramtoni | Oldean<br>Longido |
| DAR ES SALAAM | Dar es Salaam<br>GPO<br>Mzizima | Sokoine Drive<br>Kijitonyama<br>Ilala<br>Msasani<br>Ubungo<br>Bagamoyo<br>Kariakoo<br>Mafia<br>Temeke<br>Tegeta<br>Kawe<br>Chang'ombe<br>Mwananyamala<br>Muhimbili<br>Kigamboni<br>Libya Street<br>Kibaha<br>Air Port<br>Mzizima<br>Mbagala | Kibiti<br>Mkuranga<br>Utete<br>Chalinze<br>Boko<br>Yombo Vituka | Buguruni<br>Mtoni Kijichi<br>Ubungo Kibangu<br>Mbagala<br>Zakhem<br>Mwenge<br>MbeziLuis<br>Biafra<br>Kipunguni<br>Kimara<br>Matangani<br>Kigogo CCM<br>Rombo Store<br>Segerea<br>Sinza<br>Tabata Kisukuru<br>Gongo la Mboto<br>-Mzambarauni<br>Ubungo External<br>Ubungo Darajani | |

| MKOA | HPO | DPO/SDO | FRANCHISED PO | MDC | SUB PO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kurasini<br>Pugu Road<br>Mlandizi<br>Upanga<br>Oyster Bay<br>University Hill<br>UCLAS<br>Ikwiriri<br>Kisarawe<br>Tabata CCM | | | |
| DODOMA | Dodoma HPO | Kondoa<br>Mpwapwa<br>Kongwa<br>St. John's<br>Bunge | Kibaigwa<br>Soko Kuu<br>Mvumi | | |
| IRINGA/NJOMBE | Iringa | Njombe<br>Mafinga<br>Makete<br>Ludewa<br>Makambako | Mazombe<br>Kilolo<br>Tosamaganga<br>Mufindi<br>Mgololo<br>Ilembula<br>Migoli<br>Kihesa | Ifunda<br>Malangali<br>Lupembe<br>Bulongwa | |
| KAGERA | Bukoba | Biharamulo<br>Chato<br>Kamachumu<br>Karagwe<br>Kyaka<br>Muleba<br>Ngara | Kanyigo<br>Rubya<br>Rulenge<br>Ntoma (delivery center) | | |
| KIGOMA | Kigoma | Kasulu<br>Kibondo | Manyovu<br>Nguruka<br>Uvinza | | Kalema |

| MKOA | HPO | DPO/SDO | FRANCHISED PO | MDC | SUB PO |
|---|---|---|---|---|---|
| KILIMANJAR O | Moshi | Marangu<br>Mkuu<br>Mwanga<br>Hai<br>S ame<br>Himo<br>S anya Juu<br>Usangi<br>Tarakea | Langasani<br>Ugweno<br>Hedaru<br>Maparara<br>Kil R oad<br>G onja<br>KIA<br>KC MC | | Mbaga Manka<br>Kisiwani<br>Makanya<br>S uji<br>Kihurio<br>Ndungu<br>Kibosho<br>Mango<br>Kirua Vunjo<br>O ld Moshi<br>Mwika<br>Uchira<br>Machame<br>Mamba<br>Myamba<br>Useri<br>Kahe |
| LINDI | Lindi | K/Masoko<br>Nachingwea | Liwale<br>R uangwa | | |
| MAR A | Musoma | Bunda<br>Mugumu<br>Tarime | | Kibara<br>Butiama<br>S hirati | |
| MBE YA/S O NG WE | Mbeya | Tukuyu<br>Kyela<br>C hunya<br>R ujewa<br>C himala<br>Mbozi<br>Tunduma<br>Ileje | Mkwajuni<br>S ongwe<br>Mbalizi<br>Iyunga<br>Uyole<br>Mwakaleli<br>Mzumbe | | Isoko<br>Makongorosi<br>Mlowo<br>Igurusi<br>MUS T<br>(Mbeya<br>University of<br>S cience&<br>Tech |

| MKOA | HPO | DPO/SDO | FRANCHISED PO | MDC | SUB PO |
|---|---|---|---|---|---|
| MOROGORO | Morogoro | Ifakara<br>Kilosa<br>Kidatu<br>Chuo Kikuu (SUA)<br>Mzumbe<br>Mahenge<br>Madaraka<br>Mlimba | Mikumi<br>Mawenzi<br>Turiani<br>Mtibwa<br>Mang'ula<br>Malinyi<br>Ngerengere<br>Dumila<br>Kimamba | Kihonda<br>Gairo | Msowero<br>Kingolwira<br>Kidugalo<br>Dakawa |
| MTWARA | Mtwara | Masasi<br>Newala<br>Ndanda | Tandahimba<br>Kitangali<br>Mikindani | | |
| MWANZA/GEITA | Mwanza | Pamba Rd<br>Geita<br>Sengerema<br>Magu<br>Nansio<br>Ngudu<br>Misungwi<br>Bugando<br>Nyegezi<br>Kirumba | Nyakato | | Igoma |
| RUKWA/KATAVI | Sumbawanga | Mpanda<br>Namanyere | Laela | | |
| RUVUMA | Songea | Mbinga<br>Tunduru | Madaba<br>Namtumbo<br>Peramiho<br>Mbambabay | | Liuli |
| SHINYANGA/<br>SIMIYU | Shinyanga | Kahama<br>Maswa<br>Bariadi<br>Mwanhuzi | Isaka<br>Malampaka<br>Kishapu<br>Mwadui | Kolandoto | Lalago |
| | | Ushirombo<br>Bunungu<br>Masumbwe | | | |

| MKOA | HPO | DPO/SDO | FRANCHISED PO | MDC | SUB PO |
|---|---|---|---|---|---|
| TABO R A | Tabora | Nzega<br>Urambo<br>Igunga<br>S ikonge<br>Nkinga | Ndala<br>Kaliula<br>Bukene<br>Tumbi | | Ulyankulu<br>Bongomela<br>Kipalapala<br>Mabama<br>Usoke |
| S ING IDA | S ingida | Manyoni<br>Kiomboi | Kinampanda<br>Majengo<br>Itigi | | Mtinko<br>Ilongero<br>Iguguno<br>Nduguti<br>Mkalama |
| TANG A | Tanga | Korogwe<br>Lushoto<br>Muheza<br>Handeni<br>Pangani | Bumbuli<br>Amani<br>Mombo<br>S onge<br>S oni | | Kwalukonge<br>Kwamkono<br>Mgwasi |
| UNG UJA/ PE MBA | Kijangwani | C hakechake<br>Wete<br>S hangani | Mahonda<br>Makunduchi<br>Mkoani | Jambiani | Kengeja<br>Tunguu |
| | | | | | |

C ha : S hirika la Posta zania (TPC )

Ufunguo:

HPO = Head Post O ffice `

DPO = Departmental Post O ffice

S DO = S tamp Distribution O ffice

FPO = Franchised Post O ffice

S PO = S ub Post O ffice

MDC = Mail Delivery C entre

# Kiambatisho Na.09

TAKWIMU ZA MWENENDO WA USIKIVU WAREDIO ZA TBC(TBCTAIFA,TBC FM NA TBC-INTERNATIONAL)2015/16–2022/23.

| Na | Mkoa | Wilaya | Frequency | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2021/22 | 2022/23 | TBC FM | TBC TAIFA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Arumeru | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.7 |
| 2 | Arusha | Monduli | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.7 |
| 3 | Arusha | Longido | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 91.3 | 93.3 |
| 4 | Arusha | Karatu | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.7 |
| 5 | Arusha | Arusha Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.7 |
| 6 | Arusha | Arusha Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 7 | Arusha | Ngorongoro | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.7 | 89.7 |
| 8 | Dar es Salaam | Ilala | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 9 | Dar es Salaam | Kinondoni | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 10 | Dar es Salaam | Temeke | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 11 | Dar es Salaam | Kigamboni | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 12 | Dar es Salaam | Ubungo | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 13 | Dodoma | Bahi | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 14 | Dodoma | Chamwino | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 15 | Dodoma | Dodoma Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 16 | Dodoma | Kondoa | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 17 | Dodoma | Kongwa | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 18 | Dodoma | Mpwapwa | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 19 | Dodoma | Chemba | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 20 | Geita | Bukombe | FM | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 21 | Geita | Chato | FM | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 22 | Geita | Mbogwe | FM | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 23 | Geita | Nyang'whale | FM | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 24 | Geita | Geita Urban | FM | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 25 | Iringa | Iringa urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 26 | Iringa | Kilolo | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 27 | Kagera | Bukoba Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 28 | Kagera | Bukoba Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 29 | Kagera | Muleba | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 30 | Kagera | Kyerwa | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 31 | Kagera | Misenyi | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 32 | Kagera | Karagwe | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 33 | Kagera | Ngara | FM | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 34 | Kigoma | Kasulu Rural | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 89.9 | 87.9 |
| 35 | Kigoma | Kasulu Urban | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 89.9 | 87.9 |
| 36 | Kigoma | Kigoma Ujiji | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 37 | Kigoma | Uvinza | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 89.9 | 87.9 |
| 38 | Kigoma | Kigoma Vijijini | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 39 | Kigoma | Kakonko | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 98.9 | 96.9 |
| 40 | Kigoma | Kibondo | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 96.9 | 98.9 |
| 41 | Kigoma | Buhigwe | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 42 | Kilimanjaro | Hai | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90.0 | 87.9 |
| 43 | Kilimanjaro | Moshi Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90.0 | 87.9 |
| 44 | Kilimanjaro | Moshi Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90.0 | 87.9 |
| 45 | Kilimanjaro | Mwanga | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90.0 | 87.9 |
| 46 | Kilimanjaro | Rombo | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 87.9 | 90.0 |
| 47 | Kilimanjaro | Siha | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 87.9 | 90.0 |
| 48 | Kilimanjaro | Same | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.7 | 89.7 |
| 49 | Lindi | Lindi Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 50 | Lindi | Lindi Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 51 | Lindi | Ruangwa | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 52 | Lindi | Liwale | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 53 | Lindi | Nachingwea | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 54 | Lindi | Ruangwa | FM | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 87.9 | 89.9 |
| 55 | Manyara | Babati | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 56 | Manyara | Hanang | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 57 | Manyara | Mbulu | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 58 | Mara | Musoma Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 59 | Mara | Musoma Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 60 | Mara | Rorya | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 61 | Mara | Tarime | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 100.5 | 90.1 |
| 62 | Mara | Butiama | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 63 | Mara | Bunda | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 64 | Mbeya | Chunya | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 87.7 | 89.7 |
| 65 | Mbeya | Mbarali | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 87.7 | 89.7 |
| 66 | Mbeya | Mbeya Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 87.7 | 89.7 |
| 67 | Mbeya | Mbeya Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 87.7 | 89.7 |
| 68 | Mbeya | Mbozi | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 87.7 | 89.7 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 69 | Mbeya | Kyela | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 100.5 | 104.9 |
| 70 | Mbeya | Rungwe | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 100.5 | 104.9 |
| 71 | Morogoro | Morogoro Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 87.9 | 89.9 |
| 72 | Morogoro | Morogoro Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 87.9 | 89.9 |
| 73 | Morogoro | Mlimba | FM | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 87.9 | 89.9 |
| 74 | Morogoro | Gairo | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 75 | Morogoro | Kilosa | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 76 | Morogoro | Mvomero | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 77 | Mtwara | Masasi | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 105.9 | 87.7 |
| 78 | Mtwara | Newala | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 97.4 | 100.9 |
| 79 | Mtwara | Tandahimba | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 97.4 | 100.9 |
| 80 | Mtwara | Nanyumbu | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 81 | Mtwara | Mtwara Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 82 | Mtwara | Mtwara Urban | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 83 | Mwanza | Kwimba | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 84 | Mwanza | Ukerewe | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 85 | Mwanza | Ilemela | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 86 | Mwanza | Magu | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 87 | Mwanza | Misungwi | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 88 | Mwanza | Nyamagana | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 89 | Mwanza | Sengerema | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 90 | Njombe | Ludewa | FM | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 91 | Njombe | Makete | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 89.9 | 87.9 |
| 92 | Pwani | Kibaha | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 93 | Pwani | Kisarawe | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 94 | Pwani | Mkuranga | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 95 | Pwani | Bagamoyo | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.8 |
| 96 | Katavi | Mpanda | FM | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 97 | Katavi | Mlele | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 98 | Rukwa | Sumbawanga Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 99 | Rukwa | Nkasi | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 100 | Ruvuma | Songea Urban | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 101 | Ruvuma | Songea Rural | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 102 | Ruvuma | Nyasa | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 92.5 | 89.7 |
| 103 | Ruvuma | Namtumbo | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 90 | 87.7 |
| 104 | Ruvuma | Tunduru | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 105 | Ruvuma | Mbinga | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 106 | Simiyu | Busega | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 89.9 | 87.9 |
| 107 | Shinyanga | Shinyanga Urban | FM | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 108 | Shinyanga | Kahama | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.7 |
| 109 | Singida | Singida Mjini | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.5 | 87.7 |
| 110 | Singida | Singida Vijijini | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.5 | 87.7 |
| 111 | Tabora | Tabora Mjini | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 112 | Tabora | Nzega | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 113 | Tabora | Uyui | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 114 | Tabora | Sikonge | FM | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 87.9 | 89.9 |
| 115 | Tanga | Korogwe | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 116 | Tanga | Muheza | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 117 | Tanga | Pangani | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 118 | Tanga | Handeni | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 119 | Tanga | Kilindi | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| 120 | Tanga | Lushoto | FM | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 89.9 | 87.9 |
| 121 | Tanga | Tanga Mjini | FM | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 89.7 | 87.7 |
| | | | Jumla | 83 | 7 | 8 | 5 | 18 | | |
| | JUMLA | | | 83 | 7 | 8 | 5 | 18 | 121 | |

## Kiambatisho Na. 10

### WILAYA AMBAZO MIRADI YA MAENDELEO YA UPANUZI WA USIKIVU INAENDELEA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA(2021/22NA2022/23)

| Na | Mkoa | Wilaya | Na | Mkoa | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Simiyu | Bariadi | 12 | Kilimanjaro | Rombo DC |
| 2 | Simiyu | Itilima | 13 | Tanga | Mkinga |
| 3 | Simiyu | Maswa | 14 | Kigoma | Kakonko |
| 4 | Simiyu | Meatu | 15 | Pwani | Rufiji |
| 5 | Songwe | Mbozi | 16 | Pwani | Kibiti |
| 6 | Songwe | Songwe | 17 | Rukwa | Kalambo |
| 7 | Songwe | Momba | 18 | Tabora | Igunga |
| 8 | Songwe | Ileje | 19 | Tabora | Urambo |
| 9 | Njombe | Makambako | 20 | Tabora | Kaliua |
| 10 | Njombe | Waging'ombe | 21 | Singida | Manyoni |
| 11 | Njombe | Njombe mjini | 22 | Mbeya | Chunya |
| 12 | Njombe | Njombe Vijijini | 23 | Lindi | Liwale125 |

| Na | Mkoa | Wilaya | Na | Mkoa | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|
| 24 | Mara | Serengeti | 30 | Kagera | Kyerwa |
| 25 | Dodoma | Chemba | 31 | Iringa | Mufindi |
| 26 | Tanzania - Zanzibar | Unguja na Pemba | 32 | Lindi | Kilwa |
| 27 | Iringa | Mufundi | 33 | Manyara | Babati Vijijini |
| 28 | Shinyanga | Shinyanga Vijijini | 34 | Manyara | Kiteto |
| 29 | Arusha | Karatu | | | |

# Kiambatisho Na. 11

WILAYA AMBAZO MRADI WA UPANUZI WA USIKIVU UTATEKELEZWA MWAKA WA FEDHA(2023/2024)

| Na | Mkoa | Wilaya | Na | Mkoa | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dodoma | Kongwa | 6 | Manyara | Hanang' |
| 2 | Dodoma | Mpwapwa | 7 | Morogoro | Ulanga |
| 3 | Iringa | Kilolo | 8 | Singida | Iramba |
| 4 | Katavi | Tanganyika | 9 | Kilimanjaro | Siha |
| 5 | Morogoro | Gairo | | | |

# Kiambatisho Na. 12

WILAYA AMBAZO HAKUNA USIKIVU WA REDIO AU USIKIVU WAKE NI HAFIFU.

| Na | Mkoa | Wilaya | Na | Mkoa | Wilaya |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Iringa | Mafinga | 7 | Shinyanga | Kishapu |
| 2 | Morogoro | Malinyi | 8 | Tabora | Tabora Vijijini |
| 3 | Kagera | Biharamulo | 9 | Singida | Mkalama |
| 4 | Manyara | Simanjiro | 10 | Singida | Ikungi |
| 5 | Pwani | Mafia | 11 | Geita | Bukombe |
| 6 | Rukwa | Sumbawanga Vijijini | 12 | Tanga | Pangani |

## Kiambatisho Na.13

### USAJILI WA LAINI ZA SIMU KWA KILA MTOA HUDUMA HADI MWEZI APRILI, 2023




Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

## Kiambatisho Na.14

### Uwiano kwa Asilimia ya Laini za Simu Zilizosajiliwa kwa Mkoa kufikia Aprili 2023



## Kiambatisho Na.15

### MWENENDO WA SIMU ZA ULAGHAI KUANZIA JUNI 2013 MPAKA APRILI, 2023

*Chanzo: Mamlaka ya Mawasilaino Tanzania (TCRA)*



## Kiambatisho Na.16

### MWENENDO WA BEI ZA DATA NJE YA VIFURUSHI 2015- APRIL 2023




Chanzo: Mamlaka ya Mawasilaino Tanzania (TCRA)

## Kiambatisho Na.17

### MWENENDO WA ONGEZEKO LA MATUMIZI YA INTANETI NCHINI KUFIKIA APRILI, 2023




Chanzo: Mamlaka ya Mawasilaino Tanzania (TCRA)

# Kiambatisho Na.18

## HALI YA MAWASILIANO YA INTANETI NCHINI KUFIKIA MWEZI APRILI, 2023

| Na. | | | Aprili, 2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | IDADI YA WATU | | 61.7 Milioni |
| 2 | Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 2G kwa Idadi ya watu (2G Population Coverage) | 98% | 60.5 Milioni |
| 3 | Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 3G kwa Idadi ya watu (3G Population Coverage) | 74% | 45.7 Milioni |
| 4 | Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 4G kwa Idadi ya watu (4G Population Coverage) | 58% | 35.8 Milioni |
| 5 | Uwiano wa Mawasiliano ya simu kwa maeneo ya kijiografia (3G Geographical Coverage) | 59% | 557,601 $Km^2$ |
| 6 | Uwiano wa Mawasiliano ya simu kwa maeneo ya kijiografia (4G Geographical Coverage) | 40% | 38,7485 $Km^2$ |
| 7 | Asilimia ya Simu Janja (Smartphone Penetration) | 21% | 21 Milioni |




Wizara ya Habari, Mawasiliano
na Teknolojia ya Habari,
Mji wa Serikali Mtumba
9 Mtaa wa Mawasiliano,
S.L.P. 677,
40470 DODOMA.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Ahsante Mheshimiwa kwa kutoa taarifa kidigitali, na hii ndiyo mara ya kwanza tunaona bajeti inasomwa kwa dakika 25 tu. Haya ndiyo mambo tunayataka. Siyo mnaleta hesabu za kuku, hesabu za inzi sijui. Haya.

Wageni wengine ni watangazaji wa kipindi cha Dadaz Kituo cha *East African TV,* mpo? Ahsanteni. Mkurugenzi wa Mjini*FM,* Salam Sharaf au Mendez, karibu.

Mheshimiwa Shangazi Katibu wa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi anawatangazia Wabunge wote wa CCM kikao cha *Party Caucus* leo Ijumaa saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Wote mhudhurie.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itaendesha semina kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara pamoja na Sera ya Ubia ya Shirika la Nyumba Taifa *(NHC)*. Semina hiyo itafanyika siku ya Jumatatu tarehe 22 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge. wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hiyo muhimu ili kuwajengea uelewa kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara hiyo.

Sasa namwita Mwenyekiti. Karibu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Miundombinu.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambao unajumuisha maelezo ya jumla, muundo wa taarifa, pamoja na ufafanuzi wa namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake; Sehemu ya Pili ni uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024; sehemu ya tatu ni maoni na ushauri wa Kamati; na sehemu ya nne ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024; kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilichambua taarifa za utekelezaji za Fungu 68 - Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2). Katika ulinganisho huo, Kamati ilitathmini mwenendo wa

makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023. Katika hatua hii, Kamati ilifanya tathmini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, ufanisi wa utekelezaji wa miradi husika pamoja na tija ambayo inapatikana katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi uliofanyika kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati imezingatia masuala muhimu yanayogusa sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Masuala hayo ni pamoja na umuhimu wa Wizara kuhakikisha inachangia utekelezaji bora wa Ibara ya 18 ya Katiba ambayo pamoja na masuala mengine, inaweka haki ya kila mtu kutafuta, kupokea na kutoa habari; kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi kuhusu masuala muhimu ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Hali ya Upatikanaji wa Fedha; ili kutekeleza malengo waliyojiwekea, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya shilingi 282.05. Kati ya fedha hizo, shilingi 26.27 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 255.77 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2023 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi bilioni 89.86 sawa na asilimia 31.86 ya bajeti iliyodhinishiwa. Kwa wastani, hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara ilikuwa chini ya matarajio kwani hadi kufikia Februari, 2023, fedha iliyopokelewa ilikuwa ni wastani wa chini ya asilimia 32. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge

kutolewa kwa wakati kabla ya mwaka wa fedha 2022/2023 kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 255.7 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo. Wastani wa mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo ulikuwa chini ya matarajio kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2023 ni asilimia 30.15 ya fedha ilikuwa imepokelewa kutekeleza miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mapokezi hafifu ya fedha iliyotengwa, inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi na kufifisha manufaa yaliyotarajiwa kutokana na bajeti husika. Mathalani, wananchi hasa wa pembezoni mwa nchi (mipakani), bado wanapata changamoto ya kupata habari kwa sababu ya kutokuwa na usikivu wa masafa ya Shirika la Utangazaji *(TBC)*. Aidha, kwa Mradi wa Mkongo wa Taifa kutopokea fedha za kutosha, kunafifisha juhudi za kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mawasiliano ya kutosha nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha kwamba inatoa fedha kwa ukamilifu, usawa na kwa wakati ili kuchochea utekelezaji wa miradi yote kwa kuzingatia mahitaji ya wanachi na vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu taarifa za baadhi ya miradi iliyofanyiwa uchambuzi na Kamati:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mradi Na. 4283 - Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, hadi kufikia Februari, 2023 ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulikuwa umefikia kilometa 1,663 sawa na asilimia 37 ya lengo. Kazi nyingine iliyofanyika ni pamoja na kununua mitambo 26 kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma sawa na asilimia 23 ya lengo, na kukamilisha upembuzi yakinifu, kwenye vijiji 2,116 visivyokuwa na mawasiliano. Aidha, ujenzi wa Mkongo wa Taifa umefanyika kuunganisha Tanzania na Jamhuri

ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika kwa kilomita 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utekelezaji huo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali za utekelezaji wa miradi kama ifuatavyo:-

(i) Kasi ndogo ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa ikilinganishwa na lengo la mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, hatua za Wizara kuingia mkataba wa maelewano na Shirika la Umeme Tanzania kwa ajili ya kufanya kazi pamoja, zinaweza kuongeza ufanisi.

(ii) Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi hadi mwezi Februari, 2023 haukuwa wa kuridhisha. Kiasi cha fedha kilichopatikana ni asilimia 26.5 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji.

(iii) *TTCL* kutokuwa na mamlaka ya kuumiliki Mkongo wa Taifa kutokana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuendelea kuumiliki moja kwa moja, jambo linalosababisha mkanganyiko wa katika utendaji; na

(iv) Sheria ya Manunuzi haitoi fursa kwa *TTCL* kununua vifaa vya mawasiliano vilivyotumika kutoka kampuni nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha utaratibu wa kumilikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa *TTCL* na kuboresha Sheria za Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na. 4279 - Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC);* mradi huu umetengewa jumla ya shilingi 13,136,500,000 kwa mwaka 2022/2023. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2023 Wizara ilipokea shilingi 3,952,529,729.09 sawa na asilimia 30 ya lengo. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa usikivu kwenye Wilaya ya Mlele, Mbinga pamoja na ujenzi wa minara katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Pemba na Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa mradi huu zikiwemo usikivu hafifu wa redio za *TBC* hasa maeneo ya mipakani mwa nchi, ukosefu wa chanzo mahususi cha fedha kwa *TBC* kwa ajili ya uendeshaji na kugharamia miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini kuhusu namna bora ambayo itaisaidia *TBC* kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato ili kuiwezesha kujiendesha na kutekeleza kikamilifu miradi ya maendeleo hususani inayohusu usikivu wa masafa ya *TBC* nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makusanyo ya maduhuli, katika mwaka wa fedha 2022/2023, iliidhinishiwa kukusanya shilingi 150,700,000,000 wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 463.45.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2023, Wizara ilikusanya Shilingi bilioni 21.8 sawa na asilimia 14.46 ya lengo, wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya jumla ya shilingi bilioni 514. 5 sawa na asilimia 111.07 ya lengo. Kwa wastani, hali ya makusanyo ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake inaridhisha hadi kufikia Februari, 2023, ambapo ni robo ya tatu ya mwaka wa bajeti, makusanyo yalikuwa asilimia 94.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2023, *TCRA* ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 352.739 ambayo ni sawa na asilimia 226 ya lengo. Kamati imebaini kwamba, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Februari, 2023, *TCRA* iliuza masafa kwa njia ya mnada ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 221 kilipatikana ukilinganisha na shilingi bilioni 51 iliyopangwa kukusanywa katika chanzo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyingine zilizokusanya maduhuli kwa kiwango cha kuridhisha ni *UCSAF, TCRA-CCC, TTCL* na *TSN*. Kamati inazipongeza taasisi hizo kwa makusanyo hayo na inaendelea kuishauri Serikali kuboresha mifumo ya makusanyo na ufuatiliaji ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba, Wizara ilijiwekea malengo ya kukusanya shilingi bilioni 150.7 ambapo hadi kufikia Februari, 2023 ilifanikiwa kukusanya shilingi bilioni 21 tu ambayo ilitarajiwa na kutokana na mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pekee ungeweza kuipatia Wizara mapato ya takribani shilingi bilioni 99.5. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichokusanywa kufikia Februari, 2023 ni shilingi bilioni 10.7 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya sababu za kutofikiwa kwa malengo hayo, ni uwezo mdogo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo Wizara imeshindwa kuuza na hivyo kuilazimu Serikali kuchukua hatua za kuongeza uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ya kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ni kuwepo kwa makisio yasiyo na uhalisia. Hivyo basi, Serikali itathmini uwezo wa kila taasisi kuweka makisio ya makusanyo kulingana na uwezo wa taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyingine ambazo hazikuwa na makusanyo ya kuridhisha kufikia Februari, 2023 ni *TBC, ICTC*, na Shirika la Posta. Changamoto ya makusanyo hafifu inatokana na taasisi hizo kutokuwa na mifumo thabiti ya kukusanya maduhuli na pia kuwepo kwa malengo yasiyo na uhalisia kulingana na uwezo wa taasisi husika kukusanya. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya uwezo wa kila taasisi katika ukusanyaji wa mapato ili kuwa na malengo yanayoakisi uwezo wa taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya maoni na ushauri yaliyotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha, ni Serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Mfuko wa *UCSAF* pamoja na kuisimamia Shirika ya Mawasiliano *TTCL* kukamilisha miradi ya ujenzi wa minara ikiwa ni pamoja na kuwasimamia kwa karibu watoa huduma wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna baadhi ya maoni na ushauri wa kamati ambayo hayajatekelezwa kikamilifu. Kamati ilishauri Serikali kukabidhi uendeshaji wa Mkongo wa Taifa Mawasiliano kwa *TTCL*. Hata hivyo, Kamati ilitaarifiwa kwamba mchakato wa suala hilo unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Muundo wa bajeti, Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu 68 – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 210.95 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 29 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shillingi bilioni 181.95 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara imepungua kwa asilimia 25.27 kutoka shilingi bilioni 282 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Fedha ya Matumizi ya Kawaida imeongezeka kwa asilimia 10.4, fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo imepungua kwa asilimia 28.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kuwa hatua hii itaongeza motisha kwa Watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Makusanyo ya Maduhuli katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 770.16 Kiwango hiki ni ongezeko la asilimia 35.35 ukilinganisha na shilingi bilioni 569 iliyopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kipekee, Kamati inazipongeza taasisi chini ya Wizara ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa zile taasisi ambazo Katika mwaka wa fedha 2022/2023 hazikutimiza malengo ya makusanyo. Kamati inazishauri taasisi hizo kuhakikisha kwamba wanajiwekea mikakati madhubuti ya makusanyo ili kuiwezesha Serikali kutimiza malengo yake katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida, kwa ujumla Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa wastani wa asilimia 10.36 ukilinganisha na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* kutoka Shilingi bilioni 9.03 hadi Shilingi 10.48.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi Mengineyo *(OC)* kwa kuwa ongezeko hilo litasaidia masuala ya uratibu wa shughuli zinazosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maendeleo, katika mwaka wa fedha 2023/204, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 18.95 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa asilimia 28.9 ukilinganisha na Bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 146.77 ni fedha za ndani, nashilingi bilioni 35.17 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kamati imebaini kwamba, shilingi bilioni 35 zilizotengwa kwa fedha za nje ni kwa ajili ya kutekeleza Mradi Na. 4280 wa Tanzania ya kidijitali ikiwa ni pungufu kwa asilimia 10.94 ukilinganisha na shilingi bilioni 39.3 iliyotengwa kutekeleza Mradi huo katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sehemu ya dira ya Wizara ni kuwa na jamii iliyowezeshwa kidijitali kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kutenga fedha zitokanazo na makusanyo ya ndani ili kutekeleza mradi huo na hatimaye kufikia malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa jumla, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ina mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa na ukuaji wa uchumi. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali kama ifuatavyo: -

(a) Kamati imebaini kwamba, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Bajeti ya matumizi ya kawaida hususani matumizi mengineyo *(OC)* yameongezeka. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati ili kuwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri mahususi.

(i) Wizara ishirikiane na makampuni ya mitandao ya simu pamoja na Jeshi la Polisi ili kumaliza tatizo la utapeli wa kimtandao ikiwamo kufungia namba za matapeli. Aidha, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ishirikiane na vyombo vya dola ili kubaini na kuhakikisha kwamba wahalifu wa makosa ya mitandao wanashitakiwa;

(ii) *TCRA* itoe elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya data na vifurushi ili kuondoa malalamiko ya watumiaji wa huduma hiyo.

(iii) Serikali ipunguze gharama za mawasiliano pia *TCRA* ihakiki ubora wa mawasiliano yanayotolewa na watoa huduma ili kujua kama yana sifa na viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)*

(i) Serikali ibebe madeni inayodaiwa Shirila la Mawasiliano Tanzania ili kuweka sawa mizania ya hesabu zake ili kuiwezesha kupata mikopo katika taasisi za fedha.

(ii) *TTCL* waongeze ufanisi katika utekelezaji wa miradi wanayopewa ili ikamilike kwa wakati, mfano ujenzi wa minara.

(iii) Serikali ihakikishe michakato kuikabidhi *TTCL* usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa unakamilika ili uweze kujiendesha kibiashara;

(iv) Sheria ya manunuzi irekebishwe kwani inazuia *TTCL* kununua vifaa vya mawasiliano vilivyotumika toka kampuni nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta *(TPC)*

(i) Serikali iisaidie Posta kupata mtaji;

(ii) Serikali ifute deni kwa posta na ili kuweka sawa mizania ya hesabu zake;
(iii) Serikali isaidie shirika ili liweze kulipwa madeni yake kutoka taasisi za Serikali;

(iv) Serikali kwa kushirikisha wadau muhimu ifanye tathmini ili kuona iwapo inafaa kwa Shirika la Posta kupata kamisheni kutokana na usafirishaji wa mizigo na vipeto unaofanywa na kampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*

(i) Serikali iisaidie *TBC* ipate fedha za kutosha ili iweze kujiendesha kibiashara sambamba na kuboresha usikivu hasa maeneo ya mipakani na kuboresha miundombinu iliyochakaa;

(ii) *TBC* ifanye maboresho ya miundombinu ya hifadhi za hotuba za viongozi ili iwe ya kidijitali na kuwekwa katika majukwaa mbalimbali na mitandao ya kijamii kama vile *YouTube*;

(iii) Serikali iboreshe posho na stahiki kwa watumishi wa *TBC* na walipwe kwa wakati ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi;

(iv) Serikali iwezeshe *TBC* kupata mgao wa fedha kutoka kwa wadau wa Safari *Channel* ili waweze kufanya maboresho ya vipindi na kuchochea utalii;

(v) Serikali iongeze uwezo wa fedha kwa *UCSAF* ili iweze kuisaidia *TBC* kuongeza usikivu maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania *(TSN)*

(i) Serikali iisaidie *TSN* ili waweze kulipwa madeni wanayozidai Taasisi za Serikali;

(ii) Kutokana na ununuzi wa mitambo inayoendelea kufanyika katika kampuni ya *TSN,* Serikali iendelee kuisimamia *TSN* ili waweze kujiendesha kibiashara;

(iii) Taasisi za Serikali kutumia *TSN* katika huduma za machapisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimihsho, maelezo hitimisho, sekta ya habari na mawasiliano ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwani sekta hii huwezesha sekta nyingine zote kuweza kufikia malengo. Uwekezaji katika sekta ya mawasiliano ni chachu kubwa ya maendeleo ya uchumi na kijamii kama ilivyo katika uwekezaji wa huduma nyingine. Hivyo, ni muhimu Serikali kuhakikisha sekta hii inastawi na inachangia kwa kiwango kikubwa zaidi maendeleo ya uchumi wa nchi kama inavyoeleza katika ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Ibara ya 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani, napenda kumshukuru Spika Dkt. Tulia Ackson kwa kuongoza vema Bunge hili ukisaidiiwa na wewe Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano wa kutosha uliofanikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wao katika utekelezaji wa majukumu ya kamati naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akisaidiwa na Mheshimiwa *Engineer* Andrea Mathew Kundo, Mbunge Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Mohammed Khamis Abdullah, na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Selestine Gervas Kakele kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati kila mara walipohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wa kamati wanaipongeza sana Timu ya Yanga, *GSM* na *Engineer* Hersi kwa historia kubwa waliyoipatia nchi yetu kuingia katika fainali za shirikisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Shughuli za Bunge hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msimamo wa Kamati kuhusu hoja. Baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano a Teknolojia ya Habari, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

1.0 **UTANGULIZI**
1.1 Maelezo ya Awali
**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4): -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inajumuisha maelezo ya jumla, muundo wa taarifa, pamoja na ufafanuzi wa namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake.

b) Sehemu ya Pili ni Uchambuzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; pamoja na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Sehemu ya Tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na

d) Sehemu ya Nne ni Hitimisho

1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimballi yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika, k**atika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilifanya mambo yafuatayo: -

a) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1))
b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 (Kanuni ya 117 (1))
c) Kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.
d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SEHEMU YA PILI**

2.0 **UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

2.1 **Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.[1]

[1] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023

2.2 **Mawanda ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilichambua taarifa za utekelezaji za **Fungu 68** - Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2). Katika ulinganisho huo, Kamati ilitathmini mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo kwa Mwaka wa 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutathimini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika hatua hii, Kamati ilifanya tathimini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, ufanisi wa utekelezaji wa miradi husika pamoja na tija ambayo inapatikana katika miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi uliofanyika kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati imezingatia masuala muhimu yanayogusa sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Masuala hayo ni pamoja na umuhimu wa Wizara kuhakikisha inachangia utekelezaji bora wa Ibara ya 18 ya Katiba ambayo pamoja na masuala mengine, inaweka haki kwa kila mtu kutafuta, kupokea na kutoa habari; kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu ya kijamii.[2]

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na

[2] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Teknolojia ya Habari umehusisha taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni: -

a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)
b) Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)
c) Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)
d) Shirika la Posta Tanzania (TPC)
e) Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)
f) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)
g) Tume ya Taifa ya TEHAMA (ICTC)
h) Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC)

2.3 **Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023**

2.3.1 Malengo ya Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilijiwekea malengo ya utekelezaji wa bajeti. Malengo hayo yalijikita katika vipaumbele vifuatavyo: -

a) Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera zinazohusu Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, TEHAMA, Posta na Mawasiliano ya Simu;
b) Kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari nchini;
c) Kufanya tafiti, maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA;
d) Ulinzi na usalama wa mtandao;
e) Kusimamia ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na
f) Kuanzisha na kusimamia Postikodi.

2.3.2 Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo waliyojiwekea, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 282,056,786,000**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 26,279,346,000** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 255,777,440,000** kwa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2023 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Sh. 89,866,607,135.75** sawa na **asilimia**

**31.86** ya bajeti iliyodhinishiwa kwa Mwaka wa Feha 2022/2023. Kati ya fedha ziliopokelewa, **Sh. 12,785,953,117** ni fedha za Matumizi ya Kawaida (sawa na **asilimia 48.65** ya bajeti iliyoidhinishwa) na **Sh. 77,080,654,018.75** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (sawa na **asilimia 30.15** ya bajeti iliyoidhinishwa).

*Kielelezo Na. 1*




**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara uko chini ya matarajio kwani hadi kufikia Februari, 2023, fedha iliyopokelewa ilikuwa ni wastani wa chini ya **asilimia 32**. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba, fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kutolewa kwa wakati kabla ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 kuisha.

2.3.3 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 255,777,440,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 215,777,440,000** ni Fedha za Ndani na **Sh. 40,000,000,000** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, Fedha zilizotengwa zilikusudiwa kutekeleza Miradi ifuatayo: -

a) **Mradi Na. 4283** - Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano
b) **Mradi Na. 4280** - Tanzania ya Kidijitali
c) **Mradi Na. 4234** - Anwani za Makazi na Postikodi
d) **Mradi Na. 6226** - Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA
e) **Mradi Na. 6567**- Habari kwa Umma
f) **Mradi Na. 4279** - Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)
g) **Mradi Na. 6505** - Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kutathimini utekelezaji wa miradi husika na kutoa ushauri mahususi kwa Serikali ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoainishwa awali, wastani wa mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo ulikuwa chini ya matarajio kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2023 ni **asilimia 30.15** ya fedha ilikuwa imepokelewa kutekeleza miradi husika. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kati ya miradi hiyo, baadhi yake ilipokea fedha kwa wakati na kuvuka matarajio wakati miradi mingine ilipokea fedha pungufu.

**Mheshimiwa Spika, Mradi Na. 6505** - Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji unaotekelezwa na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ulipokea **asilimia 132** ya makisio hadi kufikia Februari, 2023. Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi huo na kujionea utekelezaji wake ambapo TSN ilikuwa tayari imenunua mitambo ya uchapaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huo ambao utaisaidia TSN kuongeza ufanisi wa kujiendesha na kuendana na mbadiliko ya teknolojia katika soko.
Aidha, Kamati imebaini kwamba **Mradi Na. 6567** - Habari kwa Umma ulikuwa umepokea **asilimia 92** ya makadirio na hivyo kuwezesha Wizara kuimarisha kitengo cha habari kwa umma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kamati imebaini kwamba, miradi mingine inayotekelezwa na Wizara ilikuwa imepokea fedha pungufu ambapo, kwa wastani, hadi kufikia Februari, 2023 miradi hiyo ilikuwa imepokea chini ya **asilimia 35** ya matarajio kama ifuatavyo: -

a) **Mradi Na. 4283** - Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulipokea **asilimia 25**
b) **Mradi Na. 4280** - Tanzania ya Kidijitali ulipokea **asilimia 26**
c) **Mradi Na. 4234** - Anwani za Makazi na Postikodi ulipokea **asilimia 30**
d) **Mradi Na. 6226** - Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA ulipokea **asilimia 15**
e) **Mradi Na. 4279** - Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ulipokea **asilimia 30**

**Mheshimiwa Spika,** hali ya mapokezi hafifu ya fedha iliyotengwa, inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi na kufifisha manufaa yaliyotarajiwa. Mathalani, wananchi hasa wa pembezoni mwa nchi (mipakani), bado wanapata changamoto ya kupata habari kwa sababu ya kutokuwa na usikivu wa masafa ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Aidha, kwa Mradi wa Mkongo wa Taifa kutopokea fedha za kutosha, kunafifisha juhudi za kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mawasiliano ya kutosha nchi nzima.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha kwamba inatoa fedha kwa ukamilifu, usawa na kwa wakati ili kuchochea utekelezaji wa miradi yote kwa kuzingatia mahitaji ya wanachi na vipaumbele vya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muhtasari, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu taarifa za baadhi ya miradi iliyofanyiwa uchambuzi na Kamati:-

a) **Mradi Na. 4283 - Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**
**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi kufikia Februari, 2023 ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulikuwa umefikia kilometa 1663 sawa na **asilimia 37** ya lengo. Kazi nyingine iliyofanyika ni pamoja na kununua mitambo 26 kwa ajili ya vituo

vya kutolea huduma sawa na asilimia 23 ya lengo, na kukamilisha upembuzi yakinifu, kwenye vijiji 2116 visivyokuwa na mawasiliano. Aidha, ujenzi wa Mkongo wa Taifa umefanyika kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia ziwa Tanganyika Kwa kilomita 60.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji huo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali za utekelezaji wa miradi kama ifuatavyo: -

i) Kasi ndogo ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa ikilinganishwa na lengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, hatua za Wizara kuingia mkataba wa maelewano na shirika la umeme Tanzania kwa ajili ya kufanya kazi pamoja, zinaweza kuongeza ufanisi.

ii) Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi hadi mwezi Februari, 2023 haukuwa wa kuridhisha. Kiasi cha fedha kilichopatikana ni **asilimia 26.5** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji;

iii) TTCL kutokuwa na mamlaka ya kuumiliki Mkongo wa Taifa kutokana na Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuendelea kuumiliki moja kwa moja, jambo linalosababisha mkanganyiko wa kiutendaji; na

iv) Sheria ya manunuzi haitoi fursa kwa TTCL kununua vifaa vya mawasiliano vilivyotumika kutoka kampuni nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha utaratibu wa kumilikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa TTCL na kuboresha sheria za manunuzi.

*b)* ***Mradi Na. 4279 - Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)***

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulitengewa jumla ya **Sh. 13,136,500,000** kwa mwaka 2022/23, Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 28 Februari 2023 Wizara ilipokea **Sh. 3,952,529, 729.09** sawa na **asilimia 30** ya lengo. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa usikivu kwenye wilaya ya Mlele na Mbinga

pamoja na ujenzi wa minara katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Pemba na Unguja.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa mradi huu zikiwemo: -

i) Usikivu hafifu wa redio za TBC hasa maeneo ya mipakani mwa nchi.
ii) Ukosefu wa chanzo mahususi cha fedha kwa TBC kwa ajili ya uendeshaji na kugharamia miradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini kuhusu namna bora ambayo itaisaidia TBC kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato ili kuiwezesha kujiendesha na kutekeleza kikamilifu miradi ya maendeleo hususani inayohusu usikivu wa masafa ya TBC nchi nzima.

2.3.4 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, iliidhinishiwa kukusanya **Sh. 150,700,000,000** wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiriwa kukusanya **Sh. 463,455,215,184.65**. Fedha hizo zilitarajiwa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo ada na tozo, mauzo ya picha za viongozi, mauzo ya masafa, na huduma mbalimbali ikiwemo huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023, Wizara ilikusanya **Sh. 21,803,399,822.60** sawa na **asilimia 14.46% ya lengo** wakati taasisi zilizo chini ya Wizara zilikusanya jumla ya Sh. ya **Sh. 514,772,233,347.65** sawa na **asilimia 111.07** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, hali ya makusanyo ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake inaridhisha kuwa hadi kufikia Februari, 2023, ambapo ni robo ya tatu ya mwaka wa bajeti, makusanyo yalikuwa **asilimia 94.3**. Pamoja na hali hiyo, Kamati imebaini masuala kadhaa kuhusu mwenendo wa makusanyo ambapo baadhi ya taasisi zimefanya vizuri katika ukusanyaji na kuvuka malengo wakati taasisi nyingine hazikufikia malengo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023, TCRA ilikuwa imekusanya **Sh. Bilioni 352.739** ambayo ni sawa na **asilimia 226** ya lengo. Kamati imebaini kwamba, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Februari 2023, TCRA iliuza masafa kwa njia ya mnada ambapo kiasi cha **Sh. Bilioni 221** kilipatikana ukilinganisha na **Sh. Bilioni 51** iliyopangwa kukusanywa katika chanzo hicho.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi nyingine zilizokusanya maduhuli kwa kiwango cha kuridhisha ni UCSAF, TCRA-CCC, TTCL na TSN kama ambavyo imeainishwa katika **Kielelezo Na. 2**. Kamati inazipongeza taasisi hizo kwa makusanyo hayo na inaendelea kuishauri Serikali kuboresha mifumo ya makusanyo na ufuatiliaji ili kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Wizara ilijiwekea malengo ya kukusanya **Sh. Bilioni 150.7** ambapo hadi kufikia Februari, 2023 ilifanikiwa kukusanya **Sh. Bilioni 21** tu. Kwa malengo ambayo Wizara ilijiwekea, ilitarajiwa kwamba, mauzo ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pekee ungeweza kuipatia Wizara mapato ta takribani **Sh. Bilioni 99.5**. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichokusanywa kufikia Februari, 2023 ni **Sh. Bilioni 10.7** tu. Kamati ilitaarifiwa kwamba, moja kati ya sababu za kutofikiwa kwa malengo hayo ni uwezo mdogo *(capacity)* wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo Wizara imeshindwa kuuza na hivyo kuilazimu Serikali kuchukua hatua za kuongeza uwezo wake.

**Mheshimiwa Spika**, sababu nyingine ya kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ni kuwepo kwa makisio yasiyo na uhalisia, hivyo basi Serikali itathimini uwezo wa kila taasisi na kuweka makisio ya makusanyo kulingana na uwezo wa taasisi kukusanya.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi nyingine ambazo hazikuwa na makusanyo ya kuridhisha kufikia Februari, 2023 ni TBC, ICTC, na Shirika la Posta.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, changamoto ya makusanyo hafifu inatokana na taasisi hizo kutokuwa na mifumo thabiti ya kukusanya maduhuli na kuwepo kwa malengo yasiyo na uhalisia kulingana na uwezo wa taasisi hizo kukusanya. Kamati

inaishauri Serikali kufanya tathmini ya uwezo wa kila taasisi katika ukusanyaji wa mapato ili kuwa na malengo yanayoakisi uwezo wa taasisi.

2.3.5 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lako lilipopitisha Bajeti ya **Fungu 68** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati isipokuwa kwa maeneo machache ambayo hayajatekelezwa kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya maoni na ushauri yaliyotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha, ni Serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Mfuko wa UCSAF pamoja na kuisimamia Shirika ya Mawasiliano (TTCL) kukamilisha miradi ya ujenzi wa minara ikiwa ni pamoja na kuwasimamia kwa karibu Watoa Huduma Wengine.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Serikali imeendelea kuisaidia UCSAF katika kutafuta pesa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mawasiliano vijijini. Katika mwaka huu wa 2022/2023, Serikali imetenga jumla ya Dola za Marekani milioni 30 kupitia fedha za mradi wa Tanzania ya Kidigitali ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia ili kutekeleza miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini. Fedha hizo zitawezesha ujenzi wa minara katika maeneo 763 na sehemu nyingine ya fedha hizo zitatumika kuongeza nguvu ya minara 488.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, kuna baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati ambayo hayajatekelezwa kikamilifu. Kamati ilishauri Serikali kukabidhi uendeshaji wa Mkongo wa Taifa Mawasiliano kwa TTCL. Hata hivyo, Kamati ilitaarifiwa kwamba mchakato wa suala hilo unaendelea.

2.3.6 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kufanya uchambuzi wa majukumu yaliyotekelezwa na Wizara na taasisi zake. Baadhi ya majukumu yaliyotekelezwa ni kama ifuatavyo: -

*a)* ***Shirika la Posta (TPC)***

**Mheshimiwa Spika**, Shirika limeboresha miundombinu ya mtandao wa eneo mahususi (LAN) katika ofisi kuu za Posta 12 ikiwemo Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na maeneo mengine. Aidha, Shirika limefanikiwa kupata mradi wenye thamani ya dola za marekani 120,000 kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa utumiaji na upokeaji fedha kwa njia ya kielectroniki

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Posta linakabiliwa na changamoto kubwa kama zifuatazo: -

i) Shirika kutokuwa na mtaji wa kutosha; ii) Shirika kuelemewa na deni la Sh. Bilioni **26.8** kutokana na kushindwa kuwasilisha kodi, riba mbalimbali kwa wakati (PAYE, SLD na VAT) kati ya 2007 na 2016; na

iii) Taasisi za serikali kutolipa fedha wanazodaiwa na shirika.

*b)* ***TCRA***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea TCRA ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa masuala mbalimbali. Moja kati ya shughuli zilizofanyiwa ukaguzi na Kamati ni utendaji wa Mfumo wa Kusimamia Mawasiliano (TTMS). Mfumo huu unawezesha kufuatilia kwa karibu watoa huduma pamoja na kupata takwimu mbalimbali za mawasiliano. TCRA imeendelea kusimamia uendeshaji wa mtambo ambao unawezesha
yafuatayo: -

(i) Kubaini simu za ulaghai
(ii) Kanzidata ya namba tambulishi
(iii) Usajili wa namba za simu i

(iv) Usimamizi wa simu za ndani na Kimataifa
(v) Usimamizi wa miamala ya fedha
(vi) Ufuatiliaji wa miamala ya watoa huduma za malipo
(vii) Kuhakiki mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano ya simu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba TCRA inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i) Changamoto za usalama wa mtandaoni na uhalifu wa mtandaoni kuongezeka; na

ii) Kutokuwepo kwa bodi ya wakurugenzi ya TCRA;

iii) Kutokuwepo na uelewa wa matumizi sahihi ya vifurushi na data katika jamii;

iv) Changamoto ya ubora wa huduma katika mawasiliano; na

v) Kupanda kwa gharama za mawasiliano (data na vifurushi).

2.4 **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

2.4.1 Muundo wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, **Fungu 68** – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 210,957,625,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Sh. 29,003,685,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 181,953,940,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2), Kamati ilifanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Mwaka wa Feha 2023/2024. Kielelezo Na. 4 kinabainisha tofauti ya makadirio hayo.

*Kielelezo Na. 4*




**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Wizara imepungua kwa **asilimia 25.27** kutoka **Sh. Bilioni 282** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kufikia **Sh. Bilioni 210** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Fedha ya Matumizi ya Kawaida imeongezeka kwa **asilimia 10.4**, fedha iliyotengwa kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo imepungua kwa **asilimia 28.9**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi ya Kawaida kwa kuwa hatua hii itaongeza motisha kwa Watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

2.4.2 Malengo ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/204, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya **Sh. 770,161,665,188.62.** Kiwango hiki ni ongezeko la **asilimia 35.35** ukilinganisha na **Sh. 569,004,647,064** iliyopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. **Kielelezo Na. 5** kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli hayo.

*Kielelezo Na. 5*

| TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2022/2023 (TZS) | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2023/2024 (TZS) | TOFAUTI KWA ASILIMIA (+/-) |
|---|---|---|---|
| WIZARA | 150,700,000,000 | 150,700,000,000 | 0% |
| TCRA | 155,897,258,292 | 221,167,037,333.62 | +42.2% |
| TCRA - CCC | 710,000,000 | 710,000,000 | 0% |
| TTCL | 145,391,356,216 | 240,000,000,000 | +65% |
| POSTA | 43,761,234,400 | 39,476,613,000 | -9.79% |
| UCSAF | 34,760,583,156 | 35,102,688,605 | +0.98% |
| ICTC | 5,468,105,000 | 5,284,725,000 | -3.4% |
| TBC | 15,809,165,000 | 46,860,319,000 | +196% |
| TSN | 16,506,945,000 | 30,860,282,250 | +87 |
| **JUMLA** | **569,004,647,064** | **770,161,665,188.62** | **+35.35%** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kipekee, Kamati inazipongeza taasisi chini ya Wizara ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa zile taasisi ambazo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 hazikutimiza malengo ya makusanyo kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa katika **Kielelezo Na. 2**, Kamati inazishauri taasisi hizo kuhakikisha kwamba wanajiwekea mikakati madhubuti ya makusanyo ili kuiwezesha Serikali kutimiza malengo yake katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

2.4.3 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 10.36** ukilinganisha na Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka

kwa fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) kutoka **Sh. 9,030,029,000** hadi **Sh. 10,481,530,000**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) kwa kuwa ongezeko hilo litasaidia masuala ya uratibu wa shughuli zinazosimamiwa na Wizara.

2.4.4 Mpango wa Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/204, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 181,953,940,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa **asilimia 28.9** ukilinganisha na Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama ambavyo imeainishwa katika **Kielelezo Na. 3**. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 146,777,440,000** ni Fedha za Ndani, na **Sh. 35,176,500,000** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, **Sh. Bilioni 35** zilizotengwa kwa Fedha za Nje ni kwa ajili ya kutekeleza **Mradi Na. 4280** wa Tanzania ya Kidijitali ikiwa ni pungufu kwa **asilimia 10.94** ukilinganisha na **Sh. Bilioni 39.3** iliyotengwa kutekeleza Mradi huo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Fedha hizo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa sehemu ya Dira ya Wizara ni kuwa na jamii iliyowezeshwa kidijitali kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kutenga fedha zitokanazo na makusanyo ya ndani ili kutekeleza mradi huo na hatimaye kufikia malengo hayo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 **MAONI NA USHAURI**

3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ina mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa na ukuaji wa uchumi. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali kama ifuatavyo: -

a) Kamati imebaini kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida hususani Matumizi Mengineyo (O.C) yameongezeka. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati ili kuwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inashauri Wizara na taasisi hizo kuwa wabunifu wa namna bora ya utekelezaji wa majukumu yao ili fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) zinazofika zinatumika kwa weledi.

b) Serikali itumie fedha za mafunzo na matumizi mengineyo kuwapatia watumishi mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi.

3.2 Maoni na Ushauri Mahususi

***Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)***

a) Tatizo la utapeli kwenye mitandao ya simu za mkononi bado ni kubwa litafutiwe ufumbuzi wa kudumu sambamba na kuzuia jumbe fupi zinazotumwa bila idhini au matakwa ya mteja;

b) Wizara ishirikiane na makampuni ya mitandao ya simu pamoja na Jeshi la Polisi ili kumaliza tatizo la utapeli wa kimtandao ikiwamo kufungia namba za matapeli. Aidha, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ishirikiane na vyombo vya dola ili kubaini na kuhakikisha kwamba wahalifu wa makosa ya mitandao wanashitakiwa;

c) TCRA itoe elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya data na vifurushi ili kuondoa malalamiko ya watumiaji wa huduma hiyo;

d) Serikali ipunguze gharama za mawasiliano pia TCRA ihakiki ubora wa mawasiliano yanayotolewa na watoa huduma ili kujua kama yanakidhi sifa na viwango vinavyotakiwa.

***Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)***

a) Serikali ibebe madeni inayodaiwa Shirila la Mawasiliano Tanzania ili kuweka sawa mizania ya hesabu zake ili kuiwezesha kupata mikopo katika taasisi za fedha;

b) TTCL waongeze ufanisi katika utekelezaji wa miradi wanayopewa ili ikamilike kwa wakati, mfano ujenzi wa minara;

c) Serikali isimamie TTCL ili iweze kulipwa madeni wanayodai Taasisi za Serikali;

d) Miundombinu ya TTCL itumiwe pia na TBC ili kuboresha ufanisi wa usikivu wa redio na runinga;

e) Serikali iharakishe mchakato wa kuikabidhi TTCL usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa ili uweze kujiendesha kibiashara;

f) Elimu itolewe kwa wananchi kuhusu utunzaji wa miundombinu kando ya barabara; na

g) Sheria ya manunuzi irekebishwe kwani inazuia TTCL kununua vifaa vya mawasiliano vilivyotumika toka kampuni nyingine; na

h) Serikali iangalie upya tozo ya upitishaji wa Mkongo wa Taifa pembeni mwa barabara hususani TANROADS.

***Shirika la Posta (TPC)***

a) Serikali iisaidie Posta kupata mtaji;

b) Serikali ifute deni kwa Posta na ili kuweka sawa mizania ya hesabu zake;

c) Serikali isaidie shirika ili liweze kulipwa madeni yake kutoka taasisi za Serikali;

d) Serikali kwa kushirikisha wadau muhimu ifanye tathmini ili kuona iwapo inafaa kwa Shirika la Posta kupata kamisheni kutokana na usafirishaji wa mizigo na vipeto unaofanywa na kampuni binafsi nchini.

***Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)***

a) Serikali iisaidie TBC ipate fedha za kutosha ili iweze kujiendesha kibiashara sambamba na kuboresha usikivu hasa maeneo ya mipakani na kuboresha miundombinu iliyochakaa;

b) TBC ifanye maboresho ya miundombinu ya hifadhi za hotuba za viongozi ili iwe ya kidijitali na kuwekwa katika majukwaa mbalimbali na mitandao ya kijamii *(Mf. YouTube)*;

c) Serikali iboreshe posho na stahiki kwa watumishi wa TBC na walipwe kwa wakati ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi;

d) Serikali iwezeshe TBC kupata mgao wa fedha kutoka kwa wadau wa Safari Channel ili waweze kufanya maboresho ya vipindi na kuchochea utalii.

e) Serikali iongeze uwezo wa fedha kwa UCSAF ili iweze kuisaidia TBC kuongeza usikivu maeneo ya mipakani.

***Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania (TSN)***

a) Serikali iisaidie TSN ili waweze kulipwa madeni wanayozidai Taasisi za Serikali;

b) Kutokana na ununuzi wa mitambo inayoendelea kufanyika katika kampuni ya TSN, Serikali iendelee kuisimamia TSN ili waweze kujiendesha kibiashara; na

c) Kamati inazishauri Taasisi za Serikali kutumia TSN katika huduma za machapisho, majarida na makala.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 **HITIMISHO**

### 4.1 Maelezo ya Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Habari na Mawasiliano ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwani sekta hii huwezesha sekta nyingine zote kuweza kufikia malengo. Uwekezaji katika sekta ya mawasiliano ni chachu kubwa ya maendeleo ya uchumi na kijamii kama ilivyo katika uwekezaji wa huduma nyingine. Hivyo ni muhimu Serikali kuhakikisha sekta hii inastawi na inachangia kwa kiwango kikubwa zaidi maendeleo ya uchumi wa nchi kama inavyoeleza katika ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Ibara ya 61.

### 4.2 **Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza vema Bunge hili ukisaidiiwa na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, na kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano wa kutosha uliofanikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati.

Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Angelina Malembeka, Mb. | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Livingstone Lusinde, Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mwatum Dau Haji, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Santiel Eric Kirumba, Mb. | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb. - Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akisaidiwa na Mhe. Eng. Andrea Mathew Kundo, Mb. – Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti.

Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Mohammed Khamis Abdullah, na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Selestine Gervas Kakele kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati kila mara walipohitajika kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ***ndc*** kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Shughuli za Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, ***ndc***, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Yona Kirumbi na Ndg. Janeth Malangu wakisaidiwa na Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.3 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu
19 Mei, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tuna wageni wa ziada wa Mheshimiwa Nape, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Ndugu Lilian Madeje ambae anatoka kwenye tume ya *TEHAMA*, Liliani Madeje na tume yenu ya *TEHAMA* ahsanteni. Mkurugenzi wa Star times Ndugu Seleman Kwa niaba ya Katibu Mkuu, Ndugu Golden pota Mkurugenzi Mkuu Minara Tanzania *Ltd*, karibu. Dangilo Kaniki, Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano Serikalini, Minara Tanzania, Jackline Waiso, Mkurugennzi wa *Multichoice* Tanzania *DSTV*, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaanza sasa mjadala, tunaanza na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ajiandae Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, Antipas Mgungusi.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuanza kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na leo tuko hapa salama kabisa. Pia, tumpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweka fedha nyingi sana kwenye Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. N

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri, rafiki yangu Nape Nnauye na Naibu Waziri, *Engineer* Kundo, kwa kazi nzuri sana ambayo mnafanya na tukianzia na hafla ile ya kusaini mikataba kwa ajili ya minara karibu 158. Kwa kweli hongereni sana ile ilikuwa ni *innovation* nzuri sana na sisi tunaotoka vijijini mmetufurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wizara hii ni muhimu sana. Huko duniani sasa *digital economy* ni kitu muhimu sana na ndio dunia ya sasa inakokwenda. Pia, nilikuwa nasoma ripoti ya World Bank hapa tunaambiwa *digital economy* ina *range between 14 to 16 percent* ya *GDP*. Kwa hiyo, ni eneo zuri sana na lazima kwa kweli tuendeleze na tuweke pesa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Katibu Mkuu na timu nzima ya wizara hii na hasa hasa Mkurugenzi wa *UCSAF* unajua sisi tunaotoka vijijini ni lazima tumsifie Mkurugenzi wa *UCSAF, I think she is the best CEO in my opinion. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliandika ripoti hapa 2021, Mheshimiwa Waziri, nilileta kata karibu 15 za Kiteto zilikuwa na shida ya mawasiliano lakini leo kwenye bajeti yako hapa nimefurahi sana. Nimesoma ukurasa wa 100 nimekuta kata 12 zipo kwenye minara hiyo. Kata za Laiseri vijiji vyote kata hiyo ilikuwa haina mnara hata mmoja leo naona hapa. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru ulimtuma Mheshimiwa Naibu Waziri, alifika Kata hii ya Laiseri. Kwa hiyo, wananchi wa huko Kiteto wa Kata ya Laiseri, Lengatei, Loolera, Magungu, Namelock, Partimbo, Sunya, Loitepesi, Songambele, Peresa, Njoro, Dosidosi, Ndirigishi. Sasa, tutaachaje kusifia kwa namna hiyo? *Honestly* kata karibu 12 na vijiji zaidi ya 23. Mwenyezi Mungu awabariki sana na wananchi wa Kiteto kwa kweli watakuwa wamefarijika na bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, liko jambo hapa la wizi unaotokana na mitandao. Imekuwa ni janga kubwa kidogo na linawasumbua sana watanzania walio wengi. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri, tuendelee kuongeza teknolojia ili wezi hawa na matapeli wa mitandao wasiwatapeli watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, tumekuwa unajua kwa mujibu wa Sheria kila mtu anatakiwa aripoti kosa na tumekuwa tuki–*volunteer.* Hawa matapeli wanaotupigia tumekuwa tunaripoti kwa makampuni ya simu. Ambacho hatupati ni *feedback* kutoka kwa makampuni ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima mkampuni ya simu yatuambie kama wateja kwamba ile simu uliyoripoti na sisi tumefanya moja, mbili, tatu na tunaendelea. Hiyo itajenga *customer care* nzuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, wewe waandikie makampuni ya simu hapa. Haiwezekani sisi turipoti halafu tena wakati mwingine wanasema kabisa kwa *quality control* tunarekodi hii simu yako tusikilize halafu tunaripoti hizi simu na hawatupi mrejesho. Wakifanya hivyo itasaidia kupunguza wizi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri, vyombo vya habari. Vyombo vya habari ni sekta muhimu sana na kwa kweli nakumbuka *incident* yako moja wapo jana nilikuwa naangalia *YouTube,* vyombo vya habari vilifanya kazi nzuri sana. *If it wasn't* wao sijui tukio lile lilikuwaje. Kwa hiyo, *please* wasaidie sana na mkae. Ni taaluma ambayo ni nzuri sana inatupatia habari na kupata habari ni jambo la kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri, alisema Mheshimiwa Rais, siku ile ya kusaini mikataba, kwa sababu ya Sheria hizi za manunuzi kutengeneza mlolongo ambao ni *bureaucracy* kubwa inachukua muda wakati fulani, tungependa minara hii ifike vijijini kwa haraka. Pia, Mheshimiwa Rais, alisema mwezi mkoja tu na ilikuwa tarehe 13 karibu wiki moja sasa hivi imekwishakatika. Sisi ambao tumefurahi kupata minara hii tunategemea baada ya mwezi mmoja vibali vile vinavyotakiwa viwe vimepatikana lakini lazima mlete Sheria ya *Procurement* tuangalie ipunguze hii *bureaucracy.*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tupate pesa halafu tuendelee kukaa miezi sita, nane kwa sababu ya kuleta vifaa. Tunataka wananchi wapate huduma hii kwa haraka sana. Nadhani kwa sababu tunazungumzia habari ya kidijitali na

TEHAMA, nilifikiri wewe ungekuwa na *regime* tofauti kabisa. Yaani wewe lazima uende haraka zaidi kuliko wengine. Haiwezekani wewe uwe na sekta hii ambayo tunazungumza habari ya kidijitali halafu *bado Procurement Law* ile ambayo inachukua muda mrefu zaidi inafanya kama vile ni *manual system.*Vile vile, hata hapa Mheshimiwa Naibu Spika, amesema wewe umetumia muda mfupi sana hapa, hiyo ndio *TEHAMA*, ndio *digital.* Kwa hiyo, lazima ninyi muwezeshwe mwende haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nilizungumza mwaka 2021 na 2022, kuhusu *Radio* Tanzania kutokusikika Kiteto lakini vilevile nafarijika kwenye hotuba yako ya mwaka 2022 na hata safari hii nimeona Kiteto ukurasa wa 125 kwamba mtaongeza usikivu, watanzania wale wa Kiteto ni vema wakaanza kufuatilia redio yao ya Tanzania. Haiwezekani miaka 60 baada ya uhuru bado wana Kiteto hawapati taarifa kutoka redioTanzania. kwa hiyo, nakushukuru sana kwamba Kiteto sasa itafunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri, suala hili la mawasiliano, tulikuona ukienda Mlima Kilimanjaro kupandisha *internet.* Unajua wakati tunapandisha Mwenge wa Uhuru Mlima Kilimanjaro kulikuwa na *quotation* nzuri sana ya Baba wa Taifa. Sasa lazima tuwe na *slogan* sasa kwa kuwa Mlima Kilimanjaro ni mlima mrefu Afrika lazima tuwe na *slogan* ya kupandisha ile na mantiki yetu ni nini?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ahsante.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naunga mkono hoja na Mungu awabariki sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante *Advocate* kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Ally Anyigulile, ajiandae Mheshimiwa Mgungusi.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Hapa juzi tumeshuhudia utiaji wa saini wa minara 758 ambayo inakwenda kujengwa kwenye maeneo ambayo ni ya wananchi wa kawaida sana. Hii imetokea

ni kwa mkupuo mmoja kwa mwaka mmoja. Huko nyuma tangu uwepo wa Tanzania imekuwepo minara 1383 tu. Jambo kama hili linatokea kipindi hiki cha Mheshimiwa wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, haijawahi kutokea kipindi chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nataka nisema sisi Wabunge kama wawakilishi wa wananchi hatutakiwi kuona haya wala soni kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Waswahili wanasema mtu husifia chake hasa kinapompendeza. Mheshimiwa Rais, anatupendezesha Tanzania inang'ara. Ahsante sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanayofanyika lengo lake kubwa ni kuhakikisha ufanisi wa mawasiliano, *data* lakini pia kumpunguzia mzigo wa gharama za *bundle* mtanzania aliyeko huko chini. Pia, haya yatawezekana iwapo kila unapokwenda mnara *REA* watapeleka umeme na umeme utarahisisha uendeshaji wa minara hiyo badala ya sasa ambapo minara inazungushiwa mafuta ya *diesel* kila siku, inaongeza gharama kubwa

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko zote, pamoja na minara yote hiyo ubora wa mawasiliano, ubora wa usikivu usipoboreshwa tutaendelea kuliwa. Na nataka niseme, katika hili kuna mahali mimi ninaamini sisi hatuko vizuri katika Tanzania na hasa katika *vertical modulation.* Namuona Mheshimiwa Waziri anacheka, ni kwa sababu nimekuwa nikiwaambia siku zote. Hawa Mawaziri wako vizuri sana na nataka niseme ingekuwa ni kipindi kile ndio tunaoita wanajeshi wa mwamvuli lakini katika hili la *vertical modulation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumefeli hata ukisafiri kidogo ukipanda kakichuguu tu mawasiliano yanakatika na yanapokatika hela yetu inaliwa huko ndiko tunakowaibia wananchi

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano mmoja, ukitoka Kasumuru kwenda Blantyre, Malawi ni kilomita zaidi ya 1300. Ukitoka pale, kama unaongea na simu unauwezo wa kuongea na

simu isikatike unapanfa milima unashuka milima mpaka unafika Blantyre. Tanzania nini kinashindikana? Ninaiomba Serikali yangu iangalie ubora wa mitandao ili wananchi wapate ile quality inayotakiwa kwenye usikivu na pia hata kwenye pesa yao wanayoitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo usikivu tu, hata hapahapa ukimpigia mtu simu ukiongea dakika moja hujamalizia hata ya pili itakuta mikwaruzo imeshaingia kwenye simu. Sasa hapo ubora unakuwa wapi ningeomba hili liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili niipongeze Serikali, imenunua mtambo wa kuchapa hapa kwa wenzetu wa *TSN,* lakini pamoja na juhudi zote hizi iwapo Serikali na Mawaziri hamtasisitiza wadaiwa wa taasisi hizi pamoja na taasisi zingine, hasa Serikali na Wizara kutokulipa madeni tutakuwa tunaua kabisa. Hata tununue mitambo gani msipolipa madeni mtakuwa mnaua kabisa haya mashirika yetu. Tunaomba mlipe madeni mnayodaiwa. Na mnapolipa madeni msiwape hawa wanao simamia wakaanza kuota mnvi kwa sababu inaonekana wao hawadai wakati ni ninyi hamlipi. Kuna wakati mtu unaweza ukadai ukashindwa; sasa naomba tuwasimamie hawa wenzetu wapate pesa zao ni pamoja na *TTCL* wapewe pesa zao wanazodai kwenye Mashirika, Posta vivyo hivyo Serikali isimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kuhusu hawa vijana wanaoanza kwenye TEHAMA. Nashukuru sana wapo *startups* wanakuwa wanalelewa. Wapo Watanzania wazuri hata ukienda kule kwangu Kyela ukienda Mbeya, wana uwezo wa kutengeneza mifumo yote katika Serikali hii *e-GA* kwa nini inang'ang'ania kutengeneza mifumo wakati wapo vijana ambao kwa kuwapa kazi tungetoa ajira lakini pia tungepata kodi? *e-GA* ambacho wanatakiwa kufanya ni kusimamia ubora na kuangalia uendeshaji wa mifumo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni kuhusu suala la anuani za makazi. Imekuwa kama watu wamerusha tu hili jambo linafanyika. Hivi kweli Tanzania tumekosa majina? Mtu anasema Barabara ya Shule, Barabara ya *Church*, Barabara ya Msikiti,

Barabara ya *Mosque*. Kweli hakuna majina kabisa Tanzania? Tumeshindwa hata kutoa majina hata ya Wanyama? Haiwezekani, tusijidharirishe, unapoandika anuani hii ni ya kimataifa, unapo mwambia mtu alieko Marekani mimi naishi kwenye barabara ya *school* anakushangaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Antipas Zeno, jiandae Mheshimiwa Yahaya Massare, jiandae Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi kwanza nimesimama ku-*withdraw* mchango wangu wa leo kwa maana ya kwamba nimeshapata majibu jana kwa Waziri nimepata minara ya kutosha Malinyi na sasa wakandarasi wako *site* kwa hiyo sina cha kuchangia nashukuru *UCSAF* na Wizara ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Yahaya Massare jiandae Mheshimiwa Zuena Bushiri, jiandae Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi, na mimi nishukuru Serikali ya chama changu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kazi hii ambayo sasa inaenda kuifanya nchi ifunguke kwa mawasiliano. Ni juzi tu tumeshuhudia pale Mheshimwa Rais akishuhudia kusainiwa kwa minara 758 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tukio ambalo kwa hakika litakuwa Faraja sana minara hii ikijengwa katika nchi hii na mimi eneo langu lilikuwa na changamoto hii na tunatenda kutibu japo hatumalizi. Tumepata minara michache sana. Katika majimbo yaliyopata minara michache mojawapo ni la kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi nimepata minara minne tu. Mnara wa Rungwa, katika Kata ya Rungwa, Mnara wa Kintanura Kata ya Mwamagembe, Mnara wa Gurungo katika Kata ya Sanjaranda na Mnara wa Ipalari katika Kata ya Kintinku. Katika

Wilaya ya Manyoni tumepata minara mingi sana lakini imeelemea jimbo moja. Kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri alione hili. na uhitaji wa minara michache sana mitatu tu tukipata tutafungua watu wetu. Mnara wa Mhanga katika Kata ya Ipande, Mnara wa Tulieni katika Kata ya Kalangali na Mnazi katika kata hiyohiyo ya Kalangali, tutakuwa tumelifungua Jimbo la Manyoni Magharibi, Halmashauri ya Itigi kwa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto, minara mingi iliyopo katika jimbo langu ni ya 2G michache sasa inaanza kwenda katika 3G. Dunia imehama. Dunia imehama kutoka katika *talking* na sasa watu wengi wanatumia data, na hata wanapiga simu za kutumia data mawasiliano ya kimataifa Zaidi, ni pamoja na watu wangu, pamoja na kuwa ni wa maeneo ya vijijini lakin,i sasa hivi nao wamekwenda katika ulimwengu wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana Wizara hii ya vijana hawa ambao ni mahiri kabisa, na umemsifia Waziri wa Wizara hii kwa kutumia dakika chache kusoma taarifa yake kuliko Mawaziri wote katika Bunge hili. Kwa hiyo kwa umahiri huu ninaomba sasa autumie ili kuhakikisha maeneo yote ya nchi hii yanafunguka, likiwemo jimbo langu. Minara hii mitatu ninaiomba, tuhakikishe wananchi wa eneo hili ambao nao wanasumbuka kupata mawasiliano nao wanapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo hili la bando, nimeendelea kuwaomba Wahesimiwa Mawaziri, watumishi na wadau katika Wizara hii. Watu wa umeme wana Luku. Ukiweka Luku yako kwa kadri ya pesa ulizoweka itakwisha pale matumizi yatakuwa umetumia lakini bando ukiweka hata muda ukiisha yaani haujatumia kwa sababu tu ni la muda maalum inakuwa imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa basi tusaidiwe katika suala hili tufike mahali zihesabiwe kama ni *unit* kama ni kitu gani kutokana na utaratibu wenu basi matu matumizi yake ndio yalingane na malipo yale isiwe ni bando la muda maalum. Inawezekana ukaomba bando la wiki moja lakini matumizi yale ndani ya wiki moja yasiishe, kwa hiyo bando lile likatike na lisiishe.

Mimi leo nimeshuhudia kwenye simu yangu, nilikuwa nimeweka bando lakini limeisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna changamoto nyingine, unaweka bando mwezi mmoja kabla ya mwezi unaambiwa limekwisha lakini ukiangalia matumizi hayakuwa katika kiwango hicho; hili ni jambo ambalo linatakiwa pia liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, sisi watu wa Itigi tunachangamoto sana ya usikivu wa Redio. Watu wetu ni wananchi wa daraja la chini, wananchi ambao wanatumia Redio, *TV* mpaka wawe na madishi na *TV* yenyewe ni vitu vya gharama. Redio shilingi elfu 10 mtu anapata habari anaisikiliza dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika ukurasa wa 125, kwamba umeiweka Manyoni, mnaenda kuongeza usikuvu wa Redio. Lakini changamoto kubwa Mheshimiwa Waziri ipo Itigi, siyo Manyoni. Kwa hiyo muangalie ni namna gani watu wa Itigi wanapata mawasiliano ya Redio. Pale kuna Redio imeweka mtambo wake sitaki kuitaja kwa sababu ndio tunayosikiliza. Sasa mnapoenda kufunga mhakikishe watu wa Itigi wanapata mawasiliano ya Redio ya *TBC* Redio yao ya Taifa, wamskie Mheshimiwa Rais wao anapohutubia Taifa kupitia redio yake ndogo, redio ya mkulima. Sisi kwetu kule wakulima ndio wengi. Kwa hiyo ninaomba sana hili jambo liharakishwe ili wananchi waweze kupata mawasiliano. Iko ahadi yako Mheshimiwa Nape, uliahidi hapa katika Bunge hili, kwamba mtakwenda kuanzisha Chuo cha Teknolojia ya Habari sijui mmefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja basi utuambie Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Jamhuri ya Muungano, vijana wetu. Dunia inahama kutoka kwenye elimu ile ya kizamani; hata hizi *VETA* zilizopo sasa zinapitwa na wakati. Sasa ninyi mtakapokuja na Chuo hiki cha Teknolojia ya Habari mtaisaidia Tanzania kwenda na upepo ambao upo duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Zuena Bushiri, jiandae Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuifungua Tanzania kwa njia ya mawasiliano. Nimpongeze Waziri Mkuu, nimpongeze Waziri Nape, nimpongeze Waziri Kundo pamoja na watendaji wote wa sekta hii ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nitachangia kuhusu usikivu wa redio ya *TBC* katika maeneo ya mipakani, ukosefu wa mawasiliano katika maeneo ya mipakani pamoja na Hifadhi ya Mkomazi ambayo jina lake maarufu kwa kule kwetu inaitwa Kambi ya Simba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuhusu ukosefu wa mawasiliano ya redio ya Taifa *(TBC)*. Katika Mkoa wa Kilimanjaro maeneo ya mipakani hatuna usikivu kabisa wa redio yetu, mara nyingi ukifungua redio unasikiliza redio za kenya kitu ambacho Watanzania wanakosa kupata Habari ya nchi yao. Jambo hili tumekuwa tukiliongea, mimi binafsi nimeliongelea sana hapa katika Bunge hili lakini hata leo hii katika Mkoa wa Kilimanjaro maeneo ya Rombo, Vijiji vya Kikererwa na vijiji vingine jirani ambavyo viko mpakani hawasikii kabisa redio yetu ya *TBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali, katika minara hii ifanye jitihada ya kupeleka minara hiyo katika maeneo hayo ili na sisi Watanzania tujivunie shirika letu la mawasiliano jinsi linavyofanya kazi kuliko tukikaa kule tunasikiliza redio za wenzetu hatupati habari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi tena katika mawasiliano maeneo hayohayo. *Safaricom* imekuwa ikitawala sana maeneo

haya, kiasi kwamba hata mtu akiwa yuko kule kijijini hawezi kupata mawasiliano ya Vodacom, Tigo na kampuni nyingine za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme walinzi wakubwa wa mipakani ni wananchi wanaoishi kule. Kwa hiyo kwa kukosa mawasiloiano kwao tunakosa hata kupata taarifa mapema pale ambapo panakuwa na changamoto yoyote katika maeneo ya mipakani. Niiombe Serikali katika minara hii 758 wahakikishe sasa kwamba maeneo yote ya mipakani yanapata minara ili Watanzania na sisi tuweze kupata huduma stahiki ya mawasiliano katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika maeneo ya Hifadhi ya Mkomazi. Nimesimama hapa Bungeni zaidi ya mara mbili nikiongelea changamoto ya mawasiliano katika Hifadhi ya Mkomazi. Hifadhi ile inawanyama wakali, hifadhi imetokea kuwa na changamoto nyingi za wananchi kuporwa mali zao, hifadhi ile hata Askari wa Wanyamapori maeneo yale walituomba sisi kama Kamati tusaidie ili waweze kupata mawasiliano kwa kuwa inaweza ikatokea changamoto yoyote ndani ya hifadhi lakini hawana mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali yangu sikivu Serikali ya Chama Cha Mapinduzi; Mheshimiwa Rais ameshuhudia utiaji saini wa minara 758. Katika minara hiyo niiombe sana Serikali iangalie maeneo ya hifadhi kwa kuwa kule ndani ya hifadhi kunakuwa na changamoto nyingi. Inaweza ikatokea hata Wanyama wakali lakini utoaji wa taarifa ukawa ni hafifu sana hivyo niombe katika minara hiyo 758 serikali itupe jicho katika Hifadhi ya Mkomazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nichangie kuhusu suala la wizi wa mitandaoni. Ni ukweli kwamba vijana wengi wanatumia kuibia wananchi katika mitandao unaweza ukafungua simu ukaambiwa nitumie pesa kwa namba hii hii jina litatoka fulani fulani fulani. Mheshimiwa Nape nakuamini Waziri wangu, Mheshimiwa Kundo nakuamini Waziri wangu, ninyi ni vijana mmepewa hii Wizara kwa kuwa ni vijana ambao ni wachapakazi

hakikisheni kwamba kazi hii wanayoifanya matapeli wanataka kuwazidi akili. Msikubali kabisa hali hii ya wizi wa kutumia simu nchini Tanzania ukaendelea, udhibitini. Naamini mnao uwezo wa kufanya hivyo ili wananchi waweze kuishi vizuri na kuona kwamba wizi huu umetokomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi naungamkono hoja, lakini nitaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa uwaeleze Watanzania hasa wa Mkoa wa Kilimanjaro…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI: …**ni lini wataondokana na adha ya kusikiliza *safari com* badala ya Vodacom na mitandao mingine ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa unatumia muda wa watu wengine, Mheshimiwa Sichalwe, ajiandae Mheshimiwa Amandus Julius, jiandae Mheshimiwa Butondo.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, niishukuru Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo yote ambayo amefanya kwenye Wizara hii lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja na timu nzima kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Niipongeze na kuishukuru Serikali kwa baadhi ya minara ambayo tumepata ndani ya Jimbo la Momba kwenye Kata za Chululumo, Msangano, Nzoka na sehemu zingine. Tunaomba kueneelea kuboreshewa minara kwenye Kata za Kapelle, Tungwa, Mkomba lakini pamoja na Kata ya Chitete ikiwa ni sambamba na kuhakikisha mnatuchepushia Mkongo wa Taifa kufika makao makuu Chetete.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kidogo niku-*challenge* Mheshimiwa Waziri *in very positive way*. Kwenye zile ajira ambazo ziko kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi wewe ndiye mtu kwenye Wizara hii umebeba ajira nyingi sana za vijana kama ukiamua tu ukiamua kutumia teknolojia *in very positive way*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Juzi wakati nachangia kwenye Wizara ya Profesa Mkenda ambaye Wizara yake ni Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia lakini Wizara yako ni Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tukaomba tungepata Wizara mpya ya Teknolojia ili tuweze kuendana na karne ya 21 ili tuweze kuendana na *Fourth Industrial Revolution* Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna namna tunaweza tukakwepa jambo hili ndiko wakati unakotupeleka lakini nishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi nataka kurejea; kwenye ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwenye sura ya nne ambayo inasema sayansi na teknolojia na ubunifu kwenye ukurasa wa 154.

Ilani yetu ambayo tuliinadi, inasema hivi "Chama cha Mapinduzi kinatambua kuwa uchumi wa kidijitali ni muhimu katika kuleta maendeleo kwa kuongeza ufanisi katika uzalishaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali na kutoa fursa za kuongeza vipato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Uchumi huo umeonekana kuwa eneo muhimu katika kuchangia kukuza uchumi nchini kama ilivyofanyika katika nchi zingine za kipato cha kati. Aidha, uchumi wa kidijitali unalandana na mapinduzi ya nne ya viwanda yaani maana yake fourth industrial revolution yanayokuja na ambayo hayaepukiki. Hivyo basi, CCM itaendelea kusimamia Serikali kuhakikisha kuwa teknolojia mpya za kidijitali zinatumika kuongeza ufanisi katika sekta za uzalishaji na kuepuka madhara yanayoweza kutokea. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo Chama cha Mapinduzi kinaelekeza yafuatayo:-"

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo manne, lakini naomba niende kwenye jambo moja la muhimu. Kuimarisha kituo cha utafiti hapa Mheshimiwa Waziri amekwama; kuimarisha kituo cha utafiti, ubunifu na uendelezaji wa TEHAMA ikiwemo kujenga

uwezo wa kuongeza matumizi ya teknolojia mpya za kidijitali na *artificial intelligence*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko msanii wa Mheshimiwa Waziri pale Diamond, muulize ameshapeleka kazi zake kwenye *NFT*, bado. Vyote hivyo ni vitu vya muhimu. Ni msanii wetu ilibidi tulinde kazi zake *NFT* kazi zake ziende hapo ambapo kazi zake zisije kupata huko madhara. *Block chain technology* kwa *research* ndogo ambayo nimefanya hapa kwetu Tanzania kwa mambo madogo ambayo nimefuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano unamuuliza mtu unajua nini kuhusiana na *block chain technology*, unajua nini kuhusiana na *digital currencies*, unajua nini kuhusiana na *crypto currencies*. Mtu anakuuliza kwa hiyo Mheshimiwa nikitaka kujiunga kwenye *Bitcoin* nafanyaje? Yaani swali hili *does not make sense,* yaani ni sawa mtu ananiuliza kwamba Mheshimiwa Mbunge najiungaje kwenye *T-shilling*? Yaani mtu anajiungaje kwenye *T-shilling* yaani *Tanzania shilling* hela yetu mtu anajiungaje? *Digital currencies, block chain technology* ni teknolojia kubwa sana ambayo Chama Cha Mapinduzi kwenye Ilani yetu imesema, tuboreshe Kitengo cha Utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi akiwa kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwenye Wizara hii, nilishawahi kumfuata sana kuhusiana na mambo ya *PayPal* kila wakati nilikuwa nachangia. Akaniambia tunaendelea kufuatilia dada, tunafuatilia tunaongea na watu wa *BOT*. Siku moja nikamwona tena kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile amekuja hapa anauliza mambo ya *PayPal*. Sasa nikashangaa huyu tena kaka yangu alikuwa ni Waziri, sasa tena amekuja kuuliza. Kwa hiyo unaweza ukaona utafiti huo Mheshimiwa Waziri angekua ametusaidia, amekaa vizuri na watu wa *BOT*. Tunatamani kuona teknolojia tunazozipata zisiende tofauti na kazi zetu ambazo tunazifanya na taratibu ambazo tumejiwekea kwenye nchi yetu, lakini tayari kama kungekuwa na utafiti tungejua namna ya ku-*accept PayPal* kama ni njia ya kulipa na kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi huko nje watu wetu hapa Tanzania wanalipa kwa *PayPa,l* hela zao zinapitia Kenya zinaishia huko, *why not us?* Yaani nini ambacho Kenya wanatuzidi ambacho sisi hatuna ambacho hatuwezi ku-*adapt*, nini ambacho *South Africans they have* sisi hatuwezi ku-*adapt* tukawa nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mdogo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, *block chain technology* si teknolojia ya kuidharau, ni teknolojia ambayo ina mawanda mapana. Huko ndani kuna watu wa mambo ya sheria, mambo ya *smart contract*, huko ndani kuna mambo ya watu ambayo yanahusiana na mambo ya ardhi kuna vitu vingi. Huko ndani kuna mambo ya *NFT* ambayo ni mambo ya wasanii kwa ujumla na hata waigizaji wetu, yaani viko vitu vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri kiamua tu kuikumbatia *block chain technology* vizuri kwa lengo zuri, bila kuathiri mila na desturi zetu. Ndio namwambia Mheshimiwa Waziri inaweza ikawa ni Wizara ya mfano ambayo itatoa ajira nyingi sana ambayo imeandikwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Wapo maprofesa kadhaa kwenye nchi hii ambao wameandika maandiko kuhusiana na *block chain technology*. Kwa nini tusimwombe akae nao, lengo tunataka jamii ijue, mara nyingi wananchi wamechukulia hivi. Kwa mfano kuna siku moja kuna mtu akawa ananiuliza *block chain technology* ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaona anafananisha, ni kama mtu umwambie mtoto mdogo unataka kuwa mwanasiasa? Aseme hapana, mimi sitaki, mambo ya kutukanana kwenye mikutano, mimi sitaki kuwa mwanasiasa, lakini siasa sio hivyo, siasa ndio tuko hapa sisi Wabunge tumekutana. Sisi ni wanasiasa, kwenye siasa ndiyo tunampata Mheshimiwa Rasi, kwenye siasa ndio tunampata Spika wa Bunge, kwenye siasa ndio tunampata Mheshimiwa Zungu, kwenye siasa ndio tunapata Baraza la Mawaziri, kwenye siasa hapa ndani tulipo Bunge ndio tunapitisha bajeti, ndio tunatunga sheria, ndio tunatetea mambo ya wananchi. Kwa hiyo yule mtu ameingolea siasa kwenye ka-*negativity* kadogo yaani tone yaani *drop of water* kwenye bahari, ndio ameongelea siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mtu anaposema *Bitcoin* ni wizi, sijui ni *pyramid* yaani ni kama mtu aseme mimi sitaki *internet* kwa sababu wanaonyesha *pornography*. Si sawa, *internet* inafanya vitu vingapi? Hayo ni madhara madogo ambayo yanatokana na kuwepo kwa *internet*. Kwa kuwepo kwa *block chain technology,* ni teknolojia ambayo lazima itaambatana na *challenges* nyingi tu ambazo hatuwezi kuziepuka, lakini unapoongelea *block chain technology* na vitu viliko ndani yake ni jambo kubwa, ni jitu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aende basi hata kukaa na timu yake, apitie hata vitu vichache tu mambo ya *coin market,* yaani aingie tu hata kwenye ile *website*, *coin market cup*. Aangalie pale, zile *currencies* zote, hivi kweli watu wote wale wanaweza wakawa ni wajinga wamekaa. Mheshimiwa Waziri atamani hata kumfahamu *who is* Santos Nakamoto. Huko tunapoenda Biblia yenyewe imeandika hakuna namna tutakavyokwepa kuja na *one currency. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiko huko tunakoenda hakuna namna benki zitakwepa hilo jambo ndiko tunakoenda. Kizazi chetu ndio hiki hiki Waziri anavyotuona, miaka 20 ijayo ndio tutapata Rais hapo, ndio tutapata Waziri Mkuu hapo ndio tutapata viongozi wakubwa hapo. Kwa hiyo, hiki tunachokishauri muda huu hatutamani kupitwa. Hebu aangalie sasa hivi tulivyopokea *internet*, angalia *internet* ambavyo inatusumbua. Tulichelewa kutunga sheria ambazo zitafanana na wakati tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu kwenye mitandao ya kijamii wanaweza wakamtukana hata Mheshimiwa Rais, hatujawahi kuona hata mahali wanashtakiwa kwamba walimtukana na wapo, wana *challenge*. Tunaona watu wanatukana viongozi mbalimbali matusi mengine makubwa. Tunaona watu wanaandika vitu vya ajabu, wanaposti vitu vya ajabu ambavyo viko nje na utaratibu na mila na desturi zetu, lakini hatuna sheria ambazo zinawabana kwa sababu tuliacha *internet* ikatutangulia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** … kuliko sisi. Kwa hiyo nimwomba Mheshimiwa Waziri aboreshe utafiti kama ambavyo Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inasema na kama itawapendeza kama Serikali …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia sekunde, ahsante sana muda wako umekwisha.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mengine unaweza ukamwandikia inaruhusiwa.

Mheshimiwa Amandus Julius atafuatiwa na Mheshimiwa Butondo na Mheshimiwa Neema Lugangira, ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na hatimaye kupata nafasi ya kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli ameendelea kufanya mambo makubwa kwenye nchi yetu, ameendelea kuifungua Tanzania lakini kwa mkataba huo tulioshuhudia wa utiaji saini, ujenzi wa minara zaidi ya 700 ni kielelezo tosha kwamba Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri isiyo na mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Habari kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake wote. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara hii ndio *coordinator* wa Wizara zingine. Wizara hii ikifanya vizuri wote tunakubaliana kwamba mawasiliano kwa sasa ndio habari ya dunia. Habari ya TEHAMA kwa sasa ni habari ya dunia,

Mheshimiwa Waziri Nape anafanya kazi nzuri, anafanya kazi nzuri na kwa kweli tunajivunia namna ambavyo Tanzania inakwenda kidijitali, hakuna mfano. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumpa taarifa mchangiaji anachangia vizuri sana kuisifia na kuwasifia Waziri na Naibu Waziri na kwa ushahidi tu ni kwamba Jimbo la Kilolo limepata minara tisa na kata tisa ambazo hazikuwa na minara zote sasa zinaenda kuwa na mawasiliano. Kwa hiyo sifa anazozitoa ninao ushahidi na nimependa kumpa taarifa ili aelewe kwamba hakosei. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Amandus taarifa hiyo.

**MHE. AMANDUS J. CHINGULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo naipokea kwa sababu ndio hali halisi iliyoko kwenye maeneo yote ya Tanzania kwa sasa. Kwa kweli tukipongeza kitu ambacho kiko wazi kila mmoja anakubaliana na sisi na ndio maana hata michango ya leo ya Waheshimiwa Wabunge imekuwa ni ya kidijitali kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesoma hapa na mimi nitajitahidi kutumia dakika chache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana umefika Nachingwea, wakati wa kampeni ulikuja kufanya kampeni kule Nachingwea na nakushukuru sana. Yako maeneo kwenye Jimbo la Nachingwea ukifika unazima simu kwa sababu haina kazi tena, inakuwa ni kama kopo. Baada ya hapo maana yake ni kwamba kuna maeneo ambayo sasa hayo ndiyo unaweza ukatumia simu. Sasa nishukuru kwanza Serikali na nimshukuru Mheshimiwa Waziri nimeona hapa kwenye ukurasa wa 100, nimeona minara inakuja Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na shukrani hizo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, jiografia ya Nachingwea ni

kubwa, nimwombe kwa heshima na unyeyekevu mkubwa atuongezee minara Nachingwea, tuongezewe minara ya Nachingwea. Mji wa Nachingwea kwa namna ulivyo jiografia yake Waziri anafahamu, misitu ni mingi na mbuga kule Selous anajua ipo. Kwa hiyo ukienda katika baadhi ya maeneo, kwa sababu ya miti na maeneo yale kuwa na mbuga hii ya Selous, unakosa mawasiliano kwa namna ya jiografia ya wilaya yenyewe ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema kwamba nitazungumza kwa ufupi sana. Mheshimiwa Waziri aendelee kuchapa kazi, aendelee kuchapa kazi. Sisi tupo na tunaona kazi inayoendelea na kwa kweli hata suala la utapeli wa kwenye mitandao, niwaombe tu hao ndugu kama wapo na wanasikia, watafute shughuli zingine za kufanya. Kwa namna spidi ya Wizara hii inavyoendelea ni imani yangu kwamba muda si mrefu hao nao wanakwenda kufa. Sasa ili wasife kifo kibaya cha kutangazwa kwenye mitandao, wakati ni huu wa kujisalimisha kuacha shughuli hiyo na kutafuta shughuli nyingine halali ambayo itawapatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Butondo, wajiandae Mheshimiw Lugangira na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. BONIPHANCE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa. Kwanza naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Rais ameendelea kuchanja mbuga kuhakikisha kwamba shughuli za kimaendeleo katika sekta zote zinakwenda kwa kasi kubwa na tumeshuhudia juzi zoezi la kusaini mikataba ya ujenzi wa minara na sisi Wabunge tumeshiriki na wadau wengine. Kwa kweli shughuli ile Watanzania wote wameiona kwa macho na ina kwenda kuongeza kasi ya upatikanaji wa mawasiliano katika Taifa letu la Tanzania kwa

ujumla. Kwa hiyo tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa anazozifanya katika sekta hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Nape, Waziri pamoja na Naibu Mheshimiwa Kundo …

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. BONIPHANCE N. BUTONDO:**…kwa jinsi ambavyo wameendelea kushiriki pakubwa sana kuhakikisha kwamba…

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja …

**NAIBU SPIKA:** Husikiki, *microphone* yako imekaa vibaya. *Mic* yako ina nini ina *glitch?*

*(Hapa kipaza sauti hakikufanya kazi)*

**MHE BONIPHANCE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshindwa kumsikia vizuri, lakini kwa ajili ya kulinda muda, naomba kulinda muda wangu, lakini kimsingi naamini atakuwa anazungumzia suala la muhimu sana la mawasiliano hasa katika Jimbo lake la Igalula na mimi ni mdau wa shughuli za maendeleo katika Jimbo la Igalula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba pia niwashukuru watendaji wote katika Wizara hii kwa namna ambavyo wanafanya kazi zao vizuri. Sasa la pili nataka nizungumzie suala zima la minara; tumeshuhudia utiaji wa sahihi wa ujenzi wa minara 758, lakini 304 ambayo inaenda kuongezewa nguvu. Zoezi hili muhimu linaenda kuleta tija na kuharakisha shughuli za kimaendeleo kwa ujumla katika Taifa letu. Suala la

mawasiliano ambalo lilikuwa linahangaisha hasa katika Jimbo la Kishapu, tunakwenda kunufaika pa kubwa sana kutokana na zoezi hili la kusaini mikataba ambalo limefanyika hivi karibuni. Katika hili narudia kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini tunakubaliana wote kwamba Sekta hii ya Mawasiliano ndiyo chachu kubwa ya maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie katika maeneo haya ambayo yanaenda kunufaika na suala zima la minara hii. Mimi naenda kupata jumla ya vijiji 17 ambavyo vinaenda kupata manufaa na minara hii na minara hii iko minara 11. Hii ni pamoja na Busangwa mnara mmoja, Itilima ambayo ina Ikoma, Ileberebe na Mwajiginya *B,* lakini kuna Masanga pale panaitwa Dodoma, lakini kuna Mwakipoye Iboje na Mwakipoya yenyewe lakini pia na Shagihilo ambapo kuna Kijiji cha Mangu lakini kuna Mwamalasa ambapo Magalata wanaenda mnara, lakini Talaga ambayo ina Jijongo na Nendeghese inapata mnara. Pia maeneo haya yatakwenda kusaidia vijiji vyote jirani kupata mawasiliano kwa urahisi. Kwa hili namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kundo kwa sababu alifanya ziara katika Jimbo langu na haya maeneo aliweza kuyabaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumwomba Waziri kwamba, maeneo ya Kata ya Seke Bugoro, Somagedi, Mwasubi na Bunambiu bado yana changamoto ya mawasiliano. Niombe sana katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao, waweze kufanya *consideration* katika maeneo haya na yenyewe yaweze kupata mawasiliano kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie hapa ni suala zima la redio yetu ya *TBC*. Jukumu la *TBC* na hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kabisa wazi, ya kwanza ni kuhakikisha kwamba tunaielimisha jamii, kuihabarisha jamii lakini kuiburudisha jamii lakini na kuitafakarisha kwa kuzingatia kauli mbiu ya ukweli na uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kauli mbiu hii ya Ukweli na Uhakika lakini ikiwa ni pamoja na kuhabarisha, kuelimisha lakini na kuburudisha, bila mawasiliano ya uhakika ama bila usikivu wa

uhakika, Watanzania wengi wanakosa mambo haya ya muhimu. Kwa hiyo naomba sana katika Jimbo la Kishapu maeneo makubwa sana Redio *TBC* haisikiki kabisa katika maeneo hayo. Niombe sana hili jambo liweze kufanyiwa kazi ili mradi wananchi wangu waweze kunufaika na redio hii muhimu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tumeona kabisa katika mwaka wa fedha 2022/2023, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba redio hii inasaidiwa na inakuwa na uwezo mkubwa wa kuhabarisha na kutoa taarifa zake, zilikuwa ni zaidi ya 13,133,000,000 lakini pesa ambazo ziliweza kupokelewa pekee yake zilikuwa ni bilioni 3.9 ambayo ni kama asilimia 30, unaweza ukaona kwamba ni fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha kwamba redio hii katika kila tengo la fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba redio hii inapata ufanisi, umuhimu huu tuuone kwa sababu wananchi wetu wanaenda kunufaika pakubwa sana sana. kwa hiyo nataka niiombe sana na niirai sana Serikali katika eneo la bajeti, utekelezaji wa upelekaji wa fedha zinakuwa zinatengwa katika kila mwaka wa fedha, ziwe zinapelekwa kwa asilimia 100 ili Mheshimiwa Nape, Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake sasa waweze kuona ufanisi na mafanikio ya bajeti inayotengwa katika kila kipindi cha mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la uandishi wa habari, waandishi wa habari wengi sana jamani wamekuwa wana shida, huwezi ukasema ni omba omba japokuwa lugha ile sio nzuri. Tabu kubwa ni mikataba kwa watumishi hawa. Waandishi wa Habari hawana mikataba, wamekuwa wana shida kweli. Maisha yao kama si sisi wanapokuwa kwenye majukumu hayo kutowajali na kuwapa chochote, wanaishi maisha ya tabu sana. Tunaomba hawa Waandishi wa Habari kwa sababu Waziri ni baba na mlezi, awatazame na kuhakikisha anawalea na kuhakikisha kwamba waajiri hawa wana mikataba. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la msingi ambalo nataka nilizungumzie…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo kengele ya pili, malizia sekunde mbili.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ooh! Ninaunga mkono hoja, napongeza sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, ajiandae Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa MNami napenda kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anafanya mageuzi makubwa ya teknolojia na maendeleo ya kidijitali hapa nchini kwetu, ikiwemo pia kuhakikisha kwamba Serikali inaboresha namna ambavyo inafanya kazi kwa kutumia TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Nape Nnauye na Viongozi wote wa Wizara hii kwa mageuzi makubwa ambayo anaendeleea kuleta katika sekta hii muhimu. Kipekee ningependa pia kumpongeza sana Dada yangu Justina Mkurugenzi Mtendaji wa *UCSAF* kwa kazi kubwa ambayo anafanya, siyo tu ya kupeleka minara lakini ya kuhakikisha ya kwamba shule zetu zinaunganishwa na mtandao ili watoto wetu waanze kukua kupata elimu ya kidijitali na stadi zingine tokea wakiwa kwenye umri mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo awali kulikuwa hakuna Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na badala yake masuala yote yanayohusiana na TEHAMA yalikuwa

yamegawanywa ama yametapakaa sehemu mbalimbali kwa maana ya Serikali, taasisi na maeneo mengine ya Serikali. Kwa utashi wa Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan mwaka 2021 aliamua kuunda Wizara hii mahsusi ambayo itakuwa na mamlaka na dhamana ya kusimamia na kuunganisha na kuratibu masuala yote yanayohusu na TEHAMA na ninampongeza sana Mheshimiwa Rasi kwa jambo hilo kwa sababu limeongeza tija ambayo wengi wetu tunaisifia hapa leo Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya badiliko hilo, moja ya vitu ambavyo vilifanyika ni kuhamisha *Data Center* ambayo ilikuwa iko chini ya Ofisi ya Rais na ikahamishiwa ikaletwa kwenye Wizara hii. Lengo zima ni kutimiza lengo la Serikali kuwa na sehemu moja ya kukusanya *data* na ilionekana kwa kuwa sasa tuna Wizara hii mahsusi, basi jukumu hilo liletwe kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika mchango wangu wa siku ya leo nitajikita katika *e-GA (E-government Agency)*. *E-government Agency* hivi sasa iko chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi na ninatambua kwamba chini ya *e-GA* kuna sehemu mbili. Sehemu moja ni *platform,* sehemu nyingine ni masuala ya utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupendekeza ya kwamba suala la utumishi libaki kwenye Ofisi ya Rais, Utumishi lakini suala la *e-GA platform* lihamishwe liletwe kwenye Wizara hii ambayo ndiyo ina dhamana na mamlaka ya usimamizi wa masuala yote ya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu hivi sasa ijapokuwa tunayo *e-GA* lakini kutokana na pale ambapo ipo, hivi sasa kuna mifumo mingi ambayo haisomani. Nitatoa mfano mdogo, Walimu wetu ambao wako chini ya TAMISEMI wanatumia mifano mingi kuingiza taarifa na mifano hiyo haisomani.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu tukija kwenye sekta ya afya. Leo hii mimi naweza kufanya kipimo cha *CT scan* Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa hapa Dodoma lakini nikilazimika kufanya *CT scan* Muhimbili Dar es Salaam, inabidi nifanye *CT scan* tena

kwa sababu mifumo haisomani na viko vipimo hivi vya afya ambavyo huruhusiwi kufanya mara kwa mara.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba tumepongeza maeneo mengi yamepata minara lakini kwa masikitiko makubwa kwa Wilaya ya Nyang'hwale hakuna mnara hata mmoja na taarifa tulizileta kwamba kuna tatizo la usikivu. Kwa hiyo, nataka nikupe taarifa kwamba tunapongeza lakini Wananyang'hwale tuna masikitiko makubwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar umesimama hiyo ndiyo hoja aliyokuwa anazungumza Mbunge kweli? Mheshimiwa endelea.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba utanilindia muda wangu. Kama nilivyokuwa nasema kuna umuhimu mkubwa wa mifumo hii kusomana kwa sababu pasipo kusomana inawaongezea gharama kubwa sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hapa kwenye eneo hili, *digital competitiveness* ya nchi yaani ushindani wa kidijitali wa nchi unapimwa kutokana na ushiriki wa *startups* kwa maana ya sekta binafsi. Kwa kuwa *e-GA* iko chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi, *e-GA* wanafanya mifumo yote wenyewe, hawashirikishi hata kidogo sekta binafsi wala *startups* zetu, wakati hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ninampongeza sana nimefarijika kusikia lengo la Wizara ni kuona namna gani ambavyo tutaimarisha *startups* zetu ili nasi tuweze kufika mahali *startups* zetu ziweze kuuza nje ya nchi teknolojia yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunasifika kwa mfumo wa *GePG (Government Procurement)* na mfumo wa *BRT* (Mabasi ya Mwendokasi) lakini nchi zinakuja kujifunza hapa kwetu,

kitakachokuja kutokea sasa ni nchi hizi zitajifunza kwetu, zitapeleka haya kwenye sekta binafsi yao, wale watatengeneza halafu wale watauza watanufaika kwa kile ambacho kilanzia kwetu. Hili jambo lazima tuliangalie kwa jicho la kipekee na kwa wivu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka nitatoa mfano mdogo wa nchi kama Estonia. Nchi ya Estonia ina watu milioni 1.3 tu lakini inasifika katika *startups* zao kuja na teknolojia ambazo zimeweza kuvuka mipaka. Wana *startups* 10 na hizi *startups* 10 peke yake zina thamani ya zaidi ya Dola bilioni moja. Hiyo ndiyo dhana nzima ya kuwa na masuala haya ya *e-GA* na masuala ya ubunifu kwenye Wizara ya TEHAMA. Kwa hiyo, mimi naendelea kusisitiza kwamba Serikali ione namna ya kuhamisha masuala ya *e-GA* kutoka ilipo na yaje kwenye Wizara hii ya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu hivyo, kwa kuwa *e-GA* inafanya biashara peke yake inaiongezea gharama kubwa sana Serikali. Nitatoa mfano mdogo uko Mfumo wa *TANePS*. Huu mfumo umetumia takriban zaidi ya shilingi bilioni sita na bado haujakamilika. Huu mfumo ungepewa kwenye sekta binafsi ingetumika takribani chini hata ya shilingi bilioni moja na mfumo ungekuwa umeshakamilika. Kwa hiyo mimi ambacho ningependa kumuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake anipe kauli na maoni na mipango ya Serikali, kwa kuwa sasa tunayo Wizara mahususi, Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia na Habari atuambie nini mpango wa Serikali katika kuhamisha suala la *e-GA* kwa upande wa *platform* litoke Ofisi ya Rais, Utumishi na lije kwenye Wizara hii mahsusi ili tuweze kupata tija lengwa na tuweze kuimarisha ushindani wetu wa kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bulaya, ajiandae Mheshimiwa Ndulane, ajiandae Mheshimiwa Mussa Omar Salim.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami kwa moyo safi tu kwanza

nitambue kwamba sasa hivi walau wanahabari mwanga tunauona, tumepumua kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanza kufanya kazi kwa uhuru, tunahitaji uhuru zaidi na hili Mheshimiwa Nape umelifanyia kazi, hongera sana Kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine wadau wa habari wanajua kuna mchakato wa Marekebisho ya Sheria ya Habari wanaomba usiende haraka kwenye Bunge hili. Wanaomba waweze kupata nafasi ya kutoa maoni. Wameomba sana na wanajua wewe ni msikivu, hili utalisikiliza ingawa lengo lao ilikuwa sheria mpya lakini kwa sababu kuna *amendment* kuna mabadiliko ya sheria wanaomba wapate muda wa kutosha kama wadau kuja kutoa maoni yao kwenye Kamati ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitambue kazi nzuri inayofanywa na vyombo vya habari na ubunifu pia kwa baadhi ya *TV* na redio ikiongozwa pale na mdogo wangu *Diamond* (Wasafi) wanafanya kazi nzuri kupitia kipindi chao cha *Good Morning*, kipindi cha Michezo lakini *Global Online* kipindi cha *front page* wanafanya vizuri, kuna kipindi cha *TV* cha *360 Clouds,* Jahazi na *Amplifier* kinachoongozwa na Millard Ayo. Tunasema hayo kwa ajili ya kuwapa fursa wengine waweze kufanya vizuri zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua uwekezaji wa Azam *TV* wa kidijitali. Pale imeanguka siyo chini ya shilingi bilioni 15 na tunatamani *Television* yetu ya Taifa ifikie huko. Tunahitaji *Television* ya Taifa ifikie hadhi ya *Al Jazeera*, *CNN, BBC* haya yote yanawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nape unajua mimi ni Mwandishi wa Habari, nimekaa *Newsroom* nilianza kama Mwandishi wa Habari Mwanafunzi mpaka Mwandamizi, ninajua changamoto za wenzangu. Asilimia 90 ya Waandishi wa Habari hawalipwi. Hao asilimia 90 ni kwenye *private sector,* hawalipwi na wameshazoea hiyo hali na hawana mtetezi. Mheshimiwa Nape usikubali wewe kama Waandishi ambavyo wana imani na wewe

na umewapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya, huu Muhimili usionekane tu upo upo, upewe heshima yake. Waandishi wapewe hadhi yao kwa kazi kubwa wanayoifanya kuwahabarisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mwandishi ategemee *source* kumpa chochote, siyo kwamba anapenda, Mwandishi anatakiwa alipwe na chombo chake vizuri. Akiamua kufanya *investigation story* kwa maslahi ya nchi awe na uwezo huo, asiwe mnyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nape kuna Vyombo vya Habari miaka 10 hailipi Waandishi, miaka 11 hailipi Waandishi. Kuna chombo kinadaiwa shilingi bilioni 3.5 na Waandishi. Zaidi ya miaka 10 Waandishi hawajalipwa, wafanyakazi zaidi ya 195 ambayo ni Sahara *Media. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waandishi wengine wanadai vyombo vyao shilingi milioni 100, milioni 200, milioni 300 hawalipwi lakini wapo huwasikii wakinung'unika. Wapo humu wanatuandika, wapo humu wanapeleka ujumbe kwa Watanzania nchi yao inafanya nini, kwa kinyongo lakini hawawezi kukaa nyumbani wana familia lazima watoke wakafanye kazi labda huko wataonana na watu wenye nia njema. Hii kazi siyo ya kujitolea, hii ni kazi kama Wakili, hii ni kazi kama Daktari, hii ni kazi kama Mwalimu. Wanahitaji wapate malipo yao Waandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nape hata michango kwa wale ambao wanapata mshahara kidogo haiendi kwenye mifuko. Hivi hatma yao hawa Waandishi baada ya kazi iweje? *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Napenda kumpa taarifa Dada yangu mzungumzaji kwamba anayoyazungumza ni mambo ya

msingi kweli na tunajua jinsi gani Waandishi wa Habari wanavyopata taabu. Kwa hiyo nimuongezee tu siyo vibaya vilevile katika mchango wake kama ataihitaji Wizara iweze kupitia mikataba yote ya Waandishi wa Habari ili waweze kupata stahiki zao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa yake na wewe unajua Waandishi wanavyopata taabu. Hata hao ambao wanafanya, yaani kuna kampuni Waandishi wameamua tu kufanya kazi bure. Hawana mikataba Mheshimiwa Nape, hawalipwi, michango yao haiendi. Mbali na ugumu wa maisha wanayopata sasa hivi, hatma yao baada ya kustaafu hawaijui. Mheshimiwa Nape nikasema hivi Serikali na yenyewe kwenye hili inachangiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nape kazi ya umiliki wa vyombo vya habari haitegemei mauzo kwenye magazeti, haitegemei labda tu *TV* au redio kutangaza. Vyombo vya Habari *survival* yake ni matangazo. Leo Serikali ukichanganya Vyombo vya Habari vya *private sector* na hivi vya umma mnadaiwa karibia shilingi bilioni 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapewa huduma ya matangazo, hamlipi. Sasa huyu tu kwa mfano Sahara *Media* ambaye anadaiwa na watumishi wake zaidi shilingi bilioni tatu anasema anawadai Serikali shilingi bilioni sita. Tukija *Daily News* peke yake Serikali mnadaiwa shilingi bilioni 11. Hapo sijazungumzia redio na mpaka huko kwenye *level* za Wilaya na Mikoa. Sasa kwa nini hamuwalipi matangazo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli unawezaje sasa ukaanza oparesheni ya kutaka Waandishi walipwe kama Serikali hamuwalipi Vyombo vya Habari matangazo? Inabidi muonyeshe mfano. Wamewapa huduma ya matangazo, wamewarushia *live* lazima muwalipe ili na ninyi mpate sasa nguvu ya kwenda kufanya oparesheni ya *media* ambazo hazilipi Waandishi wa Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nape hilo unaliweza na Waandishi wana imani na wewe, ulikuwa radhi ku-*sacrifice* nafasi yako kwa ajili ya kulinda heshima ya Vyombo vya Habari. Nikuombe nenda kaanze msako wa kutetea Waandishi wa Habari wawe na mikataba, Waandishi wa Habari walipwe, michango yao iende vilevile hakikisha mnawalipa Waandishi, na vyombo vya habari vya binafsi na Serikali. Hapo *TBC* nilikuwa sijaitaja kabisa lakini ninataka majibu kwa nini sasa hivi kwenye bajeti ya maendeleo imepungua kwa asilimia 28? Hilo nitataka majibu, tulitarajia bajeti iongezeke zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hapa tunasifia uwekezaji wa *Azam private,* huku kuhakikisha *TBC* inakuwa na usikivu bajeti yao shilingi bilioni 13 ili waweze kukamilisha huo mradi zimetoka shilingi bilioni tatu. Kweli tutaweza ku-*compete* na watu ambao wanakuja sasa hivi ili hii Redio yetu ya Taifa, *Television* yetu ya Taifa zifanye vizuri kama hakuna uwekezaji wa kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitahitaji majibu sahihi. Tunataka tujue hatma ya Waandishi wa Habari. Hii siyo kazi ya lelemama ni kazi muhimu sana. Waandishi wa Habari wakiwa vitani wengine wanakimbia, wao wapo mstari wa mbele kutoa habari. Sehemu yoyote kwenye *crisis* Waandishi wa Habari watakuwa mstari wa mbele lakini hawathaminiwi kutokana na kazi wanayoifanya. Nitaendelea kulisema hili na nitahitaji lifanyiwe kazi, jambo hili la Waandishi kama la kikotoo sitaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwandishi wa Habari najua kazi ya kutafuta habari, najua *risk* wanazozipata, najua changamoto wanazozipata, *I swear* sitakubali Mheshimiwa Nape. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane, ajiandae Mheshimiwa Mussa Omar Salim.

**MHE. FRACIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kwa ujumla ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dokta Samia

Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anashughulikia ipasavyo utatuzi wa kero mbalimbali na changamoto mbalimbali za wananchi wetu wa Tanzania katika tasnia hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nimpongeze sana sana sana Ndugu yangu Nape Moses Nnauye ambaye leo ningependa kumtunukia mimi binafsi cheo cha ujemadari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini miaka 118 iliyopita ililshuhudia majemadari 30 wakiongoza Vita vya Majimaji kwa ajili ya kutokomeza ukoloni wa Wajerumani. Leo nimeamua kumtunukia ujemadari Nape Moses Nnauye siyo kwa ajili ya kutupa mikuki dhidi ya wakoloni, bali ni kwa ajili ya kupambana na adui ujinga, umaskini na maradhi kupitia tasnia ambayo anaiongoza ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Bila tasnia hii kusimamiwa vizuri, adui ujinga, maradhi na umasikini hawezi kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia wiki moja iliyopita Serikali yetu imesaini mikataba kwa ajili ya ujenzi wa minara 758 katika Kata 713 hapa nchini. Hili ni tukio kubwa la kimapinduzi ambalo linakwenda kuipeleka nchi yetu katika mstari wa mbele kabisa wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoingia madarakani kwa nafasi ya Ubunge, Jimbo langu la Kilwa Kaskazini lilikuwa na vijiji 22 ambavyo vilikuwa havina mawasiliano ya simu lakini ndani ya mwaka mmoja ilipofika mwaka 2021 Serikali iliweza kutujengea minara minne katika Vijiji vya Pungutini, Nandete, Chapita na Mwengei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia juzi Serikali imeingia mkataba na kampuni mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa minara ya simu. Napenda nikutaarifu, sisi Wilaya ya Kilwa tumepata minara 15 ambayo itajengwa katika vijiji 21 vya Wilaya ya Kilwa, na jimbo langu litapata minara minane ambayo itaweza kutoa mawasiliano katika vijiji vipatavyo 10. Kwa hiyo, ukichukua ile

takwimu ya vijiji 22, ukitoa vile vinne vya mwaka 2021, ukitoa hivi 10 ambavyo vinaenda kupata huduma ndani ya miezi tisa ijayo, tayari tutakuwa na vijiji vipatavyo vinane, ndiyo vitabaki kuwa havina mawasiliano ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naipongeza Serikali kwa kuweza kufanya kazi kubwa ndani ya kipindi kifupi. Ndiyo maana nimempa huu wadhifa wa ujemedari ndugu yangu Mheshimiwa Nape Moses Nnauye. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maeneo yafuatayo yazingatiwe katika utekelezaji wa hii miradi ya ujenzi wa minara 15. Katika jimbo langu kuna Kijiji kinaitwa Zinga Kibaoni kimeainishwa kwamba nacho kitapelekewa mnara. Hiki kijiji ni kipana sana. Uki-*calculate* ile *dimension* ya kijiji toka kona moja mpaka nyingine, ni zaidi ya kilometa 40. Sasa tayari pale katikati ya kijiji kuna mawasiliano ya *Halotel.* Kuna kitongoji ambacho kina watu wengi zaidi kinaitwa Nambunju, naomba mnara huu upelekwe Nambunju. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Kijiji inaitwa Namatewa, kinajengewa minara miwili, lakini wakati huo Makao Makuu ya Kata hakuna mnara hata mmoja uliojengwa pale Kandawale. Kwa hiyo, naomba mnara mmoja ambao ulikuwa ujengwe Kandawale na *Airtel* upelekwe Kandawale ili pale Namatewa ubaki mnara mmoja. Naomba hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna changamoto katika ile minara minne ambayo ilijengwa mwaka 2021 katika Vijiji vya Pungutini, Nandete, Mwengehi, pamoja, Chapita, pamoja na Kijiji cha Mtopera. Ile minara inatumia teknolojia ya *solar* kwa ajili ya kuipa nguvu iweze kufanya mawasiliano. Hili limesababisha changamoto kwa ile minara kuweza kufanya kazi kwa masaa yasiyozidi 10 kwa siku, na matokeo yake kumekuwa na malalamiko mengi. Kwa sababu mwingine anaweka *bundle* litatumika masaa 24, lakini mwisho wa siku ndani ya masaa 14 ya saa hizo 24 mawasiliano yanakuwa hayapo na wakati bado *bundle* lake lilikuwepo kwenye simu. Matokeo yake anashindwa kupata haki yake ya kutumia lile *bundle* mpaka liweze kwisha.

Kwa hiyo, naomba Serikali iunganishe hii minara yote na mtandao wa umeme wa *REA* ambao upo katika hatua za mwisho za kukamilisha katika hivyo vijiji vyote nilivyovitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nivitaje vijiji vinane ambavyo vimebaki ambavyo havitakuwa na mawasiliano ya simu baada ya mradi huu wa maeneo 15 kukamilika. Vijiji hivyo ni vya Hanga, Kinywanyu, Ingirito, Kongwe, Marendego pamoja na Namanungutungu na pia kipo Kijiji cha Nandombo pamoja na Kijiji Nambondo. Naiomba sana Serikali katika awamu ijayo ya ujenzi wa minara hivyo vijiji vinane vifikiriwe ili tuweze kupata mawasiliano mwanana jimbo zima na wilaya nzima ya Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa naipongeza *TBC* kwa kazi kubwa wanayoifanya, na nimeona jana pale nilipokuwa napita kwenye banda lao, wamelenga kujenga kituo kikuu cha mawasiliano ya *TBC* katika Wilaya ya Kilwa pale Nangurukuru. Naomba kazi hiyo iendelee ifanyike kwa haraka kwa sababu kuna changamoto kubwa ya Mawasiliano ya *TBC*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mussa Omar, jiandae Mheshimiwa Joseph Kamonga. Mheshimiwa Mussa hayupo. Mheshimiwa Kamonga, jiandae Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mjadala wa bajeti hii. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Nampongeza sana kwa kuwa kazi anayoifanya kwenye eneo hili ni kubwa sana ni lazima tuweze kumpongeza. Vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Nape Nnauye, Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Kundo na

taasisi zao zote. Kuna *TCRA*, kuna *UCSAF,* kuna yule dada yangu Justina, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomshukuru Mheshimiwa Nape, kwa sababu anapafahamu pale Lupingu kuna mwaka alienda akiwa Mwenezi wa Chama Taifa, na nilipoenda kumwomba mnara wa simu, alimtuma Naibu wake tukaenda mpaka pale wakapanda boti mpaka sehemu inaitwa Igha. Aliwaahidi wananchi wale kwamba atawasha mnara mapema. Nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali, sasa hivi Kata yote la Lupingu, wananchi hata wakiwa kwenye maji wanavua Samaki, wanaweza kuwasiliana. Likitokea tatizo lolote, ajali yoyote, mawasiliano yanakuwa ya mapema kwa sababu kuna mnara pale ambao unaweza kusaidia kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni ishara kwamba wizara hii inatambua kwamba mawasiliano ya simu siyo anasa, ni hitaji la muhimu kwa dunia ya leo, wananchi wanatumia kwa manufaa mbaliambali kuweza kupeana habari kwa ajili ya biashara mbalimbali, fursa mbalimbali kupitia mitandao ya simu. Vilevile kwenye shule zetu za msingi, walimu wanasajili wanafunzi wa Darasa la Saba kwa kutumia mitandao ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule, zahanati zetu hii mitandao inatumika kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kila siku. Kwa hiyo, na kule Ludewa maeneo mengi ambayo yako pembezoni tuna zahanati nyingi ambazo zinahitaji mawasiliano ya simu. Tuna shule za msingi zaidi ya 100 ambao walimu walikuwa wakitembea umbali mrefu sana kwenda kusajili wanafunzi wale wa Darasa la Saba. Nafurahi kwamba tokea nimekuwa Mbunge Serikali hii ya awamu ya sita imeweza kunisaidia kupata minara 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata mnara pale Madope, tayari unafanya kazi; tulipata mnara Kijiji cha Ilawa Kata ya Madilu, unafanya kazi; Tulipata mnara Mkongobaki, Ibumi, Lupanga na Galawale pale Kata ya Ludewa ambao unahudumia hadi Nindi kule; Kuna mnara Mkumbili, kuna mnara Mkomang’ombe, Mapogoro ambao unaenda kujengwa sasa

mnara wa *Tigo*; kuna mnara Shaurimoyo na Mdiligili ambao unakwenda kujengwa sasa wa *Vodacom*; kuna mnara Kitowele; na Lupande ambao unakwenda kujengwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa Lupande alikwenda, alifanya mkutano na aliwaahidi wananchi kwamba atakwenda kujenga mnara, Serikali itapeleka mnara pale. Kwa hiyo, nafurahi sana siku ya utiaji saini mikataba ile 758 mimi nilikwenda pale kwa niaba ya wananchi wa Ludewa na niliona hawa wananchi wa Kitewele na Lupande sasa watakwenda kupata mnara kama ambavyo Mheshimiwa Waziri aliweza kuahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunapata mnara ni Mapogoro, mnara wa Tigo, kuna eneo la Ludende mnara wa *Vodacom*, kuna Iwela tumepata mnara wa *TTCL* na Igalu. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Ludewa kuishukuru sana sana Serikali. Hata mimi Mbunge mmenipa heshima sana, nikipita kwa wananchi naonekana Mbunge wa maana kwa sababu ya Mheshimiwa Nape Nnauye na Serikali ya Awamu ya Sita. Kwa sababu kule kwetu minara ilikuwa changamoto kubwa sana ila sasa hivi kwa mwendo huu, naamini tutafika mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuiomba Serikali iendelee kuangalia ile Kata ya Ibumi, eneo lile lina utajiri mkubwa wa madini, kuna migodi mikubwa inaenda kuanza pale. Kwa hiyo, mawasiliano yatakuwa muhimu sana hasa Kijiji kile cha Masimavalafu, kuna *reserve* kubwa sana za *copper* na makaa ya mawe, kwa hiyo, kuna wawekezaji kule. Naishukuru Serikali mwaka huu kupitia TAMISEMI, wataenda kutujengea daraja pale ambalo linaunganisha Kata ya Ibumi na Kata ya Itumbandyosi ambayo iko kule kwa Mheshimiwa Benaya. Kwa hiyo, maeneo haya, mawasiliano yatakuwa muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Kijiji kile cha Masimavalafu kiweze kupata mawasiliano ya simu. Tunao mnara pale wa *TTCL* na umewashwa kipindi nikiwa Mbunge, kwa hiyo, naishukuru sana Serikali, lakini *coverage* yake bado ni

ndogo. Siku ile niliongea na Mkurugenzi yule wa *TTCL* akaniahidi atatuma wataalam. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana msaada wako, hawa watu wa *TTCL* waweze kwenda pale kuongeza uwezo wa ule mnara ili uhudimie kile Kitongoji kile cha Nyamalamba na maeneo jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, Tarafa ya Mwambao Kijiji cha Lumbila Kata yote ya Lumbila, Kata ya Makonde na Kata ya Kilondo, wana mnara ule wa *Halotel* ambao nao kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameeleza, unategemea teknolojia ya umeme wa jua *(solar)*. Sasa kukiwa na hali ya hewa kidogo ya mawingu mawingu, wananchi wanakosa mawasiliano. Kabla ya Mheshimiwa Naibu Waziri wataalam walishaenda na vipimo wakaweza kutambua maeneo yote. Kwa hiyo naomba tu utekekelezaji ufanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, nashukuru sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Eric Shigongo, jiandae Naibu Waziri.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *mic* zote zinasumbua.

**NAIBU SPIKA:** Hama tu, wala huna haja ya kuuliza. Kwani ukikosa mshahara unasema, si unahamia benki nyingine! Wewe ingia tu hapo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika,…

**NAIBU SPIKA:** Njoo huku kwa Mawaziri.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa…

**NAIBU SPIKA:** Hamia upande wa huku.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Njoo huku. Njoo hapa uongee. Wewe njoo uongee. wewe vipi wewe! *Feel free. (Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo, hamia kule. Kaa kule. *(Kicheko)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kushukuru sana kwa *microphone* kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rasi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mema ambayo anaifanyia Taifa langu upande wa mawasiliano. Tanzania imeshuhudia maendeleo makubwa sana upande wa teknolojia kwenye kipindi hiki cha Awamu ya Sita. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, rafiki yangu kwa kazi kubwa anayoifanya. Nakupongeza sana kwa sababu kumekuwa na uhuru mkubwa sana wa kujieleza kwenye kipindi cha Rais wa Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii naisema niki-*declare interest* kwamba mimi ni mdau wa habari. Nimekuwepo Awamu ya Tano, na Awamu ya Nne nikifanya kazi ya habari. Kwa hiyo, ninaposema kwamba Awamu ya Sita tuna uhuru zaidi ya tulikotoka, iko sababu kubwa sana ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na wewe Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana mdogo wangu Kundo kwa kufika mpaka jimboni kwangu na kujionea hali halisi ilivyo. Sasa wananchi wa Buchosa wamenituma. Buchosa ni jimbo kubwa, lina visiwa vingi sana. Watu wa visiwani hawana minara. Mawasiliano kwao ni magumu, na kuna wakati wanakuwa kwenye hatari ya kuzama, wanashindwa kuwasiliana. Kwa hiyo, naomba mwakumbuke sana watu wa visiwa vya Sosswa, Simbaya, na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema maisha ya vyombo vya habari ni magumu. *Media houses* zina-*suffer.* Sasa ombi langu kabla sijaenda mbali ni kumwomba Mheshimiwa

Waziri, msiwapatie ruzuku vyombo vya Habari. Ruzuku wapeni *TSN*, Uhuru na wengineo. Sisi tunachokitaka na wengine huko, vyombo vya habari vya Serikali vijitoe kwenye matangazo. Yaani *ITV* wasigombanie matangazo na *TBC*. *BBC* hawachukui matangazo, *Voice of America* hawachukui matangazo, vyombo vya Serikali, visigombanie matangazo na vyombo binafsi. Hiyo peke yake inatosha kuwasaidia vyombo vya habari viweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zetu za bajeti hapa zikienda kwenye vyombo vya habari kwa ajili ya *promotion* na matangazo vyombo vitaweza kulipa wafanyakazi wake. Nami namshukuru sana dada yangu, Mheshimiwa Esther ameongea mambo mazuri kabisa hapa. Ahsante, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uongozi ni kutatua tatizo kabla halijatokea. Yaani uwe na uwezo wa kusema mwakani kutakuwa na njaa, kwa hiyo, unaweka chakula. Dunia imebadilika sana. Tanzania imebadilika sana. Mtu yeyote anaweza akashangaa kwamba zamani tulikuwa tunapiga picha; tunaweka filamu kwenye *camera,* lakini leo hii hamna. Tulikuwa tunatumia *diskette,* leo hii hazipo. Dunia inabadilika kwa kasi mno, lazima tubadilike nayo. Tusipobadilika sisi leo, utakuta tumechelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposimama hapa leo, nataka kusema hivi, huko tunakokwenda mambo yatabadilika. Sisi kama Taifa tufanye nini? Narudia yale yale ninayoyasema kila siku. Sisi kama Taifa tuelimishe watoto wetu, tuwekeze kwa kuelimisha watoto wetu. Katika hili, Mheshimiwa Waziri ni kweli wewe sio Wizara ya Elimu, lakini unashughulikia masuala ya TEHAMA. Naomba na ninasisitiza *computer* zisambazwe mashuleni, watoto wetu wafundishwe *computer* kuanzia *primary schools* ili matatizo yanayokuja huko mbele tuweze kukabiliana nayo. Tusipofanya jambo hilo, nataka niwahakikishie tutaachwa na hatutaweza kushindana na wenzetu kwenye ulimwengu unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aelewe kwamba suala la ubunifu na *innovation* ni jambo la muhimu sana. Wasaidie wabunifu wa Taifa hili. kuna vijana wengi

sana wana ubunifu, nawe unawafahamu, lakini hawana mitaji, na wameshindwa kupiga hatua mbele. Benjamin Fernandes alianzisha mnara, kijana wa kitanzania, ameanzia hapa na matokeo yake amehamia nchi nyingine kwa sababu hapa nyumbani alikosa *support*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna kijana anaitwa Magila Tech wote tunamfahamu, ame-*invent* mifumo mingi sana nyumbani. Ni kijana wa kitanzania, ana akili nyingi Mungu kamjalia, anafanya mambo mengi, lakini hapati *support* ya Serikali. Mabenki hayamtumii kutengeneza mifumo. Wanatoa kazi kwa mataifa ya nje, baadaye inaonekana kama mifumo waliyoiweka haifanyi kazi, wanamfuata Magila Tech huyo huyo aje atengeneze mfumo. Kwa hiyo, naomba tuwaelimishe sana watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, na la umuhimu na la kusikitisha ni kwamba, Rais wetu alikwenda Dubai akakutana na Mwenyekiti wa Makampuni ya *Airtel* akaahidi yule tajiri ya kwamba ataisaidia Tanzania kwenye mambo ya *technology*. Mheshimiwa Waziri kama hujui sasa unisikilize vizuri. Yule bwana ameamuru kampuni yake iliyoko hapa itoe *data* bure kwenye shule za msingi na sekondari katika nchi hii ambapo thamani yake ni Dola 830,000, lakini eti *TRA* wamekataa kutoa *exemption* ya *VAT* pamoja *excise duty. Are we serious?*

**MBUNGE FULANI:** *We are not. (Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashindwa kuelewa. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kutana na Mheshimiwa Mkenda, kutana na Mheshimiwa Mwigulu mjadiliane suala hili. Baadaye mimi nitakamata shilingi yako kwenye hili. Hatuwezi kukubali tunapewa fedha zote hizi zisaidie walimu wetu tumewagawia vishikwambi huko vijijini, lakini hawana *internet*. Halafu mtu amekataa kutoa *exemption* ya *VAT* na *excise duty*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili nitalisimamia na nitapambana na Waheshimiwa Wabunge naomba mniunge mkono nitakaposhika shilingi leo jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi ya kusema sana sina. Nakupongeza sana Waziri Nape na Makamu wako. Nakuamini sana na unajua. Nawe ni kijana mwenye akili, huwezi kushindwa kutatua matatizo yetu. Hakikisha kwamba Tanzania inakwenda mbele kiteknolojia. Jambo hilo linawezekana.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwenye *global innovation index,* Tanzania ni ya 90 Duniani, Kenya ni ya 89, lakini Mauritius ni ya 35. Sisi tunashindwa nini? Akili tunazo, tutumieni akili zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, kiuchumi, kisiasa, kidiplomasia pamoja na mambo mengi sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu na kutupatia fedha nyingi sana za miradi ya maendeleo kwani miradi inayotekelezwa hivi sasa ni mikubwa sana ambayo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020-2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wetu, wewe mwenyewe

Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge letu kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge hili toka tulivyoanza, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Nape Nnauye – Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Engineer* Mathew Kundo - Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na watendaji wa Wizara na taasisi zilizoko chini ya Wizara hii muhimu kuendana na utendaji wao wa kila siku, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kuishauri Serikali kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kupitia hotuba ya Waziri na maoni na mapendekezo ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali iangalie utaratibu wa kuboresha minara yetu ya *TTCL* kwani tuna minara mingi ya *TTCL* ina uwezo wa chini kupokea usikivu wa mawasiliano hali ambayo inawafanya wananchi wengi kutokutumia mitandao yetu ya *TTCL* kuliko mitandao mingine ya simu. Hivyo basi ushauri wangu timu ya wataalam wetu wa Wizara wafanye tathimini ya minara yote ya *TTCL* kwa lengo la kufanya maboresho ya usikivu na kuleta ushindani na minara ya mitandao mingine kwa ajili ya kujibu kiu ya watumiaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuwezesha masomo ya TEHAMA katika shule zetu za sekondari nchini hasa zile za *A-level* tunaiomba Wizara hii kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* kuzipatia shule hizi *computers* ili kuwezesha wanafunzi wetu wa shule za sekondari za kata waweze kijifunza TEHAMA na kushindana na wanafunzi wenzao wa shule binafsi na kuwajengea uwezo wa kufahamu kikamilifu matumizi ya TEHAMA kabla ya kuhitimu masomo ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali yetu idhibiti *sms* za utapeli zinaotumwa kupitia *line* za simu zetu za *TTCL* na matapeli kuomba hela kwa wananchi kwa kuwa hapo awali *line* za simu mitandao mingine zilikuwa zinatumika, ni dhahiri kuwa walifanya maboresho katika kukomesha tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA;** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote; pili, shukrani kwa vyombo vya habari na mashirika ya mitandao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lisaidiwe katika kuboresha huduma zake za maktaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Mkongo wa Taifa utafika Mbamba Bay?

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ya *TBC* Nyasa yaendelee kuimarishwa.

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ije na mkakati wa kukuza mawasiliano kutokea vijijini, kwa sasa habari zinazotolewa asilimia 95 ni za mjini pekee, hivyo kuna haja ya kuja na mkakati wa kuupatia umma mzima haki ya kutoa na kupata habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ishugulikie tatizo la waandishi zaidi ya asilimia 90 kufanya kazi kama vibarua, hawalipwi mishahara na wale wenye mishahara hawalipwi kwa wakati, Wizara iunde timu maalumu kupitia kila chombo kujua haki za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuja na hoja ya minara mingi nchini, lakini bado matumizi ya

minara yanatufanya kuwa *analogue* siyo *digital,* sasa hivi nchi nyingi zinatumia *satellite,* kwa nini tusiwekeze huko kuachana na minara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, njoo, njoo, njoo mbele tu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nipende kutoa shukrani zangu na pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake makubwa katika sekta hii ya mawasiliano kwa kufungua milango ya uwekezaji. Ambapo sisi sekta ya mawasiliano tunaiona na katika kuwekeza, katika miundombinu na mifumo ya mawasiliano na pia kwa utayari wake ili kurejea Sera na Sheria ambazo haziendani na wakati wa sasa, ambapo tuna teknolojia zinazoibukia hivyo basi Mheshimiwa Rais yuko tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuridhia mchakato wa uundwaji wa *satellite* yetu. Ambapo anaenda kuweka alama kubwa sana katika sekta ya mawasiliano na katika ulinzi wa nchi yetu hivyo tunampongeza sana kwa kutekeleza mfumo wa anuani ya makazi kwa asilimia 100 kabla hata ya kufikia mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kwa kuakikisha kwamba leo hii nasimama katika bajeti ya tatu ya Wizara hii nikiwa namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelezo yake, kwa ushauri wake wa kuhakikisha kwamba sisi wasaidizi wake tunaendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa. Nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Nape Moses Nnauye Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa uongozi wake mzuri, maelekezo yake na kwa malezi yake yenye lengo la kuinua Sekta ya Habari na Mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Katibu Mkuu, Mheshimiwa Mohammed Khamis Abdulla pamoja na Naibu

Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara yetu. Niwapongeze na kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Bariadi kwa kuendelea kunipatia ushirikiano katika majukumu yangu ndani ya jimbo na wakati napotekeleza majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kutumia fursa hii kumshukuru sana mke wangu Grace ambaye kwa kweli ananipatia utulivu na kuhakikisha kwamba nawajibika vizuri katika majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuongoza Bunge hili kwa viwango vya kimataifa. Baada ya kusema hayo sasa naomba nirejee hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunaishukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Miundombinu pamoja na michango yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wamejaribu kugusia. Niseme jambo moja Wizara hii *champion* wake ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania akisaidiwa na kaka yangu, Mheshimiwa Waziri, Nape Moses Nnauye, pamoja na Taasisi zetu ambazo ziko chini ya wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumebaini kuna changamoto katika mgawanyo wa minara ambapo Waheshimiwa Wabunge wamejaribu kugusia na mgawanyo huu tuliangalia kwa kuangalia wilaya kwa wilaya. Lakini baada ya kugawa kwa wilaya tukagundua kwamba kuna majimbo mawili kwenye baadhi ya wilaya hatimaye tukajikuta kwamba kuna baadhi ya majimbo yanapata minara mingi na majimbo mengine yanapata minara michache, hivyo tumeishaliona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitumie fursa hii katika Bunge lako tukufu kusema kwamba Mheshimiwa Rais, amesaini mikataba ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika Kata 713 kwa ujenzi wa minara 758. Hiyo ni mvua ambayo haijawahi kushuhudiwa sasa tunakuja na mvua nyingine ya kuleta minara 1,600. Ambapo Mheshimiwa Rais tayari ameisharidhia na

ameishatafuta fedha na tutaanza na minara 600, ambayo kufikia Desemba nafikiri fedha zitakuwa zimeishapatikana tayari mchakato utakuwa umeishaanza wa kutafuta wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Waheshimiwa Wabunge niwatoe hofu na Watanzania kwa ujumla mvua hii itakapokatika itaanza mvua nyingine ya minara. Kwa hiyo, tutahakikisha nchi yetu inafikishiwa huduma ya mawasiliano kwa mujibu wa utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wameligusia kwamba Wizara yetu mpaka sasa tumepokea fedha kidogo katika miradi ya maendeleo. Miradi yetu yetu inatekelezwa kwa ujenzi na wakandarasi, mkandarasi anapopatikana hatuwezi kumlipa fedha zote mpaka pale atakapokuwa anatoa *certificate* na miradi hii mingine inakamilika kwa miezi sita, mwaka mmoja. Hivyo tunatarajia kila anapokamilisha hatua moja na anapo *raise certificate* na ndipo tunapoweza kufanya malipo. Kwa hiyo, fedha zipo na tuna uwakikia watakapoleta *certificate* watalipwa na miradi itakamilika bila kuwa na changamoto yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna baadhi ya Waheshimiwa wameshauri na kuna baadhi ya changamoto nipende kusema kwamba baadhi ya changamoto zao tumezipokea, ushauri wenu tumeuzingatia, maoni yenu tunayazingatia na tutahakikisha kwamba tunaenda kuyafanyia kazi kwani nyinyi mko hapa kwa niaba ya Watanzania milioni 63 hivyo Serikali hii ya Mama Samia Suluhu Hassan ni sikivu na sisi wasaidizi wake tutahakikisha kwamba tunafanyia kazi mambo yote hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee jambo moja la mkomazi Mheshimiwa Zuena Athumani Mbunge kutoka Kilimanjaro aliongelea kuhusu usikivu wa *TBC*. Usikivu wa *TBC* tulikuwa na mtambo wetu pale Rombo Tarakea ule mtambo uko chini na sasa tunaenda kufunga mtambo mwingine pale Rombo

*DC*. Hivyo tutakuwa tumetatua kabisa changamoto ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile umeongelea kuhusu hifadhi ya Mkomazi, katika hifadhi hiyo tayari kuna mawasilino tunapeleka katika eneo la Kata ya Kilia, Kwakoa, Toloha pamoja na Mgagawa ambazo ziko pembezoni mwa nchi yetu ambapo baada ya kuweka hiyo minara itaweza kufikisha huduma ya mawasiliano katika lango la hifadhi ya Mkomazi. Kwa suala kama hili naamini kwamba Mheshimiwa Mbunge awe na subira na Serikali iko kazini kuhakikisha kwamba changamoto hii inatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wakiishukuru Serikali na sisi hatuta bweteka kwa shukurani zao. Sisi tutaendelea kuhakikisha kwamba katika maeneo ambayo bado hayajafikishiwa huduma na mawasiliano na katika changamoto zile ambazo wamekuja kuzisema kwa niaba ya wananchi wao sisi tunazichukua na tutaenda kuzifanyia kazi kwa weledi, maarifa yote kwani tunazingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru sana na niombe kusema kwamba niwashawishi Waheshimiwa Wabunge, tuiunge Bajeti yetu hii kwa asilimia mia moja kwani ni bajeti shirikishi na ni bajeti ya wananchi…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ahsante kwa mchango mzuri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge naongeza nusu saa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuhitimisha hoja. Kwa unyenyekevu mkubwa niwashukuru sana

Wabunge wote kabisa kwa maneno mazuri ya faraja mliyotupa hapa, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno yenu ni chachu ya sisi kuendelea kuwa wasikivu, wanyenyekevu lakini kuchapa kazi kwa bidii kuhakikisha yale matarajio nyinyi mliyonayo lakini na wananchi wenu yanatimizwa lakini pia tunatimiza lengo la Rais kuanzisha Wizara hii lakini na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ahsante sana, sana.. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, maneno mengi mliyoyasema hapa ni ya ushauri sisi hatuna haja ya kuyarudia hapa, niwahakikishieni tumechukua neno moja baada ya jingine mahali ambapo panakasoro tutakwenda kurekebisha, mahali ambapo pana mapungufu tutaongeza ili pakae sawa sawa, mahahi ambapo mmetupa mawazo mapya mimi na wenzangu tutayafanyia kazi na kuhakikisha tunafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vitatu nataka kuvizungumza kwa dakika tatu. La kwanza; suala la maslahi ya Waandishi wa Habari, jambo hili haliwezi kutatuliwa kwa kauli za kisiasa, jambo hili lazima litatuliwe kwa sheria na ndiyo maana tumeileta sheria ya huduma za habari hapa ili Wabunge tuipitie mle ndani tuweke misingi ya kulinda haki za waandishi wa habari wa nchi hii. Tuondakane na utaratibu wa waandishi wa habari kupewa haki zao kwa hisani, wapewe kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua katika sekta zilizo hathirika na myumbo wa uchumi kutokana na vita ya Urusi na Ukraine lakini na *Covid* sekta ya habari imeathirika sana na ndiyo maana hali ya vyombo vya habari si nzuri. Uchumi wao unayumba, leo hata tukiwatungia sheria ikawa kali namna gani utekelezaji wake utakuwa mgumu, kwa sababu hali ya uchumi wao ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa maelekezo ya Rais Dkt. Samia tumeunda timu nzuri inayoongozwa na ndugu Tido

Mhando na tumewachukua watu nguli wa sekta kwenda kuangalia hali ya uchumi wa vyombo vya habari lakini wanaenda kupitia na mikataba ya waandishi wa habari ili watuletee pamoja na sheria tutunge kanuni baada ya hapo nataka niwahakikishieni sekta hii itarudi na kupata heshima na hadhi inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawaombeni pitisheni bajeti yangu tukamalizane na jambo hili kwa kuweka mifumo na ndiyo kazi ya Waziri, Waziri siyo matamko, Waziri ni kuweka mifumo ya kutatua tatizo na ndiyo kazi naenda kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; ni suala la wizi wa matapeli mitandaoni. Ndugu zangu sekta hii nimesema hapa tuna *line* za simu karibia milioni 63 zaidi ya idadi ya watanzania maana yake watu wako wengi kwenye huu mfumo na katika wingi huo kwenye msafara wa mamba kenge wako wengi pia. Katika kulishughulikia hili tumefanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni usajili wa *line* ulikuwa holela baadaye mtu akifanya uhalifu mkimkamata mnakuta ile *line* imesajiliwa na mtu mwingine ile kesi inafia palepale, ukienda Mahakamani akiiruka inaisha. Tulichofanya tumezisajili *line* zile kwa kutumia alama za vidole na penyewe pakawa na utapeli. Ndiyo maana juzi tukafanya uhakiki, baada ya uhakiki wa juzi tunaamini *line* zote zilizoko mtaani zina mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapa nataka nitangaze kiama cha matapeli kwenye mitandao na nitaliomba Bunge lako litusamehe kidogo kwenye hili, tutafumba macho kidogo hata kwenye zile haki za msingi. Kwa sababu yako mambo yanaudhi. Kwa hiyo, leo natangaza kiama cha jambo hili, tumejipanga vizuri tutawaomba wenzetu wa polisi na wengine tuondoe huruma kwenye jambo hili tulikomeshe, tulifute kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu; na mwisho kaka yangu Mheshimiwa Eric amezungumza jambo kubwa hapa. Nikuhakikishie kaka yangu wala huna haja ya kukamata shilingi yangu, jana nimekuta na *Airtel* wamenieleza jambo hili nilipoingia

Dodoma nikakutana na Waziri Mheshimiwa Profesa Mkenda tumelizungumza, asubuhi nimeongea na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tunaenda hakuna sababu ya kubaki nalo, hili jambo limeisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie hili jambo limeisha tunazitaka hizi *data* kwenye shule zetu na juzi Rais ametuagiza kwamba tusambaze kwenye mashule yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru kwa maneno yako mazuri na naomba nisitumie muda mrefu kama nilivyofanya asubuhi. Waheshimiwa Wabunge tuaminini, pitisheni bajeti yetu, ahsanteni sana, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……..............................…Sh. 2,355,648,104

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuna mshahara wa Waziri na majina kadhaa hapa. Tunaanza na Mheshimiwa Venant Daud Protas kutoka CCM.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nilikuwa nataka ufafanuzi wa jumla. Kwanza pamoja na jitihada nzuri za Serikali ambazo zinazozifanya tumeona minala zaidi ya

700 imesainiwa. Lakini nataka tupate *commitment* ya Serikali, kumekuwepo na changamoto sana hasa barabara kubwa ambazo zote zinazolisha mikoa na mikoa kwa mfano kuna Barabara ya Majimoto kuja Inyonga kilomita 100 ukija kwenye lile pori kote pale hakuna mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ambayo inatoka Itigi kwenda mpaka Tabora Mjini zaidi ya kilomita 200 hakuna mtandao, ukienda pale na ajili nyingi zinatokea watu wanashindwa kupata msaada. Vilevile ukija maeneo ya Senkenke kwenye ule mlima hakuna mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kauli ya Serikali kupitia barabara zote kubwa ziweze kuwa na mawasiliano ili inapotokea changamoto, wananchi wanapopata changamoto maeneo hayo wawezekupata msaada? sina nia ya kushika shilingi lakini tunataka maelezo thabiti ya Serikali ili iweze kutoa maelekezo kwenye mwaka huu wa fedha iweze kujenga hizi barabara ziweze kuwa na mawasiliano na wananchi wapate huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. Hapo hapo, haifanyi kazi *okay.*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kaka yangu kwa hoja hii. Wakati tunagawa hii minara tulisema tuanze kule waliko watu, kwanza lakini kama alivyosema Naibu Waziri hapa tuna minara mingine 600 inakuja hivi karibuni na mingine elfu moja na kitu kipaumbele ni kwenye hayo maeneo aliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilipita kama miezi mitatu, nilipita kutoka Mlele kuja Tabora nimeona lile pori refu na kulikuwa na kipindi mpaka usafiri walikuwa inabidi wasafari mchana kwa sababu ya hali ile. Kwenye lile eneo tumeishaweka minara saba na kuna maeneo mingine ya aina hiyo ambayo yana changamoto za mawasiliano barabarani tumepanga huo

utaratibu upo katika hii minara tutakayoileta tutasambaza kwenye hayo maeneo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi kwenye jambo ambalo Waziri ujalizungumzia kabisa na kwenye mchango wangu nilisema. Vyombo vya habari vinategemea sana matangazo kujiendesha *including* na kulipa mishahara na posho mbalimbali ya wafanyakazi na nikasema vyombo vya habari binafsi ukichanganya na vya Serikali vinaidai Serikali karibia bilioni 30 na hizi ni pesa za muda mrefu kuna wengine miaka 10, wengine miaka mingapi lakini hata kile kidogo wanachokilipa wanatumia muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha mnalipa vyombo vya habari viweze kujiendesha lakini vilevile waweze kulipa wafanyakazi wao, Mheshimiwa Waziri nahitaji tu *commitment* wala sihitaji kushika shilingi yako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ester nashukuru sana. Kwanza nakushukuru kwa kutokuwa na nia ya kukamata shilingi lakini nakupongeza kwa kuendelea kuwatetea na wana habari katika Bunge hili unafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikweli kwamba vyombo vya habari vinadai siyo tu Serikalini lakini na maeneo mengi hii *figure* inayotajwa inatofautiana mimi hesabu niliyonayo ni bilioni 18, yeye anasema karibia bilioni 30 changamoto iliyopo ni hiyo ya kwanza. Kwamba hata hiyo namba yenyewe ya kiasi kinachodaiwa haiko sawa na jana tulikuwa na Mheshimiwa Rais kwenye shughuli ya *Azam* na Rais kwa dakika mbili tatu aliongea na wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari na akalizungumzia jambo hili, akasema moja ya changamoto kubwa tuliyonayo ni ushahidi pia wa hayo madeni. Tumekuwa na changamoto ya watu wengi kufanya kazi kwa simu anapigiwa simu na Waziri toa

tangazo anatoa. Halafu akija huku anakuwa hana ushahidi wa yale madai lakini Rais jana ameagiza, jana mchana madeni yote ambayo yana ushahidi Serikali ianze kuyalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia Bunge lako hapa nataka niwahaidi kusiwe tu Serikali kuu mpaka Serikali za mitaa kila mahali na taasisi zake. Kama kuna mtu anadaiwa ni vizuri akaanza kulipa sasa kwa yale madeni ambayo yamehakikiwa, yale ambayo hayajahakikiwa utaratibu wa kuyahakiki ufanyike na wakichelewa kuyalipa itabidi tuchukue hatua za ziada hata kama ni kwa kukata na fedha kupeleka kwa sababu hali ya vyombo vya habari siyo nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kifungu hicho kina afikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kikilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 68 – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………. Sh.572,792,800
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*………………Sh.768,009,840
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*……………………… Sh.317,584,900
Kifungu 1005 - *Legal Service Unit*………………………Sh. 371,144,604
Kifungu 1006 - *Government Communication Unit*…. Sh.377,821,200
Kifungu 1007 - *Procurement Management Unit*…..…Sh.424,012,800
Kifungu 2001 - *Communication Division*…………....Sh.2,292,747,432
Kifungu 2002 - *Information Communication and Technology*…...........................…Sh.2,194,752,632
Kifungu 4001 - *Information Services Department*...Sh.20,660,950,020
Kifungu 4002 - *ICT Systems Development Services Division*................................................Sh.992,373,608
Kifungu 4003 - *Communication Safety and Security Unit*…......................................Sh. 859,050,216
Kifungu 4004 - *ICT Infrastructure Unit*…...………………Sh. 511,547,476

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaingia kwenye *guillotine.*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*……………Sh. 4,500,000,000
Kifungu 1006 *Government Communication Unit* ……..............…Sh. 0
Kifungu 2001 - *Communication Division*…..………Sh. 27,300,000,000
Kifungu 2002 *Information and Communication Technology*… Sh. 0
Kifungu 4001 - *Information Services Department*…..............................…Sh. 26,500,000,000
Kifungu 4002 - *ICT Systems Development and Services Division*……….....................…Sh.43,653,940,000
Kifungu 4004 - *ICT Infrastructure Unit*………..……..Sh. 80,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekalisha kazi zake naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono. Sasa nitawahoji; kwamba sasa Bunge likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2023/2024. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wako na Watalamu wenu wote kwa kweli hakuna siri mnafanya kazi nzuri na mmeweza kuwafikia Watanzania wengi lakini hiyo changamoto Mishahara ya Waandishi, utapeli kwenye simu unajua ni mahusiano makubwa na *international crime organization* lakini jaribuni na nyinyi kupambana nalo kunusuru pesa nyingi za watu zinaliwa sasa hivi lakini hongereni sana.

Waheshimiwa Wabunge, hongereni sana kwa michango yenu mizuri sana na nawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni hapa wa ziada wa Mheshimiwa Nape ambao ni Ndugu Stevene Mapunda Mwenyekiti wa *TISPA* karibu, Noah Maena Katibu Mkuu wa *TISPA* vilevile karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la msiba. Katibu wa Bunge anaomba kuwa Ofisi ya Bunge imepata msiba wa mtumishi wake Ndugu Atanas Suli Nsopela (Afisa Hesabu Mwandamizi – Kitengo cha Fedha na Uhasibu) aliyefariki usiku wa kuamkia leo tarehe 19 Mei, 2023 kwa kuugua ghafla. Ofisi

inaendelea kuwasiliana na familia ya marehehemu kuhusu taratibu za mazishi, *"Raha ya Milele Umpe Ee Bwana, na Mwanga wa Milele Umwangazie, Apumzike kwa Amani, Amina"*

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo haya, nahairisha shughuli za Bunge mpaka siku ya jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.06 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 22 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*